Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NANE

### Kikao cha Kumi – Tarehe 26 Juni, 2012

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

### MASWALI NA MAJIBU

Na. 77

### Kodi na Ushuru wa Mazao Madogomadogo

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Wananchi wengi wa vijijini hutozwa kodi na ushuru wa mazao madogomadogo mara wanapopeleka kuyauza mazao magulioni chini ya Sheria Ndogo za Halmashauri za Wilaya:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa huu ni unyanyasaji wa wananchi wa Vijijini?

(b) Je, hali na ushuru wa aina hii unazingatia Sera ya Taifa Utozaji Kodi kwa mtumishi anayelipwa shilingi 100,000/= halipi kodi?

(c) Je, Serikali ipo tayari kuziekeleza Halmashauri zifute kodi hizo zisizo na tija na za kinyanyasaji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na baadhi ya vyanzo vya mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kuonekana kuwa kero *(Nuisance Taxes),* Serikali mwaka 2002 ilitangaza kufuta vyanzo hivyo vya kodi ili kuwaondolea usumbufu wananchi wanaolipa kodi hizo. Aidha, uamuzi huo haukuwa na maana ya kufuta kodi au ushuru wa mazao, badala yake Serikali ilitoa utaratibu wa ukusanyaji wa ushuru wa mazao, badala yake Serikali ilitoa utaratibu wa kukusanya ushuru huo pale zao linapozalishwa (*Payable at Source*). Viwango vinavyotakiwa kutozwa ni kati ya 3% hadi 5% ya bei ya kuuzia mazao hayo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, utozaji wa ushuru katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba unafanywa na mawakala walioteuliwa na Halmashauri kwa kuzingatia Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka

1982 na kwamba anayestahili kulipa ni mfanyabiashara wa mazao hayo na siyo wachuuzi wadogowadogo ambao lengo lao nikujikimu hasa akina mama na vijana.

Serikali inakiri kwamba upo ukiukaji wa utaratibu wa ukusanyaji wa ushuru huo kwa baadhi ya wazabuni kwa kuwatoza ushuru wachuuzi wadogowadogo ambao hawastahili kutozwa ushuru wa vitu vidogovidogo wanavyouza kama mchicha, samaki wa kukaanga, dagaa wanaouzwa kwa mafungu, vichane vya ndizi na kadhalika.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Serikali ilishafuta kodi zote zilizoonekana kuwa kero. Hivyo, naomba kutumia fursa hii kuziagiza Halmashauri zote kutotoza wachuuzi wadogowadogo ushuru wa mazao na badala yake ushuru huo unapaswa kutozwa kwa wafanyabiashara wakubwa wa mazao hayo.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu aliyotoa lakini niseme kwamba hayakidhi.

Kwa kuwa, hawa anaowasema wafanyabiashara ndiyo watozwe kodi, hawa wakiambiwa watoe kodi wanawatoza wachuuzi wadogowadogo ili wao watoe kodi kwanza watozwe wachuuzi wadogowadogo na wakulima ndiyo watoe kodi wao.

Kwa nini Serikali isiamue kwamba chanzo hiki kifutwe kabisa kwa sababu ni kero kwa wakulima na wachuuzi wadogowadogo? Kuna barriers barabarani,

kwenda kwenye magulio wananchi wanasumbuliwa sana na kama tulifuta kodi ya kichwa na kodi ya maendeleo kwa nini basi kodi hii isifutwe kabisa kabisa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jasson S. Rweikiza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ninaomba unisikilize vizuri na Wabunge wanisikilize vizuri. Hapa mimi sitengenezi majibu mapya lakini mimi hapa sitengui torati bali nakuja kuimarisha torati. Ninachozungumza hapa ni sheria ya nchi inavyosema na ninamshukuru sana Mheshimiwa Rweikiza kwamba anazungumzia jambo hili kwa sababu kama nilivyosema katika majibu niliyotoa hapa ni kweli tumecheki na watu waliopo katika maeneo yale na tumekuta kwamba wananchi hawa ambao nimewaeleza hapa ambao wanatengeneza vitumbua, maandazi na samaki wa kukaanga wanatozwa ushuru huu kitu ambacho ni kinyume na sheria tunayoizungumza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema na ninarudia kusema tena hapa kwamba kumtoza mama anayekwenda kuuza mchicha sokoni anauza pale vichane vya ndizi au vitumbua ni makosa kwa sababu sheria inakataza kwa sababu mwaka 2002 tuliondoa jambo hili.

Sasa ninachotaka kusema hapa anakwenda mbele zaidi anazungumza habari inayoitwa *produces* ile ambayo katika hii hotuba iliyopita ambayo tunaifanyia kazi sasa hivi imesema toza 3% hadi 5% nataka niainishe hapa. Yule wa kwanza niliyemsema wa vitumbua hatafuti kitu kinachoitwa faida kibao, yeye anakwenda pale kwa ajili ya kujikimu tu ndiyo anayetoka pale anakwenda kununua utumbo wa taulo na utumbo mdogo, ndiye huyo anayechukua mafuta ya Kandiri na mafuta ya taa anachukua kwenye chupa ya soda nusu huyu hatatakiwa kulipa ushuru wa aina yoyote, lakini ametoka mwanamama amebeba fuso ina kabich ndani yake au mikungu wa ndizi atalipa ushuru.

Hizi *gate* anazozisema hapa hazikuwekwa na Halmashauri bali zimewekwa na Maliasili na Utalii lakini Halmashauri zinachofaya ni kwenda kuchungulia dili tu pale, fuso limekuja hapa? Anasema bwana eeh! Umebeba humu ndani viazi magunia 100 umelipa ushuru? Anakwambia mimi nimetokea Longido pale kwangu Siha, anakwamba bwana nipatie risiti ya Longido. Risiti ya Longido isipotolewa pale kama haipo atalipa ushuru.

Suala sasa la kuondoa huu ushuru, sasa hivi tunazungumzia hotuba ya Waziri Mkuu, linaweza liakaletwa hapa tukalijadili. Lakini tunapoondoa ushuru huu usisahau kwamba tumeziambia Halmashauri zijenge Zahanati katika kila kijiji, tumeziambia zijenge shule katika kila Kata, tumeziambia zijenge shule katika kila Kata, tumeziambia zitengeneze barabara na tunaambiwa kwamba Halmashauri makusanyo yake ni

madogo, Tandahimba inapata bilioni 1.9 kutoka katika Korosho, ukiambiwa futa ndicho kinachosemwa, tufute hapa, sasa wote tuiangalie *implication* yake.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona tatizo la Bukoba Vijijini halina tofauti na Misenyi au Nkenge. Mimi naomba nipate kuelezwa kwa mfano hawa wananchi ambao tunasema hizo *barrier* tunaongelea zilizo kati ya kijiji na kijiji. Kwa mfano kwenye jimbo langu kati ya Kyaka na Kilimilire kuna *barrier*, wakati huohuo mtu huyu unayetaka kumtoza unamwambia achangie shule na hata madawati, ana ndizi moja unaitoza shilingi mia 500 wakati ndizi ni shilingi 2000/=. Tunataka msimamo wa kwa ujumla kwamba katikati ya vijiji na vijiji zisiwepo *barriers* na kama ni kukusanya unaangalia unakusanyaje.

Tutoe mfano kuna mfanyakazi swali langu ni kwamba kama mfanyakazi analipwa 100,000/= na bado hakatwi ushuru, mtu anavuma ndizi ya shilingi 2000/= hiyo ni haki?

**MWENYEKITI:** Nafikiri Mheshimiwa Waziri umeelewa, tusaidie majibu lakini kwa ufupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, lakini naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Assumpter Mchana, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ushuru tunaousema hapa ukiisoma ile sheria wanasema kwamba tunatoza *at source,* na anayetozwa pale ni yule anayenunua yaani mfanyabiashara na siyo mkulima. Najua wafayabiashara wanasema kwamba kuna *implications* zake kama alikuwa ametozwa pale maana yake hata bei atakayokwenda kumpa mkulima itakuwa kwa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwa kifupi hapa kwamba suala la *barrier* nimesema *barrier* siyo za kwetu, Halmashauri yenyewe inayohusika ndiyo inayotakiwa iweke utaratibu mzuri ambayo inafikiri kwamba unafaa kwa ajili ya kutoza ushuru tunaouzungumza hapa. Bado hili ni jambo mbalo tunaweza tukalizungumza sisi wote kwa pamoja lakini pia kwamba ni *complication* ipi inayojitokeza katika kutoza ushuru huu.

Ninachotaka kusaidia hapa ni kusema kwamba kama hizo *barrier* zinaleta matatizo Halmashauri sasa iseme kwamba itafanyaje, inaweza kwenye *source* au kule ambapo wanauza yale mazao wakapata data lakini habari tulizonazo ni kwamba wakati mwingine wanadanganya na wakati mwingine hawakwambii kweli, sasa hilo ndiyo tatizo na mjue kwamba Halmashauri kama haikutoza ukaacha kwa mfano mtu aliyepo Ulanga hakutoza ikifika Kilombero basi Kilombero watatoza na watajenga shule lakini Ulanga itakuwa imekosa. (*Makofi*)

Na. 78

## Mshahara kwa Waajiriwa Wapya

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA** aliuliza:-

Je, ni kwa nini waajiriwa wapya Serikalini wanafanya kazi zaidi ya miezi mitatu bila kulipwa mshahara?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kabla ya mwezi Oktoba, 2011 wapo Watumishi wapya ambao walikaa muda mrefu bila kupata mishahara kutokana na sababu zifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kabla ya mwezi Oktoba, 2011 wapo Watumisi wapya ambao walikaa muda mrefu bila kupata mishahara kutokana na sababu zifuatazo:-

(i)Waajiri kuchelewa kuwasilisha taarifa muhimu za kiutumishi ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya kuhakikiwa na kupelekwa Hazina.

(ii)Waajri kuwa na tabia ya kusubiri hadi watakapopokea taarifa za Watumishi wengi au watakapopata idadi kubwa ya watumish8i ndipo

wapeleke taarifa hizo ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kukwepa gharama za usafiri.

(iii)Watumishi ambao taarifa zao zilikuwa na matatizo kama kukosa vyeti kuchukua muda mrefu kupatikana kwa kuzingatia ukubwa wa nchi yetu, na (iv)Watumishi kutoripoti vituo wanavyopangiwa au kuchelewa kuripoti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua uzito wa tatizo hili kuanzia Oktoba, 2011 imeanza kutumia mfumo Shirikishi wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara *(Human Capital Management Information System (HCMIS)* ambapo mfumo huu umepelekwa kwa waajiri wote nchini yaani Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakala wa Serikali, Taasisi za Umma na Sekretarieti za Mikoa Tanzania Bara. Kwa kutumia mfumo huu waajiri wamepewa fursa ya kuingiza taarifa za mtumishi mara tu anaporipoti kazini. Aidha, mfumo huu unamwezesha mwajiri kusimamia na kufanya marekebisho ya orodha ya malipo ya m shahara *payroll* moja kwa moja na hivyo kuimarisha uwajibikaji na usimamizi wa masuala ya kiutumishi na kuongeza kasi ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ya mfumo huu wa *HCMIS* yamekwisha tolewa kwa maafisa Utumishi na Maafisa Tawala zaidi ya 616 kuhusu namna ya kuutumia mfumo, kupata mrejesho (*Feedback*) kwa kazi walizofanya na kuandaa taarifa mbalimbali kutoka katika mfumo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ambazo zimepatikana kutokana na matumizi ya mfumo huu kwa kipindi cha miezi saba iliyopita ni pamoja na kuwaingiza watumishi wapya kwenye mfumo palepale alipo mwajiri mara mtumishi anaporipoti kama atakuwa na vielelezo muhimu vinavyohusiana na elimu na sifa alizonazo ambapo kuanzia mwezi Oktoba, 2011 hadi Mei, 2012 jumla ya watumishi wapya 35,018 wameingizwa kwenye *payroll* ya Serikali na wanapata mishahara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kuanzia tarehe 1 Julai, 2011 mpaka 31 Mei, 2012 jumla ya Watumishi wa Serikali 12,547 wamefutwa katika orodha ya malipo ya mishahara ya Serikali *payroll* kutokana kufukuzwa kazi Watumishi 4,561, kustaafu kwa mujibu wa sheria watumishi 5,757 na watumishi 2,239 baada ya kufariki.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawil ya nyongeza.

Kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kumeanzishwa mfumo huu ambao utasaidia kuweka kumbukumbu vizuri lakini pia Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba kuna baadhi ya watumishi na watendaji wetu Serikalini ni wazembe kutokana na sababu alizozitoa. Je, Mheshimiwa waziri anasemaje kuhusiana na kusimamia kwa umakini mkubwa mkakati huu ili matokeo kama hayo yasitokee tena na adhabu gani watapewa hao watumishi ambao watakuwa na

taratibu zilezile za kuchelewesha mishahara ya wafanyakazi?

Pili, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba mfumo huu umeanzishwa tangu Oktoba 2011, lakini kuna waajiriwa ambao wameajiriwa mwezi wa kwanza mwaka 2012 na walichukua miezi mitatu bila kupata mishahara wapo vijijini wanaishi katika mazingira magumu hawana pa kulala wala chakula. Mheshimiwa Waziri analiambiaje Bunge lako Tukufu wakati tayari mfumo huu ulishaanzishwa? Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mwalimu Riziki kama ifuatavyo:-

Mfumo huu ulianzishwa tunaufutilia kwa karibu sana na kama kuna hitilafu yoyote ni kama nilivyoeleza jana kwamba mara nyingi watumishi wanapopangiwa sehemu mbalimbali kwa mfano walimu wengi huwa wanachelewa kuripoti na wengine huwa wanakwenda kituo ambacho hajapangiwa. Kwa mtumishi ambaye anakwenda kituo ambacho hajapangiwa kwa mfano jina lake lipo Kigoma na sisi tumeshapeleka mambo yake ya mishahara Kigoma, akiripoti sehemu nyingine ili kubadilisha sehemu nyingine inaweza ikachukua miezi mitatu au sita. Hilo ndilo linalotokea kwa kiasi kikubwa, watumishi hawaendi sehemu walizopangiwa wanajibadilisha wao wenyewe. Lakini sisi tunasema kwamba tunafuatilia kwa karibu sana kwa yule mtumishi ambaye anaripoti kwa wakati anaweka

vielelezo vyake tunatoa *feedback* haraka sana na wanalipwa haraka sana. Kinachosababisha ucheleweshaji ni kama nilivyoongea jana kwamba mtumishi anaweza akaripoti baada ya tarehe 15, akiripoti baada ya tarehe 15 lazima atakwenda mwezi unaofuata kwa sababu *payroll processing* mwisho wake ni tarehe 15 ya mwezi husika.

Kwa wale watumishi ambao amesema kwamba walikuwa hawajaingizwa kwenye *payroll* na mfumo huu ulikuwa tayari umeshaanzishwa, ni kama nilivyojibu jana kwamba kulikuwa na watumishi 205 ambao hawakupata mshahara mwezi wa tano na sababu za msingi ni kama nilivyosema kwamba ni kukosekana kwa vielelezo pamoja na kwamba walikuwa wameripoti baada ya tarehe 15. Lakini nimhakikishie mheshimiwa Riziki kwamba mfumo huu ni mzuri na unakwenda vizuri na unawasaidia watumishi kupata malimbikizo yao pamoja na kupata mishahara kwa haraka wanaporipoti kazini.

**MHE. J0HN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mfumo unaweza kuwa ni mzuri lakini Mheshimiwa Waziri amesema kwamba changamoto kubwa ni kwamba waajiri wengine hawaingizi taarifa kwa wakati kwenye huo mfumo na mfumo bila taarifa hauwezi kufanya kazi inayostahili. Ninapenda kupata kauli ya Waziri kwamba ni hatua zipi sasa ambazo ofisi ya Rais inachukua kuwawajibisha waajiri wanaochelewesha kuingiza taarifa na hatimaye kuanzisha mgogoro kati ya wafanyakazi na Serikali?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John J. Mnyika, kama ifuatavyo:-

Mfumo wowote unapoanzishwa huwa mara nyingi una changamoto zake. Changamoto mojawapo ni baadhi ya Waajiri ambao hawaja- *catch up* vizuri ku-*feed* zile *information*. Kwa hiyo, hao huwa tunawaita na tunawapa tena *training* kwa hiyo sasa hivi hakuna mgogoro sana.

Baadhi ya sehemu ule mfumo kila unapofungwa unaathiriwa na mambo mbalimbali. Mfano ni Wilaya za Ulanga na Ludewa kila wanapofunga ule mfumo unapigwa na radi.

Kwa hiyo, tunatafuta namna bora ya kuhakikisha na wao tunawafungia *system* ambayo itahimili mikiki mikiki ya aina yoyote. Lakini mpaka sasa hivi waajiri wengi wanakwenda vizuri.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata linaenda Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Lakini kwa taarifa rasmi niliyopewa na kuandikiwa hapa mezani, swali hilo majibu yake bado hayajakamilika na

yatakapokuwa yamekamilika litawekwa tena katika ratiba ya kazi siku itakapokuwa imepangwa.

Kwa hiyo, swali hilo leo halitajibiwa na hivyo tunaendelea na swali linalofuata mbalo linaenda Wizara ya mambo ya Ndani ya Nchi na linaulizwa na Mheshimiwa Mussa Mzee, Mbunge wa Jang'ombe.

Na. 80

**Wizi Kwa N jia ya Mtandao**

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE** aliuliza:-

Maendeleo ya Kiteknolojia yameleta uhalifu wa kimtandao:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimeripotiwa Polisi kutokana na wizi wa kwa njia ya mtandao?

(b) Je, Serikali imejipanga vipi kudhibiti wizi wa mtandao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mbunge wa Jang'ombe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa kiasi kilichoripotiwa Polisi kuhusiana na wizi wa njia ya

mtandao hapa nchini ni Tshs bilioni 1.3 *EURO* 8,897 na *USD 551,777.*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetunga Sheria ya *Electronic and Postal Communications Act*, 2010 na Sheria ya kudhibiti fedha haramu (*The Anti - Money Laundering Act – 2006* ambayo pia ilifanyiwa marekebisho mwaka huu, 2012. Aidha, Serikali kupitia vyombo mbalimbali vya dola kama vile Polisi, Taasisi za Fedha, Vyombo vya Habari, *TRA* na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imejiwekea mikakati ya kuelimisha wananchi kuhusiana na aina hii ya uhalifu wa Kimtandao na jinsi ya kupambana nao. Jeshi la Polisi limeanzisha kitengo mahususi cha makosa ya kimtandao (*Cyber Crime Unit*) ambacho kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kinafanya kazi ziafuatazo:-

1. Kutoa tahadhari kwa taasisi za kifedha ili ziweke ulinzi na salama madhubuti (*password security*) kwa wateja wao na kuimarisha mitambo ya usalama ya mabenki na taasisi nyingine za kifedha.

2. Kujenga uwezo wa kutoa mafunzo kwa askari polisi wapatao 250 ambao wametawanywa mikoa yote nchini ili kukabiliana na vitendo vya uhalifu kwa njia ya mtandao.

3. Kubaini, kufuatilia, kuzuia na kupeleleza uhalifu na makosa mbalimbali ya kimtandao.

4. Kutoe elimu ya tahadhari kwa wananchi kupitia vyombo mbalimbali vya habari na majarida juu ya uhalifu huu mpya.

5. Kufanya doria katika mitandao (*Online Patrol*) ya kifedha na mitandao mingine kwa mujibu wa sheria ili kubaini makosa ya aina hiyo.

6. Kupitia sheria ya kudhibiti mifumo haramu ya kifedha na mawasiliano, kitengo cha intelijensia (*Fianncial Intelligence Unit*) kimepewa mamlaka ya kufuatilia maingizo yoyote ya fedha yanayotiliwa mashaka (*Dubious Transaction*).

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninashukuru kwa majibu mazuri aliyonipa Mheshimiwa Waziri. Naomba niulize maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Je, wahalifu wangapi wamekamatwa kuhusiana na wizi wa fedha hizo?

(ii) Je, Serikali haioni haja sasa ya kuanzisha Sheria ya Wizi wa Mtandao *(Cyber Law)?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umemsikia?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Kidogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mzee naomba urudie maswali yako naona kidogo haujasikika, ama ubadilishe mic au uongeze sauti.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

(i) Je, wahalifu wangapi wamekamatwa kuhusiana na wizi wa fedha hizo?

(ii) Je, Serikali haioni kwamba kuna haja sasa ya kuanzisha Sheria ya Wizi wa Mtandao *(Cyber Law)?*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wahalifu 320 walikamatwa kuanzia Januari hadi Desemba mwaka jana 2011. Katika mwaka huu wahalifu 230 wamekamatwa kuanzia Januari hadi mwezi Mei, 2012.

Kuhusu swali lake la pili Serikali itazingatia ushauri wa kuanzisha *Cyber Law* ili kuhakikisha kwamba, wizi huu unadhibitiwa nchini. *(Makofi)*

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, anafikiria hawa askari 250 waliopata mafunzo wanatosha?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, askari 250 hawatoshi, lakini Serikali ina mpango wa kuendelea kutoa mafunzo kwa askari zaidi na kuwapatia vitendeakazi ili wizi wa namna hii udhibitiwe kabisa nchini. Aidha, kutakuwa na ushirikiano wa Kimataifa ambao utasaidia pia katika kujenga uwezo wa watu wetu.

Na. 81

**Matumizi Mabaya ya Silaha kwa Askari Polisi**

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA** aliuliza:-

Hivi karibuni kumejitokeza matukio ya Askari Polisi kutumia silaha wanazokabidhiwa kuwapiga raia wema

risasi hasa wakati wa doria au shughuli za kawaida na kusababisha vifo au kuwaumiza kwa makusudi:-

Je, Serikali inatoa tamko gani la haraka juu ya matumizi mabaya ya silaha hasa kwa askari ambao wanaonekana si walinzi wa amani bali ni wahalifu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimia Mwenyekiti, matumizi ya silaha za moto kwa Jeshi la Polisi hutawaliwa na sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza jeshi hilo. Kifungu cha 29 (1) & (2) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi (*The Police Force and Auxiliary Police Service Act*) Sura 322 na Kifungu cha 21 (1) & (2) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (*The Crimina Procedure Act*) Sura ya 20 sambamba na Kanuni za Kudumu za Jeshi la Polisi *(PGO 274)* vinampa askari Polisi uwezo wa kisheria wa kutumia silaha anapokuwa katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, askari Polisi haruhusiwi kutumia silaha hizo kinyume cha sheria na kusababisha vifo au madhara mengine kwa raia wema. Serikali imekuwa ikichukua na itaendelea kuwachukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi na kufikishwa mahakamani askari wote

watakaobainika kutumia vibaya silaha wanazokabidhiwa wakiwa kazini. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mafupi ambayo sijaridhika nayo, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa mauaji mengi yanahusisha askari Polisi yamekuwa yakihusiana na masuala ya kisiasa hususan wananchi wanapokuwa katika mikusanyiko yao ya amani bila silaha yoyote, wanavamiwa na Polisi na kuawa.

Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kurejea sheria na kanuni zake zinazompa askari Polisi uwezo wa kutumia silaha anapokuwa anatekeleza majukumu yake hata kama si halali kama haya ya kuua raia wema hovyo?

(ii)Je, Jeshi la Polisi lina kitengo maalum ya kuchunguza askari wanaojihusisha na uhalifu wa kutumia silaha kuua raia wema kama hivi ambavyo tumesikia matukio mengi yakiendelea nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, sheria na taratibu ambazo zinamwezesha askari kutumia silaha zinamkataza mara zote kutumia silaha ya moto bila ya sababu. Hata hivyo, kwa sababu kuna mazingira maalum, maelekezo yako mengi sana kwa jeshi la Polisi namna ya kutazama *circumstances* ambazo zinaweza zikabadilika katika ku-*contain* tatizo fulani.

Kwa hiyo, sheria bado zinaonekana zinakidhi kwa sababu siku zote askari hawaambiwi ku-*shoot* na wanashauriwa kutumia *minimum force* isipokuwa ikitokea *escarlation* nao inabidi wa-*escarlet forces*. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili ni kwamba, Polisi ina kitengo cha kuchunguza mauji na madhara yanapotokea mara tu kitengo hiki kinapopewa taarifa hatua za upelelezi zinaanza na ndizo zinazochukuliwa au askari kusimamishwa kazi au kufukuzwa kabisa au shauri hilo kupelekwa Mahakamani.

**MHE. FAIDA M. BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa, kuna baadhi ya wahalifu hapa nchini wanatumia nguo, vyeo na silaha za askari Polisi na kufanya uhalifu sehemu mbalimbali kwa kujifanya kama wao ni Polisi.

Je, Serikali inauchukulia hatua gani mtandao huu ili kukomesha uhalifu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kujifanya kuwa ni askari Polisi ni kosa la jinai na pale inapogunduliwa basi mhusika huchukuliwa hatua za kisheria kama Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai zinavyotaka. *(Makofi)*

Na. 82

**Mahakama ya Nyamikoma Kujengwa Upya**

**MHE. RICHARD M. NDASSA** aliuliza:-

Serikali iliahidi kujenga upya Mahakama ya Mwanzo ya Nyamikoma, Wilayani Kwimba, ambayo haijakarabatiwa kwa muda mrefu.

Je, ni lini Mahakama hiyo kongwe itajengwa upya?

**NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria kwa ridhaa yako naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali iliahidi kujenga upya Mahakama ya Mwanzo ya Nyamikoma iliyoko katika wilaya ya Kwimba ambayo haijakarabatiwa kwa muda mrefu na imechakaa sana. Aidha, ni lengo la Serikali kujenga na kukarabati majengo yote ya Mahakama ambayo yanahitaji aidha kujengwa upya au kukarabatiwa lakini kutokana na ufinyu wa bajeti Serikali imeshindwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, Mahakama ya Mwanzo ya Nyamikoma itatengewa fedha za ujenzi katika Bajeti ya fedha ya mwaka 2013/2014 kupitia fedha za ndani.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Waziri nilikuwa naomba nipate maelezo ya ziada kwa sababu Serikali imeishatoa ahadi siku nyingi tangu enzi za Waziri Mwapachu, akaja Mama Nagu, akaja

Chikawe I, akaja Kombani na sasa Chikawe II. (*Kicheko*)

(i) Naomba nihakikishiwe ni kweli fedha zitatengwa kwa mwaka ujao wa fedha?

(ii) Lakini maoteo ni shilingi ngapi zitatengwa?

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, sijui ulikuwa unamaanisha nini hiyo Chikawe I na II lakini nadhani Chikawe I ni pale Chikawe alipokuwa Waziri mara ya kwanza na II ni pale aliporudishwa kuwa Waziri kwa mara ya pili. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ukizingatia Chikawe I na II. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza Mheshimiwa Mbunge anataka Serikali imthibitishie endapo jengo hili ambalo limekuwa likiahidiwa tangu enzi za Chikawe I na sasa Chikawe II, nimhakikishie tu kwamba ni kweli jengo hili litajengwa na pia nimhakikishie tu kwamba hapatakuwa na Kairuki II.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la Pili nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba gharama za ujenzi zitategemea tathmini ya Wakala wa Majengo *(TBA)* kwa kuzingatia mwongozo wa ramani za ujenzi wa Mahakama za Mwanzo Tanzania ambapo hata katika wilaya la Kwimba ramani hiyo wanayo.

Hata hivyo, kuhusiana na maoteo ya gharama za ujenzi Mahakama hizi zimekuwa zikichukua takribani kati ya shilingi milioni 300 mpaka 600 kwani hivi sasa ni mpango wa Serikali kwamba popote linapojengwa

jengo la Mahakama basi tunajenga pia na nyumba ya Mahakimu. Lakini kwa uzoefu tu wa haraka haraka katika Mahakama ambazo tumezimaliza hivi karibuni Mahakama ya Lugoba iligharimu takribani shilingi milioni 490. Hata hivyo, kwa Mahakama ya Nyamikoma Kwimba wao wanazo tayari nyumba za Mahakimu tano (5). Kwa hiyo itategemea na tathmini kuangalia nyumba zile tano endapo zitahitaji kujengwa upya au kukarabatiwa. Ahsante sana.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wakati wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, Serikali iliahidi kujenga Mahakama Mpya ya Mwanzo Kawe, lakini mwaka ndio unaisha na hakuna dalili yoyote ya ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Kawe. Sasa nataka Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie mchakato wa Mahakama ya Mwanzo umeishia wapi.

**NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa ni kweli ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo ya Kawe ulikuwepo katika Mahakama 20 za mwanzo ambazo tulitarajia kama Serikali tutazijenga. Lakini kutokana na kutegemea fedha za Wafadhili, Wafadhili wale walipunguza misaada na ndiyo maana tulishindwa kujenga Mahakama hiyo. Lakini napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika mwaka huu wa fedha tumepata nyongeza kidogo ya bilioni 11.5 na Mahakama hii ya mwanzo iko katika mpango na hata wakati wa Kamati tulimfahamisha hilo Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Kwanza kabla ya kuuliza swali la nyongeza naomba kwa ridhaa yako niwape pole Mwenyekiti wangu wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Korogwe Mjini, Meya wa Mji wa Tanga, ambao walipata ajali jana wakiwa wanakwenda kwenye kikao kule Same.

Baada ya hapo naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, tatizo la Nyamikoma Wilaya ya Kwimba linafanana na tatizo la pale Mkomazi katika Tarafa ya Mombo ambapo limekaa kwa zaidi ya miaka saba(7). Je, Serikali inaniambia nini kuhusiana na kujenga Mahakama ya Mwanzo katika Kata ya Mkomazi?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka wa fedha kupitia Programmu ya maboresho ya sekta ya sheria, Mahakama hii ya Mwanzo ya Mkomazi ni moja kati ya Mahakama ambazo zitajengwa kupitia mradi huu. Lakini katika mradi huo tunatarajia pia kujenga Mahakama zingine nne ambazo ni Mahakama ya Kilindi, Mahakama ya Kisarawe Mjini, Mahakama ya Gairo pamoja na Mahakama zingine mbili. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri na Mahakama ya kule Mpitimbi imekamilika tunawashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata kwa ajili ya muda. Sasa swali hilo linaelekezwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na litaulizwa na Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum. Kwa niaba yake namwona Mheshimiwa Mariam Kasembe atauliza kwa niaba ya Mheshimiwa Wambura.

Na. 83

**Wanawake Wanaolima Uyoga Mtwara**

**MHE. MARIAM R. KASEMBE (K.n.y. MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA)** aliuliza:-

Akina Mama wa Mkoa wa Mtwara wamehamasika sana na Kilimo cha Uyoga kwa ajili ya chakula na kujipatia kipato:-

Je, *Program* ya Kilimo Kwanza imewasaidiaje kina Mama hao ili kuhakikisha kuwa kilimo cha zao hilo kinakuwa endelevu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mtwara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa na mkakati wa muda mrefu wa kuwahamasisha wananchi wanaoishi kwa kutegemea kilimo kuwa na mfumo wa kubuni zao mbadala la biashara ili kuwa na msaada kwa zao kuu, haswa pale ambapo matatizo ya uzalishaji kama maradhi, au matatizo ya soko mfano kuporomoka kwa bei kunapotokea . Hali hii inaathiri sana mapato na maisha ya wananchi hawa. Zao la uyoga ni zao ambalo limethibitika kustawi katika mazingira ya mkoa wa Mtwara ambapo zao kuu ni korosho. Aidha, zao la uyoga likikidhi viwango vya soko, lina nafasi kubwa ya kuongeza mapato ya wakulima wa zao hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kulitambua hilo, kupitia wataalam wa Halmashauri za Wilaya Mkoani Mtwara imekuwa ikitoa mafunzo na ushauri wa kitaalam kwenye vikundi vya wakulima wa uyoga juu ya uzalishaji bora wa zao hilo. Aidha, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine *(SUA)* kwa kushirikiana na Kituo cha Utafiti wa Kilimo-Naliendele walitoa mafunzo ya uzalishaji wa uyoga kwa vikundi 2 vya Ndanda na Amkeni-Masasi ili nao waweze kutoa mafunzo kwa vikundi vingine. Vikundi hivi pia vilipewa vifaa na jengo la kuzalishia uyoga. Aidha, Mkoa wa Mtwara uligharamia mafunzo ya Mjasiliamali mmoja wa Uyoga yaliyofanyika Dar es Salaam kama njia ya kupanua elimu zaidi juu ya kilimo hicho. Vikundi vya wakulima wa uyoga vimekuwa vikishiriki maonesho mbalimbali ya kilimo kama yale ya Nanenane na yanayoandaliwa na *SIDO* ili kutambulika na kujifunza zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa uzalishaji wa uyoga kwa mkoa wa Mtwara si wa kuridhisha sana kutokana na changamoto mbalimbali kama vile hali ya joto kali kipindi cha kiangazi, uhaba wa pembejeo kama mbegu bora, mifuko ya plastiki, upungufu wa maji ya kunyunyizia (*drip irrigation),* vilevile changamoto hizi zinapelekea mwamko mdogo kwenye kilimo hiki. Kwa kuwa zao hili ni muhimu kama nilivyoeleza, Wizara yangu itaendelea kufanya kazi kwa karibu na Mkoa na Halmashauri zake kutoa kipaumbele kwa zao hili kwa kuhamasisha na kuwapatia vikundi vya uzalishaji mafunzo huduma nyingine kadri itakavyowezekana ili kuhakikisha zao hili linakuwa endelevu na kufikia malengo ya zao mbadala kama nilivyoeleza hapo juu. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa katika majibu ya msingi Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba hawa wakulima wa uyoga wamekuwa wakipata shida ya kupata mbegu bora. Je, Serikali iko tayari sasa kuwapa mafunzo wakulima hao wa uyoga ya kutengeneza mbegu bora ili wawe wanatengeneza mbegu wenyewe ili kupunguza safari za kufuata mbegu hiyo Dar es Salaam?

Swali la pili, kwa kuwa soko la uyoga liko ndani na nje ya nchi. Je, Mheshimiwa Waziri anawasaidiaje wakulima hao wa uyoga kuwapatia fedha kama mikopo ili waweze kuzalisha kiasi cha kutosha na

kuweza kusafirisha uyoga huo nje ili na wao waweze kupata fedha za kigeni ?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema Wizara yangu kimsingi imeandaa mkakati ambao utawahamasisha wakulima hawa kwenye vikundi vyao ili waweze kuzalisha uyoga. Lazima niseme uyoga ambao tunauzalisha sisi hapa Tanzania sanasana ni uyoga wa aina moja. Lakini kimsingi kuna uyoga kama za aina sita kwa mahitaji mbalimbali. Kuna uyoga ambao ni wa kula, kuna uyoga ambao ni wa dawa, kuna uyoga ambao ni maarufu sana huko duniani ambao unajulikana sana kwamba nao unaboresha sana miili ya akinababa na unajenga mahusiano ya wanandoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo uyoga ni zao ambalo lina soko kubwa sanasana. Kwa hiyo, naomba niseme tu kwamba sio kuwahamasisha vikundi kwenye suala la mbegu tu, lakini pia kwenye kujaribu kupata masoko ya uyoga ya aina mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu tuna mkakati pale kwenye Idara ya kuhamasisha mazao haya ambayo unajenga uwezo wa kukopesheka vikundi hivi.

Kwa hiyo, tunapenda kuwaambia vikundi hivi kwamba tuwasiliane nao ili tuweze kuwaandalia na tunaweza tukasaidia pia kuwatengenezea *write ups* ambazo zinaweza kujenga uwezo wa kukopesheka

kupitia mafungu kama *Food Aid Counterpart Fund* na Mabenki. Masoko yako mengi kusema kweli Afrika ya Kusini, Ufaransa na Uingereza yote yanataka uyoga kutoka Tanzania lakini sisi kwa sababu tunazalisha tani 50 tu kwa mwaka bado hatujakidhi viwango hivyo. Lakini naomba nifungue milango kwa ajili ya vikundi hivi kufika Wizarani.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru kwa majibu ingawa nadhani aina hizo za uyoga labda ungeandaa semina maalum kwa Wabunge ili waweze kuelewa zaidi, naomba sasa nimwite Mheshimiwa James Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa wakulima wa Wilaya ya Masasi na Nanyumbu katika vikundi vyao wameanza kulima zao hili la uyoga na sifa kemkem ambazo zimetolewa kwenye zao hili la uyoga. Je, Serikali imeweka utaratibu gani ambao ni endelevu kwa kuwa wakulima hawa wanafanya kilimo kwa kubahatisha kwenye uyoga, karanga, ufuta, korosho wanakuwa hawana uendelevu wa mazao yao haya Kwa vile wanayafanya kubahatisha wakati soko ni la kusuasua au hawana maelekezo sahihi ya kupatiwa soko kutokana na teknolojia ya kisasa iliyopo na Serikali inavyo vyombo vya kuhakikisha masoko yako maeneo gani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niliposema kwenye majibu yangu yale ya awali kwamba suala la soko la zao la

uyoga halina mashaka ndani na nje ya nchi. Tatizo linalokidhi hapa ni kwamba *as with all products* lazima lile zao lenyewe likidhi vile viwango vya soko. Sasa soko la ndani ya nchi hapa kwetu Tanzania kwa sasa hivi linajielekeza kwenye soko la namna fulani. Lakini kama tukisambaza elimu hii kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Afya zao la uyoga litapata matumizi makubwa zaidi kwa sababu ni zao kama nilivyosema lina matumizi na manufaa mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hili la masoko ya nje, masoko ya nje yapo tu na yanadai kupata uyoga, lakini hatujakidhi viwango hivyo. Sasa hivi katika mambo ambayo tunayafanya ni kuboresha hivi vikundi vimefundishwa namna ya kutengeneza mabanda hayo ya uyoga. Kusema kweli ni uwekezaji kama wa shilingi milioni moja na nusu lakini baada ya hapo unavuna uyoga mara nane mpaka mara kumi na faida yake zinakwenda kwa makadirio kama shilingi milioni kumi mpaka milioni kumi na mbili. *Ishallah,* hilo ndilo jambo kubwa ambalo Wizara yangu inataka kufanya sasa hivi ili wakulima wajue kwamba pamoja na changamoto hizo bado wakijikita kwenye kilimo ambacho kinaelekezwa vizuri ni zao ambalo lina mafao lina manufaa makubwa kiuchumi. *(Makofi)*

**MHE. ESTER AMOS BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kwa sababu vijana wa mkoa wa Mtwara wamehamasika sana na kilimo cha uyoga na hii wameona ni njia mojawapo ya kuweza kujipatia ajira na kujikwamua kiuchumi. Je, Serikali imetenga kiasi gani katika mwaka huu wa

fedha kuwawezesha vijana wa Mtwara walime kilimo cha uyoga cha kisasa na kuwawezesha kuvuna uyoga kwa wingi na kujikwamua kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichosema ni kwamba kwanza hivi vikundi vinalima uyoga kwa njia ya hiari. Ni hiari yao ni *option* yao kulima uyoga. Sasa na sisi kama Wizara kwa sababu tunajua kwamba kile kilimo kina manufaa mapana tunawahamasisha wakulima. Lakini njia bora ya kuhamasisha kulima ni lazima waingie kwenye vikundi, kwa sababu hapo ndio unatoa elimu ile na fikra iliyopo ni kwamba tunapoelimisha kikundi kimoja nacho kinaenda kuelimisha vikundi vingine na ndivyo ilivyotokea kwenye kikundi cha Amkeni-Masasi, tumewaelimisha wao na wao wamekwenda kuelimisha vikundi vingine vinne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilichosema ni kwamba kuna *Fund* kama *Food Aid Counterpart Fund* na zingine. Vikundi hivi vikija na maelezo ambayo yanaonekana kabisa kwamba hawa wanaweza kukopesheka au wanaweza kupatiwa mitaji na ikawasaidia, Wizara yangu itaingilia kati katika kuwafungulia hiyo milango. Kwanza hiyo *Food Aid Counterpart Fund,* lakini pia kuwapa misingi kama hiyo ya *write up* na maelekezo ambayo yanawawezesha kukopesheka katika taasisi hizo za kifedha.

Na. 84

## Ajira Katika Majeshi Nchini

**MHE. SALUM K. BARWANY** aliuliza:-

(a) Je, ni vigezo gani vinatakiwa na vinavyotumiwa ili kuajiriwa katika Majeshi yetu (JWTZ), Polisi na Magereza?

(b) Je, ni nani anayehusika na mchakato wa ajira za Majeshi hayo katika ngazi ya Mkoa na Wilaya?

(c) Je, ni vijana wangapi waliosailiwa na kupata ajira katika Majeshi hayo kutoka Mkoa wa Lindi mwaka 2011/2012?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mbunge wa Lindi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania linaajiri vijana kwa kuzingatia sifa kadhaa. Kijana anayeajiriwa na Jeshi la Ulinzi anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

(1) Awe raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, (2) Awe na umri kati ya miaka 18 hadi 23. Vijana waliopitia Jeshi la Kujenga Taifa miaka miwili,

wanatakiwa wawe na umri kati ya miaka 18 hadi 25, (3) Awe na afya njema na akili timamu, (4) Awe hajaoa/kuolewa na asiwe na mtoto, (5) Awe mwenye nidhamu na hajapatikana na hatia yoyote mahakamani wala kufungwa, (6) Awe amefaulu masomo ya elimu ya kidato cha nne na kuendelea, (7) Awe na cheti halisi cha kuzaliwa na cheti halisi cha kufaulu masomo ya Kidato cha nne na kuendelea.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeacha utaratibu wa zamani wa kuajiri askari wapya kutoka mikoani na Wilayani. Hivi sasa Jeshi linaajiri askari wapya kutoka katika Jeshi la Kujenga Taifa au Jeshi la Kujenga Uchumi kwa upande wa Zanazibar. Jeshi la Wananchi limeamua kutumia utaratibu huu wa kuwaajiri vijana kutoka JKT au JKU moja kwa moja ili liweze kupata fursa ya kutosha kuchunguza tabia na ujasiri wa vijana kabla ya kuwaajiri.

(c)Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania halikuajiri vijana katika kipindi cha mwaka 2011/2012 kama alivyouliza Mheshimiwa Mbunge. Hata hivyo, JKT limewaandikisha vijana 115 kutoka Mkoa wa Lindi ambao hivi sasa wako makambini wakiendelea na mafunzo ya JKT. Jeshi la Kujenga Taifa hutoa nafasi kwa vijana kutoka kwenye Mikoa yote ya Tanzania kujiunga na JKT ili kujenga umoja na mshikamano wa Kitaifa.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Historia ya Majeshi yetu kabla na baada ya uhuru ilionekana kwamba yanatoka katika

maeneo fulani ndani ya Taifa letu. Kwa utaratibu huu mpya, ambao Jeshi la Ulinzi unaanzisha katika kuwaajiri vijana wetu huoni kwamba tunaweza tukapoteza sura ya Jeshi letu kuwa sura ya Kitaifa kwani bado kuna malalamiko mengi katika nchi yetu kwamba vijana wetu hawapati fursa hiyo, hilo la kwanza.

La pili, kwa sababu Zanzibar JKU hawachukui vijana sasa hivi katika Jeshi la Kujenga Uchumi. Je, ni dhahiri kabisa kwamba Zanzibar hakutokuwa na vijana ambao wanajiunga na Jeshi la Wananchi wa Tanzania? (*Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala lake la kwanza aliuliza kwamba kwa utaratibu wa sasa je, hatuwezi kuendelea na ule utaratibu wa zamani kwamba baadhi ya watu katika maeneo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hawakupata nafasi ya kuajiriwa katika Jeshi la Ulinzi.

Mimi nasema utaratibu ambao tunautumia sasa ni utaratibu mzuri. Kama nilivyosema katika maelezo yangu ya majibu ya msingi nilisema utaratibu ambao tunautumia sasa hivi ni kwamba tunawachukua vijana ambao wanajiunga na JKT kupitia mikoa yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa maana hiyo tukitoa fursa hiyo inatuhakikishia kwamba wakati wa kuwapima vijana, vijana wote katika mikoa yote watapata fursa hiyo ili mradi kama wanazo sifa kama nilivyosema, wawe na sifa ya msingi, wawe na umri kati ya miaka 18 na 23, wawe na akili timamu, wawe na nidhamu. Sasa kama sifa za msingi wanakidhi basi bila

shaka nina hakika sasa ule utaratibu wa zamani pengine tulipokuwa tunaona kwamba ni vijana tu kutoka baadhi ya maeneo mengine ndio waliokuwa wanapata fursa kwa utaratibu huu wa sasa tukiusimamia vizuri nina hakika kwamba wananchi wote wa mikoa yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watapata fursa hiyo.

Lakini swali la pili ni kwamba anasema sasa hivi vijana wa Zanzibar hawajiungi na Jeshi la Kujenga Uchumi, sijui taarifa hizi Mheshimiwa Mbunge amezipata wapi kwa sababu, mimi nilikuwa Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi kwa kipindi cha miaka kumi. Novemba 2000 hadi Oktoba 2010, nakijua kilichokuwa kinaendelea. Sasa katika kipindi hiki cha miaka miwili bado nimekuwa kwenye Wizara ambazo zinashughulikia masuala ya ulinzi na usalama kwa pande mbili zote za Muungano. Kwa hiyo, ninajua kile kinachoendelea. Hata hivi karibuni tarehe 8 Juni, 2012 nilipata nafasi ya kukutana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Dkt. Mwinyi, ambaye anashughulikia masuala ya vikosi vya SMZ, bado alinieleza kwamba suala hili la vijana kwenda JKU bado linaendelea. Sasa nasikitika sana Mheshimiwa Mbunge sijui taarifa hizi amezipata wapi.

Lakini sehemu ya pili, sisi tunapowachukua vijana wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kujiunga katika JKT tunatoa nafasi pia kwa Zanzibar. Hivi juzi kama wiki mbili, tatu zilizopita tulipewa nafasi 300 kwa vijana wa Zanzibar kwa ajili ya kujiunga na JKT. Sasa wale ambao hawatapata fursa ya moja kwa moja kujiunga na JKU Zanzibar watapata nafasi kuja kujiunga na JKT hapa

Tanzania Bara na kwa maana hiyo naona kwamba tutatoa fursa kwa pande zote mbili za Muungano kuwa vijana ambao wanatamani kujiunga na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

**MHE. MOHAMED H. J. MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika kipindi cha miaka 17 iliyopita ajira hizi za vikosi vilikuwa vinafanywa kwa ubaguzi kulingana na hali ya kisiasa ilivyokuwa. Hata hivi sasa inasemekana nafasi hizi kwa upande wa Zanzibar zinauzwa na Masheha. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa iundwe Tume kufuatilia ajira hizi na hata hao 300 wa hivi karibuni tuone kama hawatoki upande mmoja wa kisiasa au wa chama kimoja ili kujenga mustakabali na mshikamano wa Taifa kama ulivyosema mwanzo? (*Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema inasemekana miaka 17 iliyopita ajira za vikosi pamoja na ajira katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania zilikuwa zikitolewa kwa misingi ya kisiasa. Sasa kama inasemekana mimi siwezi kujibu tuhuma. Sasa kama alivyosema hii, hii ni dhana kama nilivyosema kwenye maelezo yangu ya utangulizi. Sisi katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania tunatoa fursa katika misingi ya haki kama nilivyosema. Kama utakumbuka vizuri kulikuwa na Maafisa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kuna wakati walituhumiwa walipokea rushwa katika uajiri, walifukuzwa kazi na bado tutaendelea kuchukua hatua hizo na

Mheshimiwa Mbunge utakubaliana nami kwamba Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni moja katika taasisi chache sana katika nchi yetu ambazo limejijengea heshima kubwa sana katika kufanya kazi kwa misingi ya uadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutahakikisha kwamba tutaendelea kuifanya kazi hiyo. Sasa kwa maana hiyo basi sioni kuna haja ya kuendelea kuunda Tume Maalum. Tutaendelea kulisimamia jambo hili kuhakikisha kwamba pande zote mbili za Muungano na mikoa yote itaendelea kupata fursa.

Sasa labda niseme tu kama Mheshimiwa Mbunge anadhani kama kuna dhana hii ya kibaguzi. Mimi nadhani hii dhana kwa sababu hata na mimi wakati mwingine pamoja na wananchi wengine tumekuwa tukifikiria tukijiuliza aah !! Kwa mfano tukiangalia kule Zanzibar kwa nini Wabunge wengi na wawakilishi wengi wanatoka Pemba. Sasa hii nadhani wakati mwingine ni dhana tu. (*Makofi)*

**MHE. SAID M. MTANDA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi bado ninajikita kwenye hiyo dhana. Nilitaka kufahamu kwamba nafasi hizi za vijana kwenda JKT zinatolewa kwa Mikoa na kama hivyo ndivyo nafasi hizi 115 ambazo zimedahiliwa vijana pale Mkoa wa Lindi kwanini vijana kati ya hawa 115 ni zaidi ya asilimia 70 wanatoka Mikoa mingine yaani Arusha, Kilimanjaro, Manyara na kutotoa fursa kwa vijana wenyewe wa Mkoa wa Lindi kuweza ku-*utilize* nafasi hizi? Je, nafasi hizi zinatolewa kwenye

Mikoa au ni kwa sifa tu haizingatii kwenye uwiano wa Kimikoa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya au njema sisi Wizara ya Ulinzi tunapotoa nafasi katika Mikoa kutafuta vijana ambao wanataka kujiunga katika Jeshi la Kujenga Taifa mara nyingi tunapokwenda kwenye Mikoa hatutafuti wazawa, maana kuna wakati Mwalimu Nyerer alisema tunapotafuta Kiongozi, nitatumia mfano wa kiongozi anasema hatuulizani makabila kwa sababu sisi hatuwezi kupunga. Sasa sisi tunatafuta vijana wa kujiunga na Jeshi tunapokwenda kwenye Mkoa tunauliza Raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini kama Waheshimiwa Wabunge wanadhani wakati tunapotoa nafasi kwa vijana wanaotakiwa kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Ulinzi pengine zinatumika vibaya pengine kunakuwa na dhana ya kwamba ni watu ambao wanaotoka katika Mikoa Fulani Fulani. Mimi nafikiri Waheshimiwa Wabunge mtupe taarifa mapema ili tuweze kuchukua hatua na tuhakikishe kwamba tunapata vijana kutoka Mikoa yote ili kujenga taswira ya kuwa na jeshi ambalo lina taswira ya umoja wa kitaifa. Nafikiri tukifanya hivyo itaonekana kwamba tunatekeleza majukumu yetu kwa misingi ya haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kama tutapata taarifa hizo mapema ninawahakikishia kwamba tutachukua hatua kama inavyostahiki. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimwulize swali dogo sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi. Toka nchi yetu ipate Uhuru sijawahi kusikia wala kusoma kwamba imetokea Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akatokea upande wa pili kwa maana ya Zanzibar. Je, chini ya uongozi wake kama Waziri tutarajie kwamba atapendekeza jina kwa Rais kwa Mzanzibar kuwa Mkuu wa Majeshi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini labda niseme tu hili ni suala la wakati. Hivi sasa tunao Mameja Jenerali wawili, Meja Jenerali Omar wa Kamandi ya Wanamaji, halafu tunao Meja Jenerali  Hassan Chema pale Makao Makuu, pia tunao Mabrigedia Jenerali wawili. Sasa nasema hili ni suala la wakati kuna wakati utafika. Lakini hata mimi Waheshimiwa Wabunge tangu historia ya Chama cha CHADEMA ilipoanza hakuna Mwenyekiti ambaye ametoka Mkoa wa Kigoma. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Safi. (*Vigelele*)

**MWENYEKITI**: *Order please.* Huyu ni Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, akimalizia kujibu swali la Kaimu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni. Naomba tuendelee na tumebakiwa na swali moja. Wakati mwingine humu ndani ya Bunge kuna raha zake. Swali lililobakia linaulizwa Wizara ya Uchukuzi na linaulizwa na Mheshimiwa Kheri  Khatib Ameir.

Na. 85

## Shirika la Ndege la Tanzania

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR** aliuliza:-

Shirika la Ndege la Tanzania ni muhimu kwa Uchumi na Ustawi wa Tanzania:-

(a) Je, Serikali ina msimamo gani kulifufua Shirika hilo?

(b) Je, ni lini Serikali inategemea kulifufua Shirika hili kama msimamo ni kulifufua?

(c) Je, tamko lililotolewa na Serikali la ubia kati ya Shirika la Uchina limefikia wapi?

**WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mbunge wa Matemwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti msimamo wa Serikali ni kuhakikisha kuwa kampuni ya Ndege ya Tanzania *(ATCL)* inaimarika na kujiendesha yenyewe ili kutoa huduma zenye tija na kuchangia katika uchumi wa nchi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya kulifufua Shirika la Ndege la Tanzania tayari zinaendelea, miongoni mwa hatua hizo ni kama ifuatavyo:-

(i)Kutenga fedha kwenye Bajeti ya Serikali ili kuchangia katika uendeshaji wa kampuni kwa mfano katika mwaka wa fedha 2011/2012 Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 16.7 ambazo ziliwezesha *ATCL* kugharamia matengenezo ya ndege aina ya *Dash 8Q300* yaliyofanyika nchini Afrika Kusini. Matengenezo hayo yaliwezesha *ATCL* kurejesha huduma zake kwa wananchi kuanzia mwezi Novemba, 2011. Aidha kutokana na Bajeti hiyo *ATCL* wanakamilisha matengenezo makubwa yanaitwa *C-check* ya ndege nyingine aina ya *Dash 8Q300* yanayofanyika hapa nchini.

(ii) Kati ya mwaka 2010 hadi sasa Serikali imeendelea kulipa mishahara ya wafanyakazi wa *ATCL* kama hatua za kuijengea uwezo kampuni hiyo ili kujenga upya mtaji wake wakati ikijiimarisha kibiashara.

(iii)Wizara imewasilisha Serikalini madeni ya *ATCL* yanayokadiriwa kufikia shilingi bilioni 106 kwa lengo la kuiondolea mizigo na kuiwezesha kampuni hiyo kufikia mahali pa kukopesheka na kuendesha shughuli zake kibiashara.

(iv) Kuimarisha uongozi wa *ATCL* kwa lengo la kurejesha nidhamu ya matumizi na uadilifu katika kulitumikia shirika.

(v) Serikali imeendelea kutafuta wawekezaji mahiri watakaoingia ubia na *ATCL* kwa lengo la kuimarisha shirika hilo.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007 Serikali ilifanya mazungumzo na kampuni binafsi kutoka Jamhuri ya watu wa China iitwayo *China Sonangol International Limited* kwa lengo la kuwekeza ndani ya *ATCL.*

Kimsingi kampuni ya China Sonangol ilikubali kushirikiana na Serikali kutekeleza mpango wa muda mrefu ambao ungewezesha *ATCL* kununua ndege za kisasa na kuongeza mtandao wake wa safari ndani na nje ya nchi. Hata hivyo mwaka 2010 kampuni hiyo ilibadili msimamo wake kuhusu kuwekeza ndani ya *ATCL* na mazungumzo ya kuwekeza ndani ya *ATCL* kusitishwa.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri maswali mawili. Kwanza, inasemekana hii kampuni ya China katika makubaliano yao ilikuwa walete ndege nane Tanzania lakini walileta ndege mbele na ndege mbili hizo hazikulipiwa. Ndege mbili zilikuwepo Tanzania lakini moja inasemekana kwamba imepata matatizo katika uwanja wa ndege wa Tabora. Nipo tayari kusahihishwa kwa hilo.

Lakini la pili, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kujitoa kwa kampuni hii ya China kwenye mkataba huo haoni kwamba ni zilezile mbinu zilizopelekea kuuwawa

kwa Shirika la Ndege na siku za nyuma hawakutaka ionekane Shirika hili linaendelea au linakuwa au linapata maendeleo katika nchi yetu?

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kwamba Mheshimiwa Mbunge aamini ninayomwambia mimi asisingatie anayoyasikia. Maana anasema inasemekana. Mimi ninachojua na ninachofahamu katika kumbukumbu za Wizara ni kwamba Kampuni hiyo ya China Sonangol ilichofanya ni kuingiza ndege mbile za *Dash 8Q300* kama nilivyosema, moja ilipata ajari sio Tabora lakini ni Kigoma na ya pili ndiyo tunaifanyia matengenezo makubwa *C-check* Jijini Dar es Salaam na itaruka baada ya muda si mrefu kutoka sasa kwa sababu pesa yote imeshapelekwa kwa matengenezo.

Lakini pili, dhamira ya kujitoa kwa Sonangol kwa kweli siwezi kufanya nadharia kwenye Bunge lako na nimewaelekeza watendaji wangu katika Wizara kwamba mmiriki wa Sonangol mara atakapokuja safari hii Tanzania ningependa nimsikilize kwa kina ni kitu gani kilimfanya pengine asitishe *interest* aliyokuwa nayo ndani ya *ATCL.*

**MWENYEKITI:** Wahehsimiwa Wabunge muda wetu umekwisha kwa hiyo tukiendelea zaidi ya hapa kwa mujibu wa Kanuni nilifidia muda tuliotumia kwa ajili ya Sala ya asubuhi kwa hiyo nafikiri tuendelee na ratiba yetu.

Ninaomba niwatambue wageni ambao tunao hapa ndani leo. Kwanza kabisa kuna mgeni mmoja wa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ambaye ni Ndugu Joel Deus Sasabo. Lakini vilevile tuna wageni wa Mheshimiwa Hawa Ghasia ambao ni watoto wake watatu. Wa kwanza anaitwa Inna Ali, wa pili anaitwa Asia Yahya na watatu anaitwa Emma Kawawa. Hawa ni watoto wa Mheshimiwa Hawa Ghasia. Sasa sijui wanaongoza na baba yao ama baba yao yeye hajahudhuria hapa. Lakini hawa ni wageni wa Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa N chi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuwatambue wageni wengine ambao wamefika Bungeni kwa ajili ya mafunzo. Wa kwanza ni kikundi cha kinamama 35 kutoka *Redeemed Assemblies of God,* naomba wasimame. Karibuni sana tunahitaji sala zenu na sasa sisi Wabunge wanawake lakini Wabunge wanaume pia muwaombee. Mtuombee tu wote kwa ujumla wetu. Tuna wanafunzi 59 kutoka chuo cha *CBE Dodoma* naomba wasimame kama wapo hapa ndani. Ahsante sana. Tuna wanafunzi 20 kutoka shule ya msingi Mikocheni. Karibuni sana.

Halafu tuna wageni wawili kutoka Bodi ya Hospitali ya Temeke. Karibuni sana. Tuna wanafunzi 19 kutoka Shule ya Sekondari ya Zanaki Dar es Salaam. Karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge matangazo ya kazi, nimeombwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge

Katiba, Sheria na Utawala Mheshimiwa Pindi Chana anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati hiyo kuwa leo tarehe 26 saa saba mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo. Kikao kitafanyika katika Ukumbi Namba 227.

Mheshimiwa Margaret Sitta, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii na yeye anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake leo tarehe 26 saa saba mchana watakuwa na kikao cha Kamati yao, hawa watakutana ukumbi namba 231 jengo la utawala.

Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Ofisi ya Waziri Mkuu Kabwe Zubeir Zitto anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa anarekebisha *addendum* kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani Ofisi ya Waziri Mkuu kifungu cha 2(1)(ii) kuondoa neno bilioni lililoandikwa kabla ya tarakimu na badala yake zibaki tarakimu tu. Anaomba kuwasilisha na ameleta hiyo *addendum* yake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya matangazo haya ya Wageni, naomba sasa Katibu atuongoze na shughuli inayofuata.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mwongo wa Spika.

**MWENYEKITI**: Mwongozo.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama katika Ibara ya 68 (7). "Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi wake."

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi anajibu swali kuhusiana na masuala ya jeshi taarifa tulizonazo ni kwamba katika *intake* iliyopita Zanzibar ilipewa nafasi 500 kati ya hizo nafasi 300 zilipelekwa JKT nafasi 200 zilichukuliwa na Ikulu Zanzibar, nafasi 100 ndizo ambazo ziligawiwa kwa mikoa mitano ya Zanzibar kila Mkoa nafasi 20. Taarifa hizi tulizipeleka hata kwa Waziri wa Ulinzi aliyepita.

Naomba mwongozo wako kauli aliyoitoa Mheshimiwa Mnyaa ya kutaka kuundwa Tume kuchunguza suala hili tunahisi bado lina mashiko. Naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge kama ni hoja ni kuundwa kwa Tume ziko taratibu za Kibunge na Kanuni ambazo zinasimamia uendeshaji wa shughuli zote. Mbunge hakatazwi. Kwa sababu kama unaona kuna haja ya kuundwa kwa Tume, chukua Kanuni na Kanuni hii inakuelekeza utaratibu wa kufanya jambo lolote ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama unaona bado hoja ya Tume ina mashiko, soma Kanuni, tafuta mahali panapotakiwa kuundwa kwa Tume, jenga hiyo hoja, njoo Bungeni na

Wabunge wakikubali watakuunga mkono na Tume itaundwa. Hoja ya kuundwa kwa Tume haiamuliwi kwa Mwongozo wa Kiti, inaamuliwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge.

Kwa hiyo, kama unaona bado unahitaji, fungua Kanuni yako jiandae, Wabunge watakuunga mkono kama ulivyosema hoja hiyo bado ina umuhimu, ndiyo utaratibu huo wala hakuna tatizo lingine lolote na kama hakuna umuhimu, Wabunge watafanya maamuzi yao.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu hatua inayofuata.

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Kushuka kwa Bei ya Sangara Katika Ziwa Victoria

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mujibu wa Kanuni ya Bunge Na. 49 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa Kauli ya Serikali kuhusiana na kushuka kwa bei ya samaki aina ya Sangara kwenye Ukanda wa Ziwa Victoria.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Kauli ya Serikali kuhusu mgogoro uliojitokeza kati ya wavuvi na wenye viwanda kutokana na wenye viwanda kushusha bei ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Victoria lina jumla ya kilomita za mraba 68,800 na liko chini ya umiliki wa nchi tatu, yaani Kenya asilimia 6, Tanzania asilimia 51 na Unganda asilimia 43. Uvuvi ni shughuli kuu katika Bonde la Victoria na inakadiriwa kuhusisha wavuvi wa kudumu wapatao 124,000. Aidha, uvuvi ni chanzo cha *protein* kwa binadamu, hutoa ajira na ni chanzo cha mapato kwa wadau mbalimbali na kulipatia Taifa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupandikizwa kwa samaki aina ya Sangara katika Ziwa Victoria mwishoni mwa miaka ya 1950 kulibadili hali ya uvuvi katika ziwa hilo kutokana na kuongezeka na samaki aina ya sangara na kupungua kwa samaki wa asili. Ongezeko hili la Sangara lilisababisha kuanziswa kwa viwanda vya kisasa vya kuchakata samaki katika Ukanda wa Ziwa Victoria mwaka 1992 na kufanikiwa kupata soko katika Nchi za Ulaya, Asia, Marekani na Australia. Hivi sasa kuna jumla ya viwanda 11 katika Kanda ya Ziwa Victoria, Mwanza viwanda saba, Musoma viwanda viwili na Bukoba viwanda viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, viwanda hivi na vile vilivyoko Nchi ya Kenya na Uganda vimekuwa vikitegemea zaidi Soko la Jumuiya ya Ulaya kwa kuwa inatoa bei nzuri ya minofu ya samaki aina ya Sangara. Soko la Jumuiya ya Ulaya lina masharti magumu na linahitaji mazao ya uvuvi yenye ubora na usalama wa hali juu. Hata hivyo, kutokana na viwanda vyetu kuzalisha mazao katika viwango vinavyokubalika kimataifa vimekuwa vikinufaika na uwepo wa soko hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya hivi karibuni, wingi wa Samaki aina ya Sangara kwenye Ziwa Victoria umeshuka kutoka tani milioni moja na laki mbili mwaka 1999 hadi kufikia tani 227,365 mwaka 2008. Hata hivyo, mwaka 2011 wingi wa samaki umeongezeka kidogo hadi kufikia tani 324,391. Sababu zilizochangia kushuka kwa wingi wa samaki katika Ziwa Victoria ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Kuongezeka kwa wavuvi, zana za uvuvi, vyombo na mbinu za uvuvi, kuongezeka kwa nguvu ya uvuvi, kulinganisha uwezo wa rasilimali iliyopo.

(ii) Kuongezeka kwa uvuvi haramu.

(iii) Mabadiliko ya Tabianchi.

(iv) Uchafuzi na uharibifu wa mazingira katika Ziwa Victoria

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imeendelea kufanya juhudi za kudhibiti uvuvi haramu na uchafuzi wa mazingira ili kuhakikisha kuwa kunakuwepo na uvuvi endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushuka kwa bei ya Samaki aina ya Sangara; Kulingana na taarifa kutoka mtandao wa *FAO Global Fish* wa mwezi wa pili mwaka 2012, *www.globalfish.org/nilepatchapril2012,* unaonesha kwamba, bei ya samaki aina ya Sangara katika masoko ya nchi za Ulaya ilianza kushuka kuanzia mwaka 2009/2010 ambapo kilo moja iliuzwa wastani

wa *Euro 7* na imeendelea kushuka hadi kufikia wastani wa *euro 4.5* mwaka 2011/12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya asilimia 95 ya Sangara anayevuliwa kutoka Ziwa Victoria kuchakatwa na kuuzwa nje ya nchi, katika kipindi cha wiki mbili zilizopita bei ya Sangara kutoka Ziwa Victoria zimeshuka kama ifuatavyo:-

Nchini Tanzania bei zilishuka kutoka shilingi 4500 kwa kilo hadi wastani wa shilingi 3000 kwa kilo pale kiwandani. Uganda bei ilishuka kutoka shilingi za Uganda 6000 hadi shilingi 4000 kwa kilo ambayo ni sawa na shilingi 2600 za Tanzania. Kenya bei ya Sanagara ilishuka kutoka Shilingi za Kenya 210 hadi wastani wa Shilingi za Kenya 120 kwa kilo ambazo ni sawa na shilingi 2300 za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii pia imechangia kushuka kwa bei ya kununulia samaki katika mialo ambapo Tanzania kwa kilo inauzwa wastani wa shilingi 2000 ikilinganishwa na bei za awali za shilingi 3500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichosababisha kushuka kwa bei ya Sangara ni kutokana na viwanda kukosa masoko katika Nchi za Ulaya kutokana na sababu zifuatazo:-

(i) Kutetereka kwa sarafu ya Euro.

(ii) Kutetereka kiuchumi na kibiashara kwa baadhi ya nchi zikiwemo Hispania, Ureno,

Italia na Ugiriki ambazo ndiyo soko kubwa la minofu ya Sangara kutoka Afrika Mashariki.

(iii) Ukosefu wa Ajira katika nchi hizo na hivyo uwezo mdogo wa kununua bidhaa zikiwemo vyakula, hivyo watu wanapendelea zaidi kula *Pork* (Nguruwe) na kuku kwa sababu bei zake ni rahisi zaidi kuliko bei ya Sangara. Kwa mfano, kilo moja ya kuku au nguruwe katika soko la Ulaya huuzwa kwa Euro tatu.

(iv) Wakati huo huu Ulaya ni kiangazi watu wanasafiri sana na hawapendelei kula mazao ambayo ni *fresh* ambayo yanahitaji gharama kubwa katika kuyahifadhi.

(v) Kumekuwepo na aina nyingine za samaki wenye bei ya chini hususan *Bursa* kutoka Mashariki ya mbali na Vietnam, Tilapia wanaofugwa kule China, *Cord* wanaotoka Ulaya na *Baramundi* wanaotoka ambao wanafanana na Sangara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu hizi ndizo zilizochangia kushuka kwa bei ya Sangara. Pia jana nimeongea na Balozi Dkt. Deodorus Kamala kule Brussels Ubelgiji ,akathibitisha kwamba sababu hizi ndizo hasa zimesababisha kushuka kwa bei ya Sangara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kama hii ya kudorora kwa uchumi iliwahi kutokea miaka ya 2008 hadi mwaka 2010 na kusababisha kuteremka kwa biashara ya

baadhi ya mazao kama vile pamba, kahawa, chai, ngozi na kadhalika katika Soko la Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya mazungumzo baina ya wenye viwanda, mawakala wa kuuza samaki na wavuvi wanaouza samaki Viwandani ili kuona namna ya kuboresha biashara na bei ya samaki. Mkutano wa kwanza kati ya Serikali na wenye viwanda pamoja na wavuvi ulifanyika na makubaliano yaliyofikiwa katika mkutano huo ni pamoja na haya yafuatayo:-

(i) Mawakala wa samaki na wavuvi wakutane na wenye viwanda husika ili kujadili bei mwafaka kwa wote yenye lengo la kufidia hasara iliyojitokeza kutokana na kushuka ghafla kwa bei ya samaki.

(ii) Umoja wa wenye viwanda vya kuchakata na kusindika samaki ambao unaitwa *TFPA* unatakiwa kuwasilisha Serikalini pendekezo la bei mwafaka kabla ya tarehe 5 Julai, 2012.

(iii) Bei zitakazotumika katika kipindi hiki cha mpito kuanzia tarehe 21 Juni hadi tarehe 5 Julai zitatokana na maelewano kati ya wenye viwanda na mawakala wa kuuza samaki viwandani. Kwa sasa kila kiwanda kimekubaliana na mawakala hao kutokana na mikataba waliojiwekea. Kwa mfano, bei za samaki kwa baadhi ya viwanda kwa sasa ni kama ifuatavyo: Kiwanda cha

*Tanzania Fish Processors (TFP)* kinanunua kwa shilingi 3000 kwa kilo hadi 3100. Kiwanda cha Omega kinanunua kwa 3000 hadi 3200 kwa kilo. Kiwanda cha *Vicky Fish* kinanunua kwa shilingi 3000 kwa kilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makubaliano yamefikiwa kati ya baadhi ya wenye viwanda na baadhi ya wavuvi kuendelea na shughuli zao za uzalishaji na uchakataji wa samaki kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa kuuza samaki viwandani: Hivi sasa kuna zaidi ya wavuvi laki moja ambao huwauzia maajenti au mawakala wapatao elfu moja ambao ndiyo wameingia mkataba na wenye viwanda vya kuchakata samaki. Wenye viwanda huwakopesha mawakala fedha za kununulia samaki, zana za uvuvi kama vile nyavu, boti na kadhalika, kwa masharti kwamba wakikusanya samaki wanawauzia wale wenye viwanda waliowapatia mikopo. Kwa mfano, Kiwanda cha *Tanzania Fish Processors* kimeshakopesha zaidi ya shilingi bilioni 3.5 kwa mawakala 70. *Omega Fish* kimeshakopesha zaidi ya shilingi bilioni mbili kwa mawakala 30, *Vicky Fish* kimeshakopesha zaidi ya bilioni 1.6 kwa mawakala 53, *Musoma Fish* kimeshakopesha zaidi ya milioni 574 kwa mawakala wa kuuza samaki 44.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ni ukweli usiopingika kwamba, Mawakala na wenye Viwanda ndiyo wanapata faida kubwa kuliko wavuvi wenyewe. Serikali inaendelea kutoa rai kwamba, wavuvi wawe na umoja wao wenye nguvu na vyama vyao vyenye

nguvu waweze kuuza samaki moja kwa moja viwandani badala ya kupitia kwa mawakala. Pia umoja huu utawasaidia kujadiliana bei yenye maslahi kwa wenye viwanda na Serikali tutakuwa pamoja na wavuvi kuwasaidia waanzishe umoja wenye nguvu ili wasinyonywe na mawakala na vile vile wasinyonywe na wenye viwanda, kwa sababu wanapokuwa hawana chama cha kuwatetea basi wanagawanywa na ni rahisi zaidi kupunjwa hata kwenye bei za minofu ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu tatizo hili litokee Serikali imeendelea kufanya yafuatayo:-

(i) Serikali imeagiza Balozi zetu zilizoko nchi zenye masoko ya Sangara kufuatilia mwenendo wa bei kila wakati ili bei ya kuuzia katika Soko la Dunia zifahamike kwa wavuvi na mawakala wote na wenye Viwanda ili waweze kushauriwa ipasavyo.

(ii) Kuendelea kufuatilia utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa kwenye mkutano wa wenye viwanda na wauzaji wa samaki kwa kuendelea kuwaelimisha wenye viwanda na wavuvi kuhusu kushuka kwa kwa bei ya samaki.

(iii) Pia Serikali inaendelea kuhamasisha ulaji wa Sangara humu nchini na nchi jirani ili Watanzania wale wanachozalisha na hivyo kutoa soko kwa mazao yetu ya ndani.

(iv) Serikali kwa kusaidiana na wenye viwanda vya kuchakata minofu wataendelea kutafuta masoko mengine badala ya kutegemea Nchi za Ulaya peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuchukua fursa hii kuwaomba wavuvi na mawakala wa samaki waendelee kuuza samaki wao viwandani kwa bei waliyokubaliana kwenye mikataba hadi hapo bei dira itakapotoka tarehe 5 Julai, 2012. Vile vile napenda kukujulisha kwamba, jana Chama cha Wavuvi *(TAF)* kutoka eneo la Kanda ya Victoria nilikutana nao na tukakubaliana nao kwamba wanaendelea kuvua samaki na kuuza kwa amani bila wasiwasi mpaka bei dira itakapotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe nitakwenda Mwanza wiki hii ili kuhakikisha kuwa bei dira yenye kutoa haki kwa wote, yaani wauzaji wa samaki na wenye viwanda inazingatiwa na inatoka kabla au tarehe 5 Julai, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa ya kutoa Kauli ya Serikali. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kauli yako hiyo. Katibu tunaendelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013 – Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, naomba nimwite Mheshimiwa Maryam Msabaha, atafuatiwa na Mheshimiwa Keissy.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana. Kwanza, nakushukuru wewe mwenyewe kwa juhudi na ushirikiano wako katika Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii na kwa upendo mliouonesha nilipopata msiba Zanzibar; Mwenyezi Mungu awabariki sana na tutazidi kupeana ushirikiano na Mungu atakufanyia wepesi katika Kiti chako cha Uenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niipongeze Hotuba ya Waziri Mkuu na Hotuba ya Waziri Kivuli ambaye ni Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, yale mazuri myachukue na yale ambayo mnayaona ni faida kwa Serikali msiyaache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi katika suala la Utawala Bora; Watanzania wengi wanasema Utawala Bora, Viongozi wanasema Utawala Bora, Utawala Bora ni nini; ni siasa safi, uongozi bora. Leo hii ukiangalia hakuna siasa safi, hakuna uongozi bora. Ukiangalia

Vyama vya Siasa wakiitisha mikutano wanatukanana badala ya kujadili sera au kujadili matatizo yaliyopo kwa wananchi, wanakaa wakitukanana na kuandikana kwenye mitandao; hii ndiyo siasa bora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tukiwa na uchaguzi kwenye majimbo badala ya watu kujadili kero za wananchi wanajadili matusi kuliko kuangalia kero ambazo zipo kwa wananchi. Ukiangalia Viongozi wengi kwenye Utawala Bora kila Kiongozi anataka akae madarakani kwa kujilimbikizia mali. Kwa kweli hili Serikali waliangalie. Zamani wakati wa Utawala wa Mwalimu Nyerere, wahujumu uchumi walikuwa wanakamatwa lakini sasa hivi sijui sheria hii imekwenda wapi! Ukiangalia tukianza kuchunguzana hapa kuna Viongozi wamepata mali nyingi hujui zimepatikana kwa njia gani. Naishauri Serikali ianze kufanya *reseach* kwa Viongozi, kama kuna Viongozi wanajilimbikizia mali kwa njia ya udanganyifu, kwa njia ya kuiibia Serikali, wachukuliwe hatua na wapokonywe mali zao zirudi kwa umma.

Kuhusu suala la Muungano, katika Hotuba yake Waziri Mkuu, ukurasa wa 12, amezungumzia suala la Muungano na kero ambazo zimetatuliwa, lakini kuna kero ambayo ni kubwa sana kwa Wazanzibari, kero ya usafiri. Tumekuwa tukitumia maboti ya watu binafsi kusafiri na siku yakikwama sisi tutakwenda wapi? Ukiangalia Kisiwa cha Pemba hakina usafiri wa uhakika. Siku zote umeshuhudia mwenyewe usafiri wa Pemba hata wakati wa *MV Spice* tumepata ajali kubwa sana na Wazanzibari wengi kupoteza uhai. Nilikuwa nataka nimhoji Waziri Mkuu; nakumbuka kulikuwa na meli za

Serikali; je, meli hizi zimeenda wapi kama MV Muungano, MV Afrika, MV Jamhuri, MV Mapinduzi na MV Maendeleo? Kama meli hizi ziliuzwa basi ni kwa nini zisinunuliwe za uhakika Wananchi wa Pemba wakapata usafiri wa uhakika na sisi Wazanzibari tukaingiza Pato la Taifa kwa meli hizi za Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la pesa za *radar*, naona Wazanzibari tumesahaulika. Sisi Wazanzibari pia tunahusika katika suala la *radar*, mtufikirie.

Elimu ya Vyuo Vikuu ni suala la Muungano; kwa nini na sisi msitupe pesa hizo tuwanunulie watoto wetu madawati, vitabu, tununue madaftari na vitu vingine ambavyo ni vya elimu? Katika suala hili la *radar* mmenyamaza kimya hamkusema na Zanzibar tunagawiwa shilingi ngapi. Naomba Waziri Mkuu utakapokuja kutoa majumuisho, useme na unipe majibu ya uhakika ndiyo niunge mkono Bajeti yako na kama hujanipa majibu ya uhakika sitaiunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini sasa hivi ukiangalia Watanzania wengi wanamkumbuka Mwalimu Julius Kambarage na sisi Wazanzibari tunamkumbuka Mzee wetu Karume? Mwalimu aliwajali sana wanyonge, Mzee Karume aliwajengea hata Wananchi wa Zanzibar, leo hii kuna maghorofa ya Michenzani na sidhani kama kuna mtu ambaye ameyaendeleza maghorofa haya mpaka leo. Tukiangalia viwanda vingi Tanzania Bara havipo; viwanda hivi vimekwenda wapi; ni nani alivichukua viwanda hivi au amevifilisi viwanda hivi? Kama kuna

watu ambao wamefilisi viwanda hivi ni kwa nini wasichukuliwe hatua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanawake tumekuwa tukiuliza maswali mengi sana katika Bunge hili kuhusu Mfuko wa Jimbo, lakini Waziri Mkuu inavyoonekana sisi Wanawake haujatufafanulia mnatuingiza vipi kuhusu masuala Mfuko wa Jimbo. Msitubague kiasi hicho, mwanamke ndiye mtendaji wa kazi, hata Naibu Mawaziri wengi na Mawaziri Kamili Wanawake najua ni waadilifu katika Serikali hii, ninasema na ninyi Mawaziri Kivuli mfanye kazi msiseme Uwaziri Kivuli mmepewa wa kujikweza ni wa kufanya kazi na mfanye kazi Watanzania wote wajue mnafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanawake wote mliopata Uwaziri mliorudi katika viti hivyo, msiseme ninyi ni bora kuliko Wanawake wengine ambao wamekaa kwenye viti vingine na sisi pia tunaweza huo Uwaziri wa Maendeleo ya Jamii na Watoto. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukirudi suala la watoto wa mitaani na wazee, itafika mahali hatutapata wageni katika Jiji la Dar es Salaam, Ubungo kumegeuka ndiyo nyumba ya kulala wageni; watu wanalala pale ukija ukitazama watoto, akina mama wanalala kwenye mitaro, wazee wanalala kwenye mitaro; kwa nini watu ambao wanahujumu uchumi ambao wamejenga majumba haya wasifirisiwe wakapewa yatima wakakaa na wale wazee wanaolala kwenye mitaro? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie hawa watu ambao wanakwepa hata kulipa kodi za Serikali, leo ukiangalia Kariakoo siyo wote wanalipa kodi. Tukiangalia pale kuna pesa chafu, maghorofa yale yote yametoka wapi? Maskini wote wamehamishwa Kariakoo wanapelekwa huko na huko kwingine mnakowapeleka pia mrudi kwenda kuwaibia mashamba yao. Tuangalie hawa wanaohujumu uchumi wapelekwe jera wakafungwe na wafilisiwe mali zao. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema kwa uchungu mkubwa sana, ukiangalia wimbi kubwa la vijana wanakimbilia mjini hawataki kulima vijijini. Mimi nakujua kwa baba yako na mzee wako nimewahi kumwona. Wewe ni mtoto wa mkulima; kwa nini hutaki kuangalia hili suala la kilimo mkalipa kipaumbele? *(Makofi/Kicheko)*

Kila siku mnasema KILIMO KWANZA; ni Wimbo wa Taifa? Huu siyo Wimbo wa Taifa, wewe ni mtoto wa mkulima sasa itashangaza wewe mtoto wa mkulima unakuja kuingizwa kwenye mambo ya ufisadi! Mimi mwenyewe kila siku nakuombea kwa Mwenyezi Mungu, akuepushe kwa sababu utamdhalilisha yule mzee pale Kijijini, utawadhalilisha na wapiga kura wako. Wewe umetoka katika familia ya kimaskini, familia ya wakulima, sasa hawa vijana mhakikishe hiki KILIMO KWANZA mnawawezesha wanabaki vijijini wanalima. *(Makofi)*

Kila siku ukienda Dar es Salaam vyakula vinapanda hujui vyakula hivi vinatoka wapi, kila siku

ukiangalia sasa vijana wengi wamekuwa wezi, vijana wengi wamekuwa vibaka, vijana wengi wamekuwa wavuta bangi, vijana wengi hata hawaeleweki. Kwa kweli angalieni namna ya kuwawezesha vijana wabaki vijijini walime ndiyo tujue KILIMO KWANZA. KILIMO KWANZA siyo cha kutajirisha mafisadi. Kuna watu wananufaika kwa fedha za KILIMO KWANZA. Mimi siungi mkono hoja mpaka Mheshimiwa Waziri Mkuu unijibu maswali yangu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Huyo ni Mariam Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Unguja Zanzibar. Ahsante sana kwa mchango wako.

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kabla ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa nafasi. Mimi ilikuwa nichangie jioni lakini nashukuru sana nimepewa nafasi asubuhi hii.

Kwanza kabisa, kabla sijasahau, tuliahidiwa fedha za rada hapa. Kwanza, tuwajue waliofanya mikataba kwa ajili ya hizi fedha za rada wameingiza hasara, fedha zetu zimekaa Uingereza miaka na miaka tunataka riba yake. Tujue mapema kwamba, hizi fedha hata riba yake Namanyere leo unashangaa fedha za rada zinakwenda kununua madaftari. Hivyo, vitabu vyenu vitakwenda kukaa wapi? Watoto wanakaa chini? Siku mbili vitabu vimeharibika, huu ni ufisadi mwingine. Tumekubaliana fedha za rada zinunue madawati na nyumba za walimu. Ndugu zangu tuungane vyama vyote hatukubali fedha za rada kununua vitabu, huu ni ufisadi dhahiri, kama

mmeshapewa fedha tujue bilioni 50 vitabu gani, zipo fedha za M-Canada bilioni 30 ndiyo mnunulie vitabu. Hizi fedha ziende kila Halmashauri na Madiwani wasimamie kwa ajili ya madawati. Tumechoka kuibiwa. Mna masikio hamsikii, mna pua hamnusi; huu ndiyo mwisho. (*Makofi*)

Vile vile nasikia Wabunge wengi wanalalamika tufufue Shirika la Reli, tufufue Shirika la Ndege, kwanza tuwajue waliofilisi Mashirika haya ni akina nani? Wamo humu humu au wapo nje, wakamatwe. Hatuwezi kufufua Shirika la Reli likafilisika tena, Shirika la Ndege likafilisika tena. Kwanza, tuwatafute waliofilisi Mashirika haya. Shirika la Ndege, Shirika la Reli*, National Insurance,* mabenki kuunguzwa, viwanda kufilisiwa, kila kitu, tuwakamate tuwafunge hawa jamaa. *(Makofi*)

Nilizungumza mwezi wa nne adhabu kali, hawa jamaa ndugu zangu ni kuwanyonga. Maana mtu anaiba dawa, kule kijijini kwangu watu wanakufa si amewaua? Ameiba dawa, fedha za dawa anakula, wananchi wanakufa kwa kipindupindu, kwa *typhoid*, kwa surua; si muuaji huyu? Huyu hastahili kuonewa huruma na yeye auwawe moja kwa moja. *(Makofi/Kicheko)*

Nchi hii nimewaambia tabu yake sheria zetu ni mbaya zinalinda wezi. Wanasema ahaa sheria, ndugu zangu wanapoiba sheria inawalinda, mwizi akiiba anatetewa. Kariakoo mtu akamwibia mama simu anapigwa mawe anauwawa, wewe unaiba mabilioni uachwe! Leo nimesikia kwenye redio, hii mikataba ya gesi tayari bilioni 300 zipo. Kama mnakanusha

kanusheni magazeti, wametangaza Wanasiasa na baadhi ya Viongozi tayari wameshafungua akaunti kule Ulaya bilioni 300, lazima tuwe macho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bandari, ndugu zangu hii bandari watatukimbia watu wengi, kila ukipita meli 17, meli 18 zipo nje hamna upakuaji eti siku tisa. Pakueni kwa siku mbili mzigo umfikie mwenyewe. Hii bandari ndugu zangu ni neema; Rwanda, Burundi, Uganda, DRC – Congo na Zambia, wanategemea bandari yetu, lakini tunapiga teke. Mzigo unakaa bandarini ukinunua pea za viatu mpaka soli inakwisha ndiyo upate mzigo wake. Sasa hii bandari faida yake nini? (*Makofi*)

Tuna bandari tatu; Tanga, Dar es Salaam na Mtwara; zina kazi gani? Kenya wana bandari moja tu wanatushinda, wana reli ile tangu Mkoloni haijachakaa lakini sisi tuna abiria nenda rudi tunapakia abiria Kigoma, Mwanza, mabehewa yanapakia mbao lakini wajanja wanakula fedha. Wakamatwe wote waliofilisi Mashirika hata waliokuwa wanafanya miaka 20 nyuma pia watafutwe, kama wamekufa pingu zipelekwe kwenye makaburi yao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi mabaya ya Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro *(Kilimanjaro International Airport);* wanapata bilioni kumi wanatumia bilioni kumi! Bodi inaundwa pale wanajilipa mishahara wanavyotaka, wananunua vitu wanavyotaka, imekuwa kama mali yao, duka lao *Kilimanjaro International Airport. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikataba ya Barabara; tunasifu barabara zinajengwa siyo kweli. Barabara inajengwa kwa bilioni 40 mnapatana mpaka mwisho wa barabara bilioni 80. Juzi nilikuwa Ngara kule, barabara moja wametengeneza kwa bilioni 40 baada ya mwaka mmoja bilioni 191. Ndugu zangu tunakwenda wapi? Tunazidi kukopa kwa Wazungu mwisho watatukimbia. Lazima tuchunguze mikataba. *(Makofi*)

Juzi Waziri alitusomea habari ya meli kupakia abiria kutoka Bagamoyo mpaka Dar es Salaam; hiyo meli itasimama wapi? Watu gani wanakaa kule baharini? Hizi *gate* zitajengwaje; kuna watu gani wamesongamana kando kando ya bahari? Ndugu zangu tusishangilie kitu, mimi nataka Waziri anioneshe hiyo michoro atakayochora hiyo feli ya kupita kutoka Bagamoyo kwenda Dar es Salaam na hao abiria watatoka wapi? Watu wanakaa baharini kule wana magari yao matajiri, leo unaniambia mtu atapanda meli bahari ikichafuka atakwenda wapi? Ubadhirifu mwingine wa hela za Serikali. *(Makofi/Kicheko)*

Naomba nizungumzie kuhusu Mifuko ya Majimbo; Mifuko ya Majimbo ndugu zangu ni hatari. Mtu ana Jimbo ukubwa kama chungwa anapewa hela sawa na mtu mwenye Jimbo kama tikiti. Jimbo ukipiga tarumbeta wananchi wote wameshasikia, mnapewa hela sawa. Hela za mafuta hali kadhalika, mtu ana kilomita sita sawa na mtu ana kilomita 800, sisi wengine tuna usafiri wa maboti, usafiri wa miguu, tunapewa hela sawa. Bora zifutwe kuliko kudhalilishana namna hii au wakae watu wa-*assess* hayo Majimbo; Majimbo

kama limau, mengine kama mbegu ya chungwa, mengine kama tikiti, yachunguzwe na miundombinu yake ichunguzwe. Hatuwezi kwenda sawa, kama vigezo vya umaskini watu wote ni maskini nchi hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine, Mikoa yote ni sawa tutengewe bajeti sawa, barabara za lami, miundombinu ya maji, miundombinu ya hospitali kila kitu, ndiyo maana mpaka sasa Mikoa mingine inatangaza kujitenga kwa kuwa ina upendeleo wa hali ya juu. Sisi Mikoa yetu hakuna upendeleo wowote iko nyuma. Sasa bajeti hii hatuipitishi mpaka iwe sawa kwa sawa. Haiwezekani Mikoa mingine kama wapo peponi, Mikoa mingine kama wapo motoni. Hakuna kitu kama hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatolea mfano mdogo wa kuchekesha; miaka ya nyuma kule kwetu Wapembe, nilikuwa mdogo, kulikuwa na wachawi wengi sana ikabidi kila wiki Makamchape wanapiga ngoma wachawi wanakuja. Kama *PCCB* imeshindwa, Polisi imeshindwa, tutafute waganga wa kienyeji wapige ngoma mafisadi wote wataleta fedha zote walizoiba. Maana mtu wa *PCCB* anasimama jamani nisaidieni wala rushwa, wewe huwaoni wala rushwa, wenye maghorofa huwaoni, wenye kutorosha hela huwaoni, tukikupelekea wewe mwenyewe unawapigia simu kaja fulani kaniletea jina lako unakula rushwa. Tutafika wapi? Wala rushwa hawajulikani hapa? Leo unapata kazi, mimi leo Mbunge kesho na keshokutwa nimejenga ghorofa nimetoa wapi fedha si rushwa hizo? Si kunikamata tu?

Nipe barua nieleze; wewe Keissy jana ulikuwa Mbunge hii hela umeitoa wapi, kodi unalipia hili jengo lako ulilojenga? Hawa wanaojenga vile vile shule hizi za sekondari kama uyoga na baadhi ya Wabunge wana sekondari, mmezungumza kuwa wanachaji ada ya ajabu na kodi hawalipi. Wanaumiza wananchi, kodi kubwa kubwa na elimu wanayotoa sawa na shule za kata mpaka *division four* wanatoa, lakini ada milioni mbili, milioni tatu, wanalipa kodi. Kuanzia sasa walipe *VAT* na kodi hamna kuwaachia hata kama Wabunge wapo, Mawaziri mna shule, mlipe msifanye miradi maduka yenu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji Namanyere, nazungumzia tatizo la nenda rudi; mwaka jana niliwaambia nitaleta akina mama waje kulia hapa, mkasema tutaleta maji. Mwaka huu ndugu zangu sikubali Bajeti ya Waziri Mkuu au Bajeti ya Waziri wa Maji bila maji Namanyere, kipaumbele mnatuambia Bwawa la Kawa, kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu, siyo Bwawa la Wananchi wa Nkasi, tumeshazungumza mara nyingi hapa bwawa la kwenye shamba la mtu kwenye ranchi siyo faida ya watu wa Nkasi, halitusaidii lolote watu wa Nkasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Barabara za Mradi wa Ziwa Tanganyika mpaka wakamtafuta na mkandarasi wakampa na vitabu, Barabara ya Karungu, Kipili, Korongwe kupitia Mpenge, Kanchui, Kabwe, Mradi wa shilingi milioni 450 mpaka leo hakuna kitu mwaka mzima kwenye vitabu. Tangu mwaka jana imezungumzwa hapa Bungeni Barabara ya Mwaro -

Kirando na mwaka huu imezungumzwa kuna Mwaro hata dalili hakuna, tunadanganya hapa Bungeni; hakuna dalili wala hakuna fedha iliyokwenda kupima, hakuna hicho kitu na kwenye kitabu umeandika tena kuna Mwaro, Kirando, bora mfute mnawadanganya Wananchi wa Kirando. Kuna matanki ya maji Kirando tangu tuko Mkoa wa Mbeya yamejengwa matanki ya mabilioni ya hela lakini mtandao wa maji hakuna. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Umeme Namanyere, wakandarasi wamekimbia sijui wamesimama hakuna kinachoendelea. Mpaka Naibu Waziri alikwenda Namanyere akaahidi kwamba, mwezi wa sita umeme utawaka hakuna cha kuwaka ni koroboi ndiyo zinawaka mpaka sasa. Mimi nashangaa, kwa hiyo, nakuomba mwaka huu umeme wa Namanyere ukamilike na Mradi wa Maji Namanyere ukamilike. (*Makofi*)

*PCCB* wanafanya kazi nchi hii, nimeshaongea tangu mara ya kwanza, *PCCB* na wao wachunguzwe *system* wanayotumia siyo nzuri, tunawapelekea matatizo wanakaa nayo mezani na wana-*deal* na watu ambao ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, kengele ya pili.

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED:** Kengele ya kwanza au ya pili?

**MWENYEKITI:** Ya pili.

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED:** Basi, nawaambia maji Namanyere muhimu. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hili ndiyo Bunge la tarehe 26. Baada ya Mheshimiwa Maryam Msabaha amefuata Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ZITTO Z. KABWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia Hotuba hii ya Waziri Mkuu. Jana Mheshimiwa Waziri amekuja kuomba Bunge limwidhinishie jumla ya shilingi trilioni 3.8 kwa ajili ya Ofisi yake na Taasisi zote zilizo chini ya Ofisi yake na takriban shilingi bilioni 113 kwa ajili ya Bunge. Fedha zote hizi takriban shillingi trilioni 3.2 zinakwenda Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla hatujamwidhinishia Mheshimiwa Waziri Mkuu fedha hizi na yeye kama Mkuu wa Shughuli za Serikali, msimamizi wa kazi za Serikali za kila siku na ambaye anaangalia utendaji wa takriban Mawaziri wote ni vizuri aweze kutoa majibu kwa baadhi ya masuala ambayo mengine ameyaainisha kwenye Hotuba yake na mengine ambayo hakuyaainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na Kigoma. Mheshimiwa Waziri Mkuu, amezungumzia katika ukurasa wa 51 wa Hotuba yake juu ya masuala ya ulinzi na usalama, lakini hakugusia kabisa operesheni ambazo zinaendelea hivi sasa katika Mkoa wa Kigoma,

nadhani na Mkoa wa Kagera kuhusiana na masuala ya wahamiaji haramu. Hivi tunavyozungumza ni kwamba, mamia ya watu wa Kigoma wameoneshwa kwamba siyo Raia wa Tanzania. Utaratibu huu umekuwa ukiendelea mwaka hadi mwaka. Napenda Mheshimiwa Waziri Mkuu, akumbuke historia baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia kati ya mwaka 1918 na mwaka 1924, Kigoma haikuwa sehemu ya Tanganyika. Kigoma ilikuwa inatawala kama inavyotawaliwa, tofauti na sasa hivi Burundi inatawaliwa tofauti na Rwanda. Kwa muda mrefu sana Mkoa wa Kigoma umeachwa nyuma katika kila kitu kimaendeleo. (*Makofi*)

Mimi nimeona lami ya kwanza ya *highway* mwaka 2008, miaka zaidi ya 40 baada ya Uhuru. Leo hii watu wa Kigoma, wa maeneo ya Kusini mwa Kigoma, wa maeneo ya Kaskazini mwa Kigoma, wanasombwa kwenye maboti na magari wakiambiwa kwamba siyo Raia wa Tanzania. Hatuwaoni Wamakonde wakiambiwa kwamba siyo Raia wa Tanzania na wanapakana na Msumbiji! Hatuwaoni Wamasai wanaambiwa siyo Raia wa Tanzania na wanapakana na Kenya! Hatuwaoni Wachaga wanaambiwa siyo Raia wa Tanzania na wanapakana na Kenya! Hatuwaoni Wanyakyusa wanaambiwa siyo Raia wa Tanzania na wanapakana na Zambia na Malawi! Kwa nini suala hili liwe ni kwa watu wa Kigoma na watu wa Katavi peke yake? Kwa nini tunatumia fedha za nchi na polisi wa nchi kwenda kusumbua watu wa Kigoma?

Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa, operesheni inayoendelea sasa hivi katika Mkoa wa

Kigoma kuwanyanyasa Raia wa Kigoma waonekane ni Raia wa Tanzania wa Daraja B ikome mara moja na Viongozi wa Kisiasa, Wabunge wote wa Mkoa wa Kigoma na Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa, tukae tuweze kuangalia kwa sababu kuna uonevu wa hali ya juu sana katika operesheni ambayo inaendelea hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba niyaseme hayo vizuri na ninarejea kwamba, tumefundishwa na wazee wetu kwamba sisi kati ya mwaka 1918 na mwaka 1924, hatukuwa sehemu ya Tanganyika iliyokuwa inatawaliwa na Mwingereza. Ninaomba nirejee; sisi ni watu wa Kigoma, kwanza, kabla hatujawa Watanganyika, kabla hatujawa Watanzania, ninaomba nilisisitize hili na watu wa Kigoma wananisikia kwa sababu tumenyanyaswa sana; ninaomba masuala ya uraia yaangaliwe kwa karibu sana. Huu ni ujumbe ambao nimepewa na watu wa Kigoma, nimeombwa niueleze na naomba Ofisi ya Waziri Mkuu, Mkuu wa Kigoma yupo hapa, Wakuu wa Wilaya, Kamanda Mkuu wa Mkoa wa Polisi wa Mkoa wa Kigoma na *IGP,* waweze kuliangalia jambo hili kuweza kuhakikisha kwamba tunawalinda raia wa Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kumekuwa na taarifa ambazo zimeandikwa katika vyombo vya habari toka wiki iliyopita; lilianza Gazeti la *The East African,* baadaye wakaja Gazeti la *The Citizen* na leo nimesikia Gazeti la Mwananchi limezungumza kwamba kuna Watanzania sita wana fedha katika akaunti kule Uswisi, zaidi ya shilingi bilioni 303. India walipopata

taarifa hizi kutoka Benki ya Uswisi waliwataja majina watu wote wanasiasa na wafanyabiashara wenye fedha nje na fedha zile zikachunguzwa, zile ambazo zimepatikana kwa haramu zikarejeshwa India.

Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aiagize TAKUKURU na Vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama, kwanza, tutambue ni Watanzania gani hawa na fedha hizi zimepatikana kwa njia zipi na zile ambazo zimepatikana kwa njia ya wizi na ufisadi zirejeshwe nchini mara moja. Kwa sababu hatujaanza kunyonya utajiri huu wa gesi tayari kuna watu ambao wameshaanza kutajirika nao. Tutakapoanza kunyonya hali itakuwaje? Kwa hiyo, nilikuwa naomba suala hili Serikali ilichukulie kwa uzito mkubwa ili itume salamu kwa mtu yeyote ambaye anatarajia kwamba atafaidika na utajiri wa rasilimali ya nchi kama gesi na madini na kadhalika ajue kwamba kokote atakapoficha fedha zake tutazifuata na zitarudi katika nchi hii. Namwomba Waziri Mkuu, aliangalie jambo hili kwa ukaribu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, hivi sasa Kiongozi wa Upinzani amezungumza jana kuna meli zipo Pwani ya Mkoa wa Pwani, Lindi na Mtwara, zinatafuta mafuta. Hakuna kampuni hata moja ya mafuta inayonunua hata mchicha kutoka Tanzania. Meli zote ambazo zipo Bandari ya Mtwara zinakwenda kupeleka huduma kwenye maeneo ambayo yanatafuta mafuta, yanapata mchele, nyanya, vitunguu, mchicha, mafuta ya kula na kadhalika kutokea Kenya kwa sababu hatujaweka utaratibu wa kufanya nchi yetu iweze

kufaidika na utajiri huu mwanzoni, kwa kuwa katika hatua hizi za mwanzoni hakuna kodi ambayo tunapata kwa sababu mafuta bado yanatafutwa.

Hatua hizi za mwanzoni tunatakiwa tufaidike na fedha inayokuja, watu waweze kutumia fedha za kutoka ndani. Hali ilivyo hivi sasa ni kwamba, makampuni ya mafuta yanatumia zaidi ya dola milioni 161 kwa ajili ya shughuli za ulinzi na makampuni yanayolinda ni ya nje. Yanabeba silaha kubwa kubwa, siku yakiamua kutugeuka na *Navy* yetu ilivyo tutapata shida. Naomba tutenge *resources* za kutosha na hata kama hatujaziweka kwenye bajeti sasa hivi, tuangalie tuimarishe *Navy* na tupige marufuku. Tuandike sheria kabisa kwamba, itakuwa ni marufuku kwa raia yeyote wa kigeni kubeba silaha zozote kubwa ili kuweza kuhakikisha kwamba ulinzi ama unafanywa na watu wa ndani au unafanywa na Navy yetu, tuweze kulinda mipaka yetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuna suala ambalo halijaisha na Kiongozi wa Upinzani Bungeni jana amelizungumzia, la mafuta na gesi katika Masuala ya Muungano. Naomba jambo hili tulimalize kwa haraka na mimi sioni ubaya hata kidogo kama tukiamua kwamba shughuli zote siyo masuala ya *regulation,* vibali na masuala ya kutoa leseni, masuala yote *commercial* yanayohusiana na mafuta na gesi, kila upande wa Muungano ushughulike na masuala yake. Hakuna sababu ya kunga’gania jambo hili, kama sisi tuna dhahabu, *Tanzanite* na madini, hayapo sehemu ya Muungano; kwa nini mafuta na gesi yawe sehemu ya Muungano?

Hili ni jambo ambalo tunatakiwa tulimalize iishe hii kero, vikao na vikao havitasaidia, tuimalize hii kero, tu-*move forward*; watu wa Zanzibar waanze utaratibu wao wa kufanya utafutaji wao, waangalie kama watayapata hayo mafuta au hawatayapata, sisi tayari huku Bara tumeshapata, tuna matrilioni ya gesi, basi na wao tuwaache waendelee na utaratibu wao, hakuna sababu ya kuchelewesha jambo hili tuweze kulimaliza mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la Kiwira na baadaye nitakuwa na mazungumzo na baadhi ya Mawaziri kuhusiana na suala hili, tuliangalie kwa makini. Tumetenga shilingi bilioni 40 kwenye fedha ya maendeleo Wizara ya Nishati na Madini kwa ajili ya nini? Kuna fedha ambayo tunaenda kuwalipa watu ambao wameuharibu mgodi. Kwa nini tuwalipe watu ambao wameuharibu mgodi? (*Makofi*)

Tunaenda kulipa bilioni 40 siyo kwa Kiwira nzima ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**MHE. ZITTO Z. KABWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia bajeti aliyoisoma hapo jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea kuhusu suala la afya na nianze na suala la huduma bure kwa wazee, watoto na akina mama wajawazito. Wiki iliyopita, niliuliza swali hapa kuhusu wazee kupatiwa huduma bure. Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kwamba, anaandaa utaratibu wa wazee kupewa vitambulisho. Sina hakika kama litakuwa ndiyo suluhisho zuri la wazee wetu hawa kupata huduma hizo bure. Kinachonishangaza, suala hili linaonekana kwamba ni la kisiasa zaidi. Akina mama wajawazito nao tuliwaahidi kwamba watapewa huduma hizo bure, sasa sijui wao watepewa vitambulisho gani wakati hali ya maumbile yenyewe inaonesha kabisa kwamba mama huyu ni mjamzito na anatakiwa kupewa huduma hiyo bure na mpaka sasa hawapati na kwa watoto huduma hiyo vile vile haipatikani.

Tunaiomba Wizara husika ichukue utaratibu mzuri wa kuweza kuhakikisha kwamba, huduma hizi zilizopitishwa ndani ya Bunge hili ziwe zinapatikana bure na wapate kwa wakati. Wanapofika hospitalini wengine wanaishia kumwona Daktari na kuandikiwa vyeti kwenda kununua dawa nje ya hospitali. Dawa hazipo mahospitalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo pia suala la ujenzi wa Vituo vya Afya na Zahanati. Zoezi hili halitekelezeki na pale linapotekelezeka vituo hivi havifanyi kazi. Ningependa kuishauri Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuwa, ni vizuri tuhakikishe kwamba Vituo vya Afya na Zahanati zilizojengwa ba zinafanya kazi, zinapata dawa za kutosha na zina wahudumu, kwa

sababu kwa sasa zipo Zanahati nyingi na Vituo vya Afya zimejengwa, lakini hazitumiki. Haya ni matumizi mabaya sana ya fedha za Serikali, hatuoni *value for money* kwa sababu hazifanyi kazi. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja, tulipokuwa kwenye kampeni ya uchaguzi wa Jimbo la Arumeru Mashariki, kipo Kituo cha Afya katika Kata ya Mkorisambo kimeanza kujengwa toka mwaka 1980, Enzi ya Mwalimu, akaja Mzee Mwinyi, akaja Mzee Mkapa na sasa ni Rais Kikwete, huwezi kuamini Kituo kile hakijaanza kufanya kazi! *(Makofi)*

Mbunge wa Jimbo la Arumeru alikuwa hajazaliwa, amezaliwa, amekwenda shule na leo ni Mbunge ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano, kituo kile hakifanyi kazi! Hii ni aibu kubwa sana, tunapitisha fedha hazifikii malengo, kwa sababu wananchi wa eneo lile hawapati huduma ya afya kwa karibu, wanahangaika kwenda mbali na kituo kipo pale. Kwa hiyo, tungeiomba Serikali na Wizara husika kuhakikisha kwamba, fedha zinazotengwa zinakwenda kufanya zile kazi na vituo vikamilike kwa wakati na wananchi wapate huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niongelee Hospitali ya Mkoa wetu wa Kilimajaro, Hospitali ya Mawenzi. Bajeti iliyopita nilikataa kuunga mkono na leo itakuwa hivyo hivyo. Nampongeza Naibu Waziri wa TAMISEMI, kaka yangu Mheshimiwa Aggrey Mwanri, baada ya kuondoa shilingi mwaka jana aliahidi kwenda kufanya ziara Hospitali ya Mawenzi, kweli

alifika na tuliongozana nae kwenda kukagua maeneo ya Hospitali ile.

Mhesshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kuwa, Hospitali ya Mawezi ilianza mwaka 1920 ikiwa kama Zahanati, lakini mwaka 1956 ilipandishwa na kuwa Kituo cha Afya. Ninapozungumza sasa ndiyo Hospitali yetu ya Mkoa. Hospitali hii imeanza muda mrefu na ukiona mazingira na majengo yake yamechakaa sana. Kwanza, imepitwa na wakati wodi zake ni ndogo, kuna msongamano mkubwa sana wa wagonjwa, lakini pia hata ofisi za Madaktari bado ni tatizo, zinavuja na tulipata malalamiko hayo mbele ya Naibu Waziri na aliahidi kuyashughulikia sijui amefikia wapi? Ninaamini atakapokuwa anajumuisha atatupa majibu. Bado wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro wanataka kujua.

Bajeti iliyopita nilikuwa naulizia Jengo la *Theatre,* Jengo hili lilikuwa jiko likafanyiwa marekebisho ikawa *theatre,* lakini walipokuwa wanapita wakaguzi kutoka Wizara ya Afya, waliifunga *theatre* ile toka mwaka 2010 mpaka hivi sasa ninavyozungumza Hospitali yetu ya Mkoa wa Mawenzi haina *theatre.* Tunategemea Hospitali za Watu Binafsi na Hospitali ya Rufaa ya KCMC ambayo tunazidi kuwaongezea Madaktari majukumu makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningetaka kujua; *theatre* yetu bado haijakamilika na ili ikamilike tunahitaji zaidi ya shilingi bilioni moja. Jengo lingine la Hospitali ya Mkoa ambalo limeanza kujengwa ni wazazi

nalo halijakamilika, fedha zilizotengwa ni kidogo, Wananchi wa Mkoa wa Kilimajaro wanataka kujua. Je, fedha hizi lini zitakamilika ili Hospitali yetu ya Mkoa iweze kufanya kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetengewa shilingi milioni 7.1, *theater* tu yenyewe inahitaji shilingi bilioni moja kukamilika iweze kufanya kazi. Je, Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi inawaambia nini Wananchi wa Mkoa wa Kilimajaro wategemee fedha zitakwenda lini ili Hospitali yetu hii iweze kufanya kazi vizuri?

Mheshimiwa Mwneyekiti, tulipata pia matatizo ya wafanyakazi, wanalalamika kuhusu kupandishwa vyeo na kutolipwa mishahara yao kwa wakati. Hili nalo ningeomba Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa tulikuwa nae kule na matatizo aliyasikia ni vizuri yakapitiwa majibu, kwa sababu wanasema tumekwenda lakini hakuna chochote kinachofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie kidogo kuhusu suala la elimu; elimu yetu imeendelea kushuka, kwenye matangazo ya redio na televisheni tunaambiwa kwamba watoto wanamaliza darasa la saba lakini hawajui kusoma na kuandika. Hii ni aibu kwa Taifa. (*Makofi*)

Hata juzi imeoneshwa kwenye vyombo vya habari kwamba, asilimia 43 ya watu wazima kutoka Mkoa wa Kilimanjaro, ambao tunaambiwa wameendelea hawajui kusoma na kuandika. Sasa kwa hali hii, Taifa linakoelekea ni kubaya. Mimi nafikiri ufike wakati sasa wa kuangalia ni sababu zipi za msingi zinazosababisha

elimu yetu kushuka. Kwanza, tuangalie walimu wetu wanaishi kwenye mazingira gani; mwalimu anakwenda shule hajui mahali pa kulala, analala kwenye nyumba za udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaunga mkono hoja mpaka nitakapopewa majibu. Nakushukuru. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba niombe mwongozo kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 49(2), Kanuni ya 64(1)(c) na Kanuni ya 116, kwa ruhusa yako naomba nizinukuu Kanuni husika: Kanuni ya 49(2) inasema kuhusiana na kauli za Mawaziri. "Kauli za aina hiyo zinaweza kutolewa kwa idhini ya Spika katika wakati unaofaa kufuatana na mpangilio wa Shughuli za Bunge na zitahusu jambo mahususi, halisi na zisizozua mjadala na muda wa kusema utakuwa ni dakika zisizozidi thelathini."

Kanuni ya 64(1)(c) inasema kwamba, naomba kunukuu: "Mbunge hatazungumzia jambo lolote ambalo linasubiri uamuzi wa Mahakama au jambo lolote ambalo lilijadiliwa na kutolewa maamuzi kwenye Mkutano uliopo au uliotangulia na ambalo halikuletwa rasmi kwa njia ya hoja mahususi na vilevile hatapinga uamuzi wowote uliofanywa na Bunge, isipokuwa tu kwa kutoa hoja mahususi inayopendekeza kuwa uamuzi huo uangaliwe upya."

Kanuni ya 116 inasema kwamba: “Mbali na majukumu ya msingi ambayo yameorodheshwa kwa kila Kamati ya Kudumu, Kamati yoyote inaweza kupendekeza kwa Spika ipewe majukumu ya nyongeza ambayo yatatajwa katika pendekezo hilo na vile vile Spika anaweza kukabidhi jambo lingine lolote kwa Kamati yoyote kwa kadiri atakavyoona inafaa, kwa ajili ya kushughulikiwa na Kamati hiyo.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kuhusiana na masuala yanayohusiana na Kauli za Mawaziri kwa kurejea Kanuni hizo nilizozitaja. Mosi, siku ya leo kumetolewa Kauli ya Waziri kuhusiana na kushuka kwa bei ya samaki aina ya Sangara kwenye Ukanda wa Ziwa Victoria. Sasa kwa lugha ya kawaida, taarifa au kauli hizi zinapaswa zisizue mjadala na kwa maneno mengine hazijadiliwi. Taarifa iliyowasilishwa ina mambo yenye kuzua mjadala na baada ya taarifa hii kutolewa, binafsi nimetumiwa *messages* kutoka nyumbani Mwanza na baada ya kutumiwa nikatoka hapa nikawa na mashaka na nilichoelezwa, nikafanya *consultation* na Wabunge wa Mwanza na ndiyo maana uliona nilikuwa nimehama kwenye kiti nimeenda kuzungumza na Mbunge wa Ilemela, Mheshimiwa Highness Kiwia. Naye amenieleza kwamba, haya yanayoitwa makubaliano baina ya Serikali na Wavuvi au Chama cha Wavuvi, kuna maeneo kadhaa ambayo bado yana mjadala na bado yanabishaniwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitaomba utoe mwongozo kama ambavyo iliwahi kutolewa kwenye kauli iliyotolewa na Serikali kuhusiana na suala la rada

ambapo kauli ilipelekwa kwenye Kamati husika ya Bunge na Kamati husika ya Bunge ikapewa jukumu la kuishughulikia kauli ile. Kwa makando makando yaliyojitokeza ambayo ukihitaji naweza kukuandikia rasmi kimaandishi kwa urefu mambo gani ambayo bado yana ubishani na bado yanaweza kuzua migogoro isiyokuwa ya lazima, uweze kuelekeza kauli hii ipelekwe kwa Kamati ya Kilimo, Uvuvi na Mifugo ikaijadili na iweze kutoa ushauri kwa Serikali na mapendekezo kama sehemu ya wajibu wa Bunge kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 63(2) ya kuishauri na kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala hili hili la Kauli ya Mawaziri, umetoa tangazo leo kwamba Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii inakutana na utakumbuka ilitolewa Kauli ya Mawaziri, jambo hili limetokea...

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Mnyika, kwa utaratibu wa mwongozo ni jambo moja, sasa naona…

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo moja linalohusu Kauli za Mawaziri.

**MWENYEKITI**: *Concept* ya hilo jambo moja umeshazungumza linahusu suala la kauli iliyotolewa hapa Bungeni leo. Hebu ngoja Mheshimiwa Mnyika, kwa utaratibu ni kwamba, jambo unalotakiwa kupatiwa mwongozo ni lile ambalo limetolewa leo Bungeni na kwa mantiki ya shughuli ambayo imetolewa leo hapa Bungeni ni kauli inayohusu masuala ya biashara ya samaki. Sasa ukianza kuhama

kwenye biashara ya samaki uka-*take advantage* ya Kauli za Mawaziri, ukataka tena kuingiza na hoja nyingine, hapo hatutaelewana.

Tutakiuka misingi ya maadili ya uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge, naomba ubaki kwenye hiyo hoja ambayo ndiyo hoja iliyoko leo hapa Bungeni, kama kutakuwa na hoja nyingine inayohusu hicho unachotaka kukisema, una nafasi ya kushauri itakapokuwa imeletwa. Kwa hiyo, naomba niku-*limit* uendelee kutunza Kanuni, uende pale ambapo hoja yako imejikita.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nitaomba Taarifa ya Kamati hii baada ya mwongozo wako wa Kamati kulishughulikia hili jambo kwa haraka iletwe Bungeni ili tuweze kuijadili; na kwa sababu umesema nizungumze jambo moja tu, nitaiandikia rasmi Ofisi ya Spika kuhusu suala la mgomo wa Madaktari ambalo vile vile Kauli ya Mawaziri iliyotolewa Bungeni ina mambo yanayohitaji kujadili kwa sababu mgomo unaendelea na bado kuna utata mwingi sana. Kwa hiyo, hili nitaliandikia rasmi.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Mnyika, unajua wewe unazijua Kanuni, naomba uwe unafuata Kanuni na uwe unatii maelezo ya Kiti. Wakati mwingine huwa unaanzisha migogoro isiyokuwa na sababu. Baada ya kukukatalia bado umeendelea ilimradi tu usikike kile ulichotaka kusema! Sasa huo siyo utaratibu mzuri na niendelee kukuomba sana, utaratibu mzuri wa Mbunge yeyote makini ni kutii utaratibu na Sheria mahali anapofanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mnyika, nimekuelewa na ukianza na ile Kanuni ya 49 imejiweka wazi kabisa inasema, kauli ya namna hiyo inaweza kutolewa kwa idhini ya Spika na mmeona Spika ametoa idhini kauli imetolewa na inasema idhini hiyo itatolewa wakati unaofaa kufuatana na mpangilio wa Shughuli za Bunge na mpangilio wa Shughuli za Bunge mmeona hapa tumeufuata kabisa na zitahusu jambo mahususi na tumeona hili jambo la biashara ya samaki kwa wavuvi wetu kule ni jambo mahususi, lakini halitaruhusu mjadala kama wewe mwenyewe ulivyosema.

Sasa nakubaliana na wewe kwamba hoja hii inaweza kuwa ni hoja ambayo inatakiwa kufanyiwa kazi kwa kina. Mheshimiwa Mnyika, nadhani kwa busara ya Kiti, Mheshimiwa Waziri hapa ametuambia kabla ya tarehe 5 atakuwa ameshafika Mwanza na atakuwa ameshapata nafasi ya kukutana na wadau wote wa samaki kule na kulishughulikia suala hilo kwa makini. Kauli imekuwa wazi na imeonesha hivyo. Nilikuwa nasuburi sana kwenye Kauli ya Mheshimiwa Waziri, asingesema kwamba anaondoka haraka kwenda kule Mwanza, kwa kweli hata mimi ningemshangaa na Watanzania wote wangemshangaa.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema anakwenda kule na amesema suala hili mpaka kufika tarehe 5 litakuwa limeshapatiwa mwafaka, hebu tumpe nafasi alifanyie kazi na kama mpaka hiyo tarehe 5 litakuwa halijapatiwa ufumbuzi wowote, sisi kama Wabunge tunayo nafasi ya kumshauri Waziri na

kuishauri Serikali yetu. Kwanza, tumpongeze kwamba hata jana ametumia muda mrefu kufanya *consultation* na wadau hao, amefanya nao kikao, kwa taarifa za ofisi yetu hapa amefanya nao kikao kwa takriban saa sita wakijadiliana suala hili. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mnyika, nilifikiri hata wewe hapa ungesimama kwa kuanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hatua hizo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, pale ambapo Serikali ama Waziri mhusika ametumia juhudi ya kushughulikia tatizo fulani, tuwe na tabia ya kuwapongeza na pale ambapo wanaonesha kwamba hawajaendana na kasi ya kushughulikia matatizo, tuna nafasi ya kuwashauri na kuwataka wafanye hivyo kwa haraka. Kwa hiyo, naomba mwongozo wangu ubaki kwamba, tumpe Mheshimiwa Waziri nafasi kama kauli yake ilivyosema na mpaka kufika tarehe 5, tatizo hili kama litakuwa halijafanyiwa ufumbuzi, tutahitaji kufanya jambo lingine la ziada, kuokoa biashara hiyo muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu na kwa maendeleo ya wavuvi wetu.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuendelee. Sikumtaja msemaji anayefuata, nafikiri baada ya mwongozo huo, sasa nimpe nafasi Mheshimiwa Assumpter Mshama, atafuatiwa na Mheshimiwa Ole-Telele.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, ninayo shukrani kubwa mbele za Mungu na mbele ya Bunge lako

Tukufu, kupata nafasi ya kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na hali ya uchumi. Pato halisia la Taifa, limepungua kwa takriban asilimia 0.6 na pato kutokana na kilimo, limepungua asilimia hiyo hiyo 0.6. Katika maelezo ya Kitabu cha Waziri Mkuu, inasemekana ni kwa sababu ya ukame na mambo ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize; kuchelewa kwa mbolea kwenda kwa wakulima ni tatizo la umeme? Kuchelewa kwa pembejeo kwenda kwa wakulima ni tatizo la umeme na tatizo la ukame? Kuchelewa kutokutoa elimu ya kutosha kwa wakulima walime nini kuzingatia hali ya hewa ilivyobadilika, tabia ya nchi hilo ni tatizo la umeme na ukame? Mimi ninadhani kwa suala la uchumi ni ukosefu wa mipango mizuri ya kiuchumi ndiyo uliosababisha tukaingia katika hasara ya kupoteza Pato la Taifa kwa asilimia hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye nafasi za watu katika majukumu yao. Mimi ningependa tu kusema, wakati mwingine tunatakiwa kuwa waangalifu kwa nafasi za watu au kwa watendaji katika kazi zao. Kwa mfano, unashangaa kuona Mtendaji mahali fulani au katika Mkoa mmoja, zinapotea shilingi bilioni sita, lakini Mtendaji hana habari. Wakati mwingine uwezo wa kutambua mambo ni mdogo. Kwa hiyo, ninashauri viwepo vigezo vya watu kupata nafasi zao na kufanya kazi kulingana na uwezo na weledi walionao ili tuweze kuongeza uchumi katika Taifa letu. Kama mtu atakuwa pale kwa sababu amekuwepo na matokeo yake

maendeleo katika eneo husika hayatakuwepo, tunahitaji watu na weledi na wawe na ubunifu na wawe na uwezo wa kufanya kazi wanazopewa ili tuweze kupata uchumi wa kutosha katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika suala la usafiri na usafirishaji. Tunao mkakati mzuri wa kuhakikisha Bandari zetu zinaenda vizuri. Tunao mkakati mzuri wa kuhakikisha tunatengeneza barabara, lakini kuna vikwazo ambavyo haviwezi kumfanya mfanyabiashara aiamini safari yake ya kutoka hapa kwenda Burundi, kutoka Dar es Salaam kuelekea Burundi. Njiani anakutana na mikono zaidi ya 50, kila kituo anasimama anatoa rushwa; bila kuondoa rushwa za barabarani, hatuwezi kupata maendeleo kupitia usafiri na usafirishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie ukweli; kuna wakati naudhika kweli, mimi mwenyewe nikitoka Dar es Salaam kuja hapa Dodoma, unakutana na mikono zaidi ya 15. Huyu mtu kama ana lori anasafirisha mizigo kwenda Burundi atasimama mara ngapi barabarani? Mimi ningeomba Waziri mhusika, ashughulike na rushwa za barabarani, zimetuchosha na hatuwezi kuendeleza uchumi kwa kutumia barabara kama hilo suala halitashughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la maji. Maji sana sana katika nchi hii anayeumia zaidi ni mwanamke. Ukitembea mahali pote, wakati mwingine kuna maeneo ambayo mwanamke akiondoka kwenda kuchota maji, anarudi jioni.

Mzalishaji mkubwa na mwongezaji wa uchumi wa Taifa hili ni mwanamke. Tangu asubuhi amekwenda kwenye maji anarudi jioni ataongezaje uchumi katika maisha yake au katika Kaya yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja niseme; kule kwangu katika Kata ya Kirimile na Kakunyu, wana Mradi wa *World Bank,* wamewachimbia maji yamebaki pale kama sinema. Kwa kuwa wale wananchi hawana uwezo wa kufikisha hiyo asilimia 20 wamebaki na maji pale wanayaangalia, hawawezi kuyatumia kwa sababu hayajasambazwa kwenye maeneo yao. Ninaiomba Serikali iwalipie hiyo hela iliyobaki, lakini maji walipie kidogokidogo na hatimaye watimize ile pesa ambayo wanadaiwa, wakamiliki yale maji kuliko kubaki pale wanayaangalia na hayawasaidii kitu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongelee suala la elimu. Elimu yetu Tanzania tunalalamika lakini hatujachunguza vizuri ni kwa nini watu hawaendi kwenye vijiji? Nadhani mwaka jana nilipoangalia takwimu za Lesotho, nilitoa Malawi, nikaangalia Uganda ni namna gani wameongeza *incentives,* wamewawezeshaje kuwapa *morale* wale wanaofundisha vijijini wakaongezea ki-*percent* kidogo ili wawe na *morale* ya kwenda kufundisha vijijini.

Mheshimiwa mwenyekiti, mwalimu anayefundisha Dar es Salaam anapata mshahara sawasawa na mwalimu anayefundisha Kakunyu. Kutoka Kakunyu kuja kwenye Benki kuchukua mshahara wake ni lazima alale

pale Kyaka. Je, huyu mwanamke au mwanaume aliyesafiri na pesa yake ya nauli kuja kutafuta mshahara wake unamlinganishaje na mtu anayetumia *message* tu kuingiza hela kwenye akaunti yake? Kwa hiyo, nilichokuwa ninaiomba Serikali, tuangalie ni namna gani tunaweza kuongeza kitu kidogo ili tuwatie *morale* wale walimu wakubali kwenda vijijini. Nchi nyingine kama Lesotho, wamewalipa mara mbili; Uganda, wameongeza asilimia 30 ya mshahara wa mwalimu. Kwa nini tusiongeze ili walimu wajisikie vizuri kwamba hata sisi tumeweza kufikiriwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba sana sana tuongeze kitu kidogo kwa walimu nao wajisikie vizuri kwenda katika maeneo hayo. Siyo hilo tu, kwa mfano, mwalimu ambaye amekataa kwenda kwenye Kituo chake tunamfanyaje? Hao walimu wamefundishwa kwa posho ya nchi yetu, wamepata pesa, wameenda chuo kwa kutumia hela ya Watanzania. Unapompa nafasi ya kwenda kule kwangu Bugorora, anakataa kwenda na anaenda shule ya *private* na anaachwa huko, hakuna linalotendeka. Kwa hiyo, naishauri Serikali ni kwa nini tusiwape Mkataba wa miaka mitano, wajue kwamba kwa miaka mitano nitakuwa *posted* popote na baada ya hapo tunamwacha aende kwa sababu atakuwa ameshatutumikia na tumeona yale matunda yetu ya kumsomesha bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa ninashauri kwa suala la elimu, walimu ambao wanagoma kwenda kwenye maeneo, tuanze Mkataba kabla hawajachukua hela ya mkopo.

Akikubali ndipo tumpe mkopo na tukijua kwamba, shule zetu za pembezoni zitapata walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilitaka kuliongelea ni suala la kahawa. Katika Tanzania hii, Mkoa wetu wa Kagera, zao kubwa la uchumi ni kahawa. Huwezi kuamini, katika Soko la Dunia mwaka huu mmepata pesa nyingi kuliko mwaka jana. Mwaka huu ndiyo mmeshusha bei ya kahawa kutoka shilingi 1,350 imekwenda shilingi 1,300; kuna sababu gani ya kimsingi ambayo mmeitumia hata kushusha kahawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu. Kwanza, naunga mkono Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu, lakini nataka kusema haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, inavyoonekana ni kwamba, mabadiliko ya Tabia Nchi, yataendelea kuathiri Uchumi wa Tanzania na siyo Tanzania tu inaonekana ni tatizo la Dunia nzima hasa kwa upande wa kilimo na mifugo. Kwa hiyo, hali ya njaa itaendelea kuwepo, lakini hatuna namna ni lazima tufanye *adaptation* au mambo ya *mitigation* katika masuala ya Tabia Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua hii, naishukuru sana Serikali kwa jinsi ambavyo imekuja na ile hoja. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa

sababu alisukuma jambo hili la kutoa mifugo kufidia hali mbaya ambayo tulikuwa tumepata katika Wilaya hizi tatu. Najua ukame umekabili maeneo mengi sana nchini, lakini wafugaji kwa kiasi kikubwa, wameathirika katika hizi Wilaya tatu; Longido, Ngorongoro na Monduli. Kuna Wilaya 55 ambazo zipo katika Hotuba ya Waziri Mkuu, ambazo pia zimeathirika. Serikali imechukua hatua ya haraka kutufidia hiyo mifugo. Japo tuanaanza na mifugo 500, lakini kwa Wilaya ya Ngorongoro, kutokana na *Task Force* ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ilikuwa nipate mifugo zaidi ya 7,000. Hapa tukianzia na hao 500 na tumeshahakikishiwa kwamba, katika bajeti ijayo, Serikali itaendelea kuangalia namna ya kuweka mifugo mingi zaidi kwa ajili ya kuwasaidia hawa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, tulipokabiliwa na suala zima la njaa, Serikali imeingilia kati. Namshukuru sana Waziri wa Kilimo, ametusaidia sisi watu wa Ngorongoro, hatulimi huko, hatufanyi biashara yoyote, tumepata magunia 36,000 au tani 3,600; ni shukrani kubwa sana kwa Serikali. Naomba mwendelee kutuangalia mpaka hapo suala la bustani hizi ndogondogo kule Ngorongoro, Mheshimiwa Rais, atakapolitolea tamko.

Mheshimiwa mwenyekiti, naishukuru pia Serikali, nimepata umeme kule Loliondo, japo ni wa jenereta, lakini si haba. Nimepata jenereta mpya nne, huo umeme ni mwingi sana. Naomba sasa Waziri wa Nishati, atusaidie kuweka msukumo kupata nguzo za kusambaza huo umeme katika Miji ya Loliondo Mjini, huko Uwaso ambao ni Mji unaokua haraka sana ni Mji

wa Biashara. Tangu wamesikia kwamba, huenda barabara ya lami ikapita pale, basi hali ya hewa ya huko, kwanza nawakaribisha karibuni sana ni mahali pazuri.

Ninaomba sana suala la nguzo na mita, Waziri anayehusika, atusaidie kusukuma tuweze kupata kwa sababu ndiyo tatizo kubwa sana hivi sasa. Tunashindwa kusambaza umeme katika Mji wa Loliondo, ambao ni Makao Makuu ya Wilaya, katika Mji wa Uwaso, katika Kijiji cha Sakala na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kupeleka huo umeme kwa sababu ni mwingi sana; tupeleke huko Digodigo, kwa Wabatemi, ambao wamejenga nyumba nzuri sana. Tupeleke Samunge, wamejenga nyumba nzuri sana na maeneo mengine ambako wananchi wamejenga nyumba zao nzuri. Hata Hoteli ambazo ziko jirani na *Lodging* ambazo ziko jirani, tunategemea kupeleka huu umeme, lakini tunahitaji nguzo haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naishukuru Serikali, kupitia *REA,* wametuongezea muda wa ile ofa ya kuwapa wananchi kwa bei nafuu, shilingi 75,000 hivi *against* shilingi 400,000 ya kuvuta umeme. Wametuongezea muda na ninawaomba Wananchi wa Miji ya Loliondo na Waso na huko ambako tunataka kupeleka huu umeme, wachangamkie hiyo tenda; vinginevyo, tunapiga kelele huku, inaletwa huko, halafu jitihada hazionekani. Nawaomba wananchi mkishapata nguzo na mita, fanyeni hiyo kazi kwa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mto wa Mbu – Loliondo – Mugumu – Makutano huko Musoma, ninaishukuru Serikali imeiangalia. Tangu miaka ya 1980, Serikali, ilikuwa na mpango wa kujenga barabara hii, lakini ikakaa tu kwa sababu mbalimbali. Serikali hiyo hiyo kwa nia njema, imefika mahali tena ikaibua Mradi huu ambao ni mkubwa sana.

Mheshimiwa mwenyekiti, ninashangaa watu wanaopiga kelele, barabara hii itaharibu mazingira. Barabara hii, mkijenga wanyama watagongwa. Wilaya ya Ngorongoro tangu mwaka 1979, hakuna Mradi wowote mkubwa wa Serikali, ni huu tu ambao sasa unakuja na umeme. Ninashukuru kwamba, tangu nimeingia, mambo yote yanaingia kwa wakati mmoja. Naishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, jambo hili lipo kwenye Ilani na nina hakika haliwezi kuondolewa, badala yake litatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amejitahidi sana katika jambo hili. Naomba Bunge hili litusaidie barabara hii iweze kujengwa kwa sababu itakuwa ni ukombozi mkubwa katika masuala yote kwa Wananchi wa Ngorongoro na watu ambao wako maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii habari ya kupotosha ya kuipa jina *Serengeti High Way, Serengeti Super High Way,* ndiyo hii imewakasirisha wafadhili huko, imewakasirisha Wazungu, wakati hii barabara haipiti katikati ya Serengeti. Kuna kilometa 55, Rais amesema na Serikali imesema, hatutajenga kwa kiwango cha

lami. Barabara hii itaanzia Mto wa Mbu, itapita Ngaresero, itakwenda Loliondo. Ikifikia Clans Camp, wataruka watakwenda upande wa Mugumu na kuelekea Musoma. Sasa kelele za nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yetu, isiwaogope Serikali ya Kenya au jirani zetu hapa, wala *International Communities,* ambazo zinahusika na wanyamapori na suala la mazingira. Kwa nini muwaogope? Hawa wenzetu wanatekeleza Miradi yao wanavyopanga. Wanajenga uwanja mkubwa sana Taveta hapa, tunajua huu uwanja unaweza ukaathiri *Kilimanjaro International Airport,* lakini ni nani amewaingilia? Nani amewasema? Kwa nini wao watuseme?

Serikali iache uwoga, isimamie mambo yake. Hii ni nyumba yetu na ni nyumba ya Serikali ya Tanzania, lazima tufanye hiyo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemaliza hilo la barabara, sasa habari ya rada. Pesa za rada kama walivyosema wenzangu wengi, ziende kwenye madawati na nyumba za walimu. *Stop,* siyo *full stop,* mimi mwenyewe hivyo vitabu kuna watu wanajitolea tu kvileta na vitabu wanavyovileta hata pengine haviendani na silabasi za kwetu tunazozitaka. Sasa tujengewe kwanza nyumba za walimu, walimu wetu wapate mahali pa kukaa na halafu hayo mambo mengine yatajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, suala la maji *World Bank.* Inaonekana huu Mradi, niseme labda

umeshindwa, *unless,* mnanihakikishia kama Serikali, haujashindwa. Mimi kule kwangu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, kengele ya pili.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, pole sana kwa sababu kasi ya mchango ilivyokuwa inazidi kwenda juu na muda ndivyo ulivyokuwa unazidi kwisha.

Waheshimiwa Wabunge, nilisema nitamwita Mheshimiwa Amina Mwidau, atafuatiwa na Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga; aah, anaanza Mheshimiwa Massauni, halafu Mheshimiwa Amina Mwidau.

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mchango wangu utajikita zaidi katika eneo la uwekezaji na uwezeshaji wananchi kiuchumi; nikiamini kabisa kwamba, eneo hili ikiwa tutalipa nguvu za kipekee, litasaidia sana kuweza kukabiliana na tatizo la ajira hasa kwa vijana. Tatizo ambalo limekuwa likijulikana siku hizi kama ni bomu la masafa marefu, ambalo limeshaanza kulipuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kulizungumzia suala hili la uwekezaji na uwezeshaji wananchi kiuchumi, nitaomba niligawe katika maeneo mawili. Eneo la kwanza ni jinsi ambavyo mikakati yetu ya kuweza kuvutia wawekezaji hasa katika zile sekta ambazo zinatoa ajira sana kwa vijana, ikiwemo kilimo na viwanda.

Eneo la pili, nitajikita katika mikakati ambayo inalenga katika kuhamasisha, kushajihisha, kuwajengea uwezo na kuwawezesha vikundi mbalimbali, ikiwemo Vikundi vya Ushirika, Vikundi vya *SACCOS,* Vikundi vya Ujasiriamali wa Kati na Wadogo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili la kwanza la uwekezaji, mimi nafikiri taasisi yetu hii ya *TIC* bado haijafanya kazi vizuri sana. Lakini pia linachangiwa zaidi kutokana na sheria ambazo tunazo leo. Sheria zetu hizi za Uwekezaji zinatoa mwanya mkubwa sana wa upotevu wa matrilioni ya pesa kwa kisingizio cha hizi *tax incentives* ambazo tunazo hasa kwa wawekezaji wa nje. Haiingi akilini hata kidogo kwamba leo nchi yetu inapoteza fedha nyingi sana kwa kisingizio cha kuvutia wawekezaji, kiasi cha takribani dola bilioni moja nukta tatu. Ukiangalia katika Afrika Mashariki nchi yetu ndiyo katika nchi za nyuma ambazo zinapokea wawekezaji wengi zaidi, Rwanda inaongoza hata Uganda wametushinda. Sasa kwa kweli suala hili inapaswa tuliangalie kwa umakini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha ambazo tutapoteza kupitia *TIC*, kupitia *Special Economic Zone*, kupitia EPZ, kupitia kwenye madini na maeneo

mengine mengi tafsiri yake ni nini? Tafsiri yake ni kwamba fedha hizi ni kama ruzuku ambayo Serikali ingeweza kuitumia kuwekeza katika miradi mbalimbali ya miundombinu, kuwekeza katika elimu na zingeweza kuleta tija kubwa sana hasa katika eneo la kuajiri vijana. Mbali na kuwa fedha hizi haziko mbali lakini pia haziwezi kuhakikiwa na Bunge hili Tukufu. Ni wajibu sasa wa Serikali yetu, mimi naunga mkono mapendekezo ambayo yamekuwa yakitolewa kila mwaka hapa kwamba wakati umefika kwa Serikali hii kufanya utafiti wa kina ili kuweza kubaini hasara na faida za misamaha hii. Ni lazima utafiti huu uainishe na kubaini ni nani ambaye anafaidika na sekta gani. Kila siku kutuletea takwimu tu ambazo zinaonyesha kwamba kuna ajira 89,000 ambazo zimepatikana mpaka sasa hivi bila kuweka ulinganisho na hasara hii ya upotevu wa fedha hizi, mimi nafikiri haijatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni hili la kuwezesha vikundi hivi vya ushirika, vya ujasiriamali na vikundi vya kuweka na kukopa. Juhudi hizi ambazo ofisi ya Waziri Mkuu, kupitia Wizara hii ya Uwezeshaji na Uwekezaji imeanzisha za kuhakikisha kwamba inasaidia wajasiriamali hawa, ni vyema zikaenda sambamba na jitihada ambazo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Uwezeshaji kule zinafanywa. Kwa mfano, kuna fedha takribani shilingi bilioni saba nukta tatu zimetolewa kwa ajili ya kuwezesha vikundi mbalimbali kwa Mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara, fedha hizi nafikiri zingepaswa pia kupelekwa Zanzibar, kama vile pesa za rada ambazo wenzangu wengine wamechangia. Labda mwingine anaweza akauliza tu kwamba hizi jitihada za kuunganisha juhudi za Serikali

hizi mbili zinakwenda vipi? Mwingine anaweza aka-*argue* kwamba lakini kule si kuna Wizara ya Uwezeshaji, mimi nafikiri hoja hii ndiyo inaongezea ule uzito wa hizi changamoto za Muungano ambapo sasa wakati huu wa mabadiliko ya Katiba inapaswa wananchi wawe makini sana ili tuweze kuja na mfumo ambao utaainisha kabisa ushiriki wa Zanzibar katika mambo ya nje Kikatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Waziri wa Kazi yule pale, anatuambia kama suala hili la Wizara hii ya Uwekezaji au Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo mimi kwa uelewa wangu hii ni Wizara ama hii ni ofisi ambayo ni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo Zanzibar, leo hii Waziri wa Kazi anapotuwasilisha katika mkutano labda waseme wa Shirika la Kazi Duniani *(ILO),* anakwenda pale kwa niaba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo Zanzibar. Hata kama ataambatana na uwakilishi kutoka Zanzibar, basi hiyo itaendelea kubakia tu kama ni desturi ama ni hisani lakini haipo kama ni matakwa ya Kikatiba. Mifano iko mingi, sikusidii kutoka nje ya mchango wangu lakini leo hii kuna mipango mizuri tu, kuna fikra nzuri Zanzibar kujiunga na *FIFA*, kujiunga na *OIC* lakini mambo haya yamekosa msingi wa mfumo wa Kikatiba, ni mambo ambayo tutataka tuyaangalie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi katika hoja yangu ya msingi, leo hii nimesimama mbele yenu nikijivunia sanasana jitihada ambazo wananchi wa Jimbo la Kikwajuni tumeweza kupiga katika kuhakikisha kwamba tunakabiliana na changamoto hii ya ajira hasa kwa vijana. Tumejaribu kuandaa mkakati makini

kabisa na kabambe ambao una lengo la kuwezesha kuwajengea uwezo vijana pamoja na kuweza kuandaa mazingira mazuri ya kuwezesha na tunatoa shukrani kwa taasisi mbalimbali ambazo zimeshirikiana na sisi kuunga mkono juhudi zetu. Nitoe wito tu kwa Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kuunga juhudi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye na yeye kwa kuona umuhimu wa programu yetu hii, ameahidi kutusaidia na aweze kushirikiana na taasisi hii kuweza kufanikisha malengo ambayo tumeanzisha. Lengo ni moja tu kuona kwamba jinsi gani tunawakomboa vijana wetu katika uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la msingi ambalo najaribu kulizungumzia kabla muda wangu haujaisha, *VETA* imejaribu kufanya kazi kubwa sanasana katika kuwajengea uwezo vijana lakini kuna Sheria hii ya *Skill Development Levy* ambapo *VETA* wanapata *one third* ya asilimia sita kutoka kwenye Mfuko Huu. Mimi nafikiri wakati umefika sasa kwa sheria hii kuangaliwa ili *VETA* waweze kukusanya fedha nyingi ili waweze kuendeleza kazi nzuri ambayo wamekuwa wakifanya kwa muda mrefu. *VETA* sasa inapata tabu sana kusaidia taasisi kama hii ambayo tumeianzisha katika Jimbo langu ambayo iko nje ya mfumo, ni taasisi ambayo isiyo ya Serikali naamini kabisa tukiweza kuongezea uwezo *VETA* itaweza kusaidia sana taasisi nyingine ambazo hata si za Kiserikali kuweza kutimiza malengo ambayo tumeyakusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa kabla ya kumalizia, naomba nichukue fursa hii kuipongeza

Serikali maana mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa mikakati yake ambayo imeelekea katika kuandaa fursa mbalimbali za mikopo, ikiwa mikopo ya Benki ya Rasilimali, mikopo ya Benki ya Posta pamoja na Mfuko wa Uwezeshaji ikiwa ina malengo ya kusaidia kuwakwamua hawa vijana na hasa kinamama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa juhudi hizi za kuwajengea uwezo ambazo tumezianzisha sisi katika Jimbo la Kikwajuni lakini pia Serikali kuzipa uwezo kupitia vyuo vya ufundi pamoja na mifuko hii ya uwezeshaji ambayo imeratibiwa na Serikali na inaendelezwa, zikiunganishwa pamoja zitasaidia sana kuandaa vijana kiuwezo lakini wakati huohuo ili waweze kutumia ujuzi wao kujiendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Masauni. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Amina atafuatiwa na Mheshimiwa Mkiwa.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa na mimi nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia wote kuwa hapa mwenye afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia, naomba nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuweza kuchukua hatua za kinidhamu za kuwawajibisha baadhi ya watendaji katika Halmashauri ambao wamekiuka maadili ya utendaji na kuwasimamisha. Pia nimpongeze kwa kuteua baadhi ya Wakurugenzi, ila masikitiko yangu makubwa, Tanga muda mrefu sana hatuna Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji. Juzi niliposikia anatangaza nilifurahi sana baadaye nikagundua kuwa Tanga hatukupewa Mkurugenzi. Namwomba Waziri Mkuu akija kufanya majumuisho hapa atuambie lini Tanga tutapata Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kama ingewezekana watu wa Tanga tungeweza kumuombea dua ili aweze kupata afya njema na Mwenyezi Mungu kwa hekima na busara alizonazo akija hapa kufanya majumuisho tarehe 1 ikiwezekana basi aje na jina kwa sababu Tanga tumechoka na Kaimu, Kaimu anakuwa anashindwa kufanya maamuzi magumu, tunaomba Mkurugenzi tafadhali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nielekee kwenye mambo ambayo nimepanga kuchangia. La kwanza, naomba kuanza na Fungu 86, Mkoa wa Tanga, kwa kweli safari hii pesa zilizotengwa ni chache sana hasa pesa za maendeleo zimepunguzwa sana, hasa ukizingatia Mkoa wa Tanga tuna Wilaya nane, kuna mamlaka za Serikali za Mitaa takriban kumi na moja, kwa pesa ambazo zimetengwa ni chache sana hasa katika miradi ya maendeleo. Mbali ya uchache

wake, vilevile ukiangalia mwaka jana hazifiki kwa wakati ambao unastahili kutoka Hazina, pesa nyingi za miradi zinachelewa kufika katika sehemu ambazo zimeelekezwa, hii inachelewesha utendaji kwa hali ya juu sana. Kama ingewezekana pesa hizi ziongezwe japo kidogo, japokuwa najua jambo hili haliwezekani lakini kama kuna uwezekano wa aina yoyote ile ingesaidia kwa sababu pesa zilizotengwa ni sawasawa kama tunatwanga maji kwenye kinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naomba nielekee kwenye afya. Tanga tuna Hospitali ya Mkoa ambayo ni Hospitali ya Rufaa ya Bombo, hospitali hii inafundisha Matibabu Wauguzi, ina changamoto nyingi sana mojawapo ikiwa ni uhaba mkubwa wa watumishi, hakuna Madaktari Bingwa, hakuna Madaktari Wasaidizi takribani wanne, hakuna Waganga, hakuna Wauguzi karibu 241 na watumishi wengine wa afya. Hii ni changamoto kubwa sana kwa Hospitali ya Rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuna msongamano mkubwa kwa sababu Wilaya ya Tanga hakuna Hospitali ya Wilaya na Mkinga vilevile hakuna Hospitali ya Wilaya, kwa hiyo, kuna msongamano mkubwa sana wa wagonjwa hasa sisi akinama ndiyo tunaathirika kwelikweli. Ukienda katika wodi ya kinamama, huwa tunasema bodaboda, mshikaki lakini hata katika wodi ya kinamama kwenye vitanda kuna mishikaki na wodi ya watoto vilevile, kwa kweli hali hii inaathiri kwa kiasi kikubwa, tunaomba Serikali ituangalie na sisi Mkoa wa Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi hakuna vitendea kazi muhimu kama *X-Tray.* Ni muda mrefu sasa hivi takribani mwaka tangu Julai, mwaka jana mpaka mwaka huu tulionao sasa hivi hakuna *X-Ray* katika Hospitali hiyo ya Rufaa, wanatumia hospitali binafsi. Kwa kweli sidhani kama Serikali inashindwa kununua *X-Ray*. Tunaomba Serikali ituangalie kwa macho mawili, matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, kabla sijaenda kwenye suala lingine katika Hospitali ya Wilaya, niwashukuru Serikali kwa kuweza kutenga angalau shilingi milioni 285 ambazo zimefanyiwa mchakato ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Vilevile katika maombi maalum ya Mkoa tumeomba shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi huo. Sasa naomba Waziri akija hapa kufanya majumuisho atuambie katika hizo pesa tulizopewa za maendeleo na hiyo shilingi bilioni moja imo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye elimu, Tanga ina historia kubwa sana ya elimu Kitaifa. Historia hiyo imeanza tangu mwaka 1980 ilipoanzishwa Shule ya Msingi Magilu ambayo ilikuwa katika Wilaya ya Muheza na shule ya kwanza ya Sekondari Tanzania kujengwa ilijengwa Tanga mwaka 1895 ambayo ilikuwa ikiitwa *Trade School* mwaka 1905, ikaitwa *Tanga School* na sasa hivi inaitwa ni *Old Tanga* ambayo iko *opposite* na uwanja wa Mkwakwani. Vilevile wafanyakazi wengi katika Mashirika ya Reli, Bandari na Posta pamoja na Makarani wengi wa Mahakama walikuwa ni wazaliwa wa Tanga. Hata viongozi wetu, baadhi ya viongozi wakubwa wa Kitaifa akiwemo

Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, amesoma Tanga, lakini leo Tanga imeshuka sana kielimu, tunaelekea mkiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu ya changamoto zilizopo Tanga, kuna changamoto kubwa sana. Kama wenzangu wengine walivyosema hapa, miundombinu na samani katika shule za msingi na sekondari hazitoshi, hakuna maktaba, hakuna nyumba za Walimu, vyoo kuna matatizo makubwa sana, mahitaji ni makubwa. Napendekeza hizi pesa za Rada zipewe Mkoa wa Tanga. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina sababu. Sababu ya kwanza, Tanga ina historia kubwa sana ya kielimu kitaifa, lakini pili Tanga ulikuwa mji wa viwanda, viwanda vyote vimekufa kwa Sera ya Ubinafsishaji. Sasa hivi tumebinafsishwa kabisa, japokuwa namshukuru Mheshimiwa ametuletea Waziri wa Viwanda na Biashara, nadhani ataiangalia Tanga kwa jicho la imani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kubwa zaidi Tanga ni Mji wa Kitaifa wakati wa Kikoloni. Watu walipoenda kwenye mkonge makabila yote yako Tanga, kwa hiyo maendeleo ya Tanga ni maendeleo ya Watanzania wote. Naomba Mheshimiwa hili lifikiriwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielekee kwenye posho za Madiwani. Naomba nigusie kidogo, namshukuru kwanza Waziri Mkuu katika hotuba yake, ukurasa wa 55 na 56 ameelezea kuwa kutakuwa na

ongezeko la posho za Madiwani. Lakini kwanza niseme shukrani kwa sababu heri moja shika tunasema sisi Waswahili wa Pwani, kuliko kumi nenda rudi. Pili hizi pesa zilizoongezwa ni kidogo kwa sababu waliokuwa wanapata...

**WABUNGE FULANI:** Ongea, ongea!

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba waongezewe.

**MWENYEKITI**: Nakushukuru sana Mheshimiwa Amina Mwidau, ama kweli tumefaidika pamoja na mchango wako lakini tumepata mithali na nahau za Kiswahili na hasa zile za mwambao wa Pwani mwa Tanzania, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilisema atafuatia Mheshimiwa Mkiwa Kiwanga, Mheshimiwa Lucy Owenya na Mheshimiwa Riziki Lulida wajiandae.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mimi naitwa Mkiwa Kimwanga na siyo Mkiwa Kiwanga.

**MWENYEKITI:** Ahsante, naomba *Hansard* warekebishe Mkiwa Kimwanga!

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu wangu kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha leo kusimama hapa na kuweza kuchangia katika bajeti hii ya Waziri Mkuu.

Pili napenda kuwapongeza wananchi wakazi wa Jiji la Mwanza kwa kuendelea kushika nafasi ya kwanza kitaifa ya Majiji Tanzania, mara saba mfululizo. Nachowaomba waendelee na uzi huohuo na waweze kutii sheria ya usafi bila shuruti. Nawapongeza sana wakazi wa Jiji la Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuishukuru Serikali kusikia kilio chetu cha muda mrefu wajumbe wa Jimbo la Ilemela na Mkoa wa Mwanza kwa ujumla na sasa wameamua kutupa Manispaa ya Jiji la Ilemela. Naomba mchakato huu ukamilike haraka iwezekanavyo ili Ilemela iweze kujitegemea kama Manispaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwanza kabisa kwenye kitabu cha hotuba ya Waziri wa Fedha, ukurasa wa 41, kipengele cha 66, ameongelea mamlaka ya Serikali za Mitaa zinahimizwa kuongeza makusanyo na mapato ya ndani kwa kuzingatia fursa zilizopo. Aidha, TAMISEMI, kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Ujerumani watakamilisha na kusambaza kwenye Halmashauri mfumo wa kompyuta wa kutunza kumbukumbu za mali na majengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Hawa Ghasia ameligusia hilo katika ukurasa wake wa 20 lakini tatizo ninalopata mimi ni

moja tu, wanataka kampuni ya Ujerumani ije itusaidie kufunga kompyuta kwenye Halmashauri zote ili kuweza kukusanya kodi za majengo na mambo mengine. Wakati huohuo napenda niulize hawa Wajerumani wanavyokuja, wanakuja kwa msaada, hawa Wajerumani wanakuja kutuchangia au kuna tutakachowachangia katika kufunga kompyuta hizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watakapokuja kufanya majumuisho, naomba wanifahamishe hili kwani kuna vijana wetu wa Kitanzania wamesoma kwa kodi za Watanzania, wanaishi katika nchi hii ya Watanzania na tunasema kwamba tunahitaji ubunifu wa vijana, tayari wamekwishabuni kitu kama hiki, nauliza hawa Wajerumani kuja Tanzania kufanya kazi ileile inayoweza kufanywa na vijana wa Kitanzania, tunawatakia Watanzania kheri? Ni kwa sababu gani tukae tunasomesha vijana wa Kitanzania na tunawaambia wawe wabunifu, tayari wameshabuni mtandao kama huu ambao wanataka Wajerumani kuja kufanya, najiuliza ama kwa kuwa Wajerumani ni weupe? Au wana nywele za kuteleza ndiyo sababu tunawathamini na tunashindwa kuthamini matunda yetu wenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijana ambao wanaweza kufanya kazi hii *GTBI*, wamefanya kazi hii katika Manispaa ya Wilaya ya Temeke na Manispaa nyingine hapa nchini na wameweza ku-*perform* vizuri tu. Kabla ya kufunga vifaa vyao, Halmashauri ya Temeke kodi ya huduma walikuwa wanakusanya mwaka 2006/2007 shilingi bilioni 2.9, mwezi Mei 2012 wanakusanya shilingi bilioni 7.5 vijana hawa wa

Kitanzania wamefanya kazi hiyo. Kodi ya nyumba za kulala wageni mwezi Julai 2012 walikuwa wanakusanya Halmashauri ya Temeke shilingi bilioni saba lakini leo hii Mei wanakusanya shilingi bilioni 26 kutokana na vijana hawahawa wa Kitanzania. Ushuru wa mabango, kabla ya kufunga mtambo huu mwaka 2006/2007 wakuliwa wanakusanya shilingi milioni 121, mwezi Mei 2012 wanakusanya shilingi milioni 700, kuna sababu gani ya kuwaleta Wajerumani wakaja kufanya kazi hii ambayo Watanzania wanaiweza? Vijana wa Kitanzania wanasoma kwa pesa za Watanzania, walipa kodi wanyonge, maskini, hivi kweli tuna nia ya dhati ya kuwaondoa vijana wetu walipo? Hivi kweli tuna nia ya dhati ya kuwaendeleza vijana hawa ili waweze kufanya kazi Tanzania na nje ya Tanzania? Au TAMISEMI hawalijui hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba waweze kuongea na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ili waweze kuwaambia vijana hawa wako wapi, wanafanya kazi gani au waende *DIT* kuwauliza vijana hawa wanapatikana wapi na wameshatuma maombi Halmashauri nyingi sana lakini Halmashauri hizo wanawapuuza vijana hawa kwa sababu ukusanyaji wa kodi za Halmashauri zinavuja, zinaliwa na wana uhakika ukifungwa mtambo huu hawataweza kuiba na wala hawataweza kuvujisha mapato. Kuna baadhi ya Halmashauri kibao wamekwenda Temeke kujifunza lakini hawakubali kufunga mtambo huu, tujiulize ni kwa nini hawakubali? Hawakubali kwa sababu unawabana na mapato yatapatikana. Haiwezekani Mtanzania akufungie mtambo utoke kwenye mapato ya shilingi 121 milioni na ufike shilingi milioni 700 leo hii umkatae,

kuna nini? Tunaomba TAMISEMI watakapokuja watuambie kuna nini ama hawawatambui ama wanawatambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Halmashauri ya Morogoro wamefungiwa mtambo lakini wameuharibu makusudi. Wameuharibu makusudi na ndiyo maana mnakaa, mnalia kwamba Halmashauri hazikusanyi mapato, zitakusanyaje wakati wanakusanyia ndani ya mifuko yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali kwa Watanzania hawa ambao wanaweza kufanya kazi hii wapewe nafasi na waiendeleze Tanzania nzima. Nashauri wapewe mara moja kazi hii na wala hatuhitaji Wajerumani waje watufanyie kazi ambayo vijana wetu wanaweza wakafanya na sisi tunaweza tukaenda kuwafanyia Wajerumani siyo wao kila siku wawe wanakuja kutufanyia mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende Serikali za Mitaa. Unapoongelea Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, moja kwa moja unamgusa Mwenyekiti wa Mtaa na Mwenyekiti wa Kijiji lakini watu hawa katika Tanzania hii wamesahaulika kabisa. Wenyeviti wa Mitaa ndiyo wana kazi kubwa kuliko kazi nyingine ya mtu yeyote yaani kuliko Diwani wala sisi Wabunge, hawa ndiyo wenye watu, wanaishi na watu na wapo karibu na watu lakini posho anayopewa Mwenyekiti wa Mtaa ni shilingi 20,000/= kwa mwezi na inalimbikizwa miezi mitano au sita na akija kulipwa anapewa miezi miwili. Hivi kweli sisi Wabunge tukipewa hiyo shilingi 20,000/= tutakubali? Watendaji wa Serikali

wakipewa shilingi 20,000/= kwa mwezi watakubali na mambo yote Mwenyekiti wa Mtaa anafanya, nenda kahamasishe sensa, nenda katuletee Kamati ya UKIMWI na ndiyo pale inapopelekea Wenyeviti wa Mitaa wanachukua rushwa ndogondogo kukidhi mambo yao na kuweza kuuza maeneo bila mpangilio, jana tumeambiwa wanauza maeneo kwa chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitowatendea haki kama sitagusa uvuvi Kanda ya Ziwa pamoja na taarifa ya Mheshimiwa Waziri na atakavyosaidia lakini tunapoongelea uvuvi Kanda ya Ziwa, wavuvi wamebakia wakinyanyasika...*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Nashukuru, nitasubiri Wizara ya Uvuvi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mkiwa, Mbunge kutoka Mwanza lakini mwashiria wa Muungano ukiwakilisha Pemba. Hongera sana kwa mjadala wako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na nilisema mchangiaji wetu anayefuata atakuwa ni Mheshimiwa Lucy Owenya atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa kuwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inamgusa mwananchi wa kijijini kabisa lakini

pamoja na hotuba yake nzuri, ni matumaini yangu atachukua yote yale mema na mazuri aliyozungumza Mheshimiwa wa Kambi ya Upinzani ili waweze kuyafanyia kazi na watayajumlisha kwa pamoja na ninajua yataleta maendeleo kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu na wafanyabiashara wadogowadogo yaani akina mama na vijana ambao tunawaita ni Machinga. Katika Majiji, Manispaa na Miji pamekuwepo na Wanamgambo na wafanyabiashara hawa wamekuwa wakifanya biashara na wamekuwa wakinyanyaswa sana na hawa Wanamgambo. Mimi sisemi kwamba wavunje sheria bali sheria na kanuni zipo lakini inaonekana kwamba wafanyabiashara hawa hawajaelimishwa wala hawajapewa vipeperushi ni jinsi gani ya kufanya biashara zile na pia Serikali haijatenga maeneo maalum ya wafanyabiashara hawa kufanya biashara. Ni vizuri Serikali ikafanya utafiti ikaangalia ni sehemu zipi nzuri za wafanyabiashara hao kufanya biashara isije ikawa kama *Machinga Complex.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hawa Wanamgambo wamekuwa wakiwapiga akina mama, wakichukua bidhaa zao na imekuwa ni jambo la kawaida nafikiri ni kamtindo ambacho wanaiga kama Msemaji wa Kambi ya Upinzani alivyosema kwamba Askari Polisi wamekuwa wakiwapiga na kuwanyanyasa wananchi na hao Wanamgambo wanaona kama ni jambo la kawaida. Ni vizuri Serikali ikachukua hatua na ikawafundisha kwamba mtu akivunja Sheria, Katiba wachukue mkondo wa sheria na si kuwapiga na

kuwanyanyasa hata kuwaibia wafanyabiashara wadogowadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya angalizo hilo, naomba sasa niongelee hali ya ukame ambao inaukumba Mkoa wa Kilimanjaro. Ni jambo lililo wazi kwamba hali ya uoto wa asili katika Mlima wetu pamoja na barafu katika Mlima Kilimanjaro inayeyuka na hii inaonyesha ni udhaifu uliopo kwa Watendaji wa Serikali ambao wameruhusu miti kukatwa hovyo na watu kulima kandokando ya mito na kadhalika. Hapa kipekee naomba nimshukuru Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa jitihada zake za kuhakikisha kwamba miti inapandwa katika Mlima Kilimanjaro lakini mimi naomba sheria zifuatwe na sheria ihamasishe watu kutokulima kandokando ya mito na elimu zitolewe zaidi kwa watu kupanda miti zaidi ili ukame huu uweze kuondoka kwa sababu kwa sasa hivi imejidhihirisha wazi kwamba kuna matatizo, kama mwaka jana mvua za vuli hatukupata na mwaka huu mvua za masika hazikutosha na mahindi yamekauka. Kwa hiyo, naitahadharisha Serikali ijiandae kwamba Mkoa wa Kilimanjaro kuna njaa inakuja, wajiandae kutuletea chakula katika Mkoa wetu kwa sababu mvua za vuli hakuna kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, bali ukame huu umepelekea hata maji ya kawaida safi na salama hakuna katika Mkoa wetu. Mfano mara nyingi tumekuwa tukiongea, Kata ya Mbokomu Moshi Vijijini, wanawake wanatoka zaidi ya kilomita 10 kuja mpaka Mjini kutafuta maji. Jimbo la Mheshimiwa Mrema, Marangu Kaskazini hakuna maji, ukija Mabogini, Jimbo

la Moshi Vijijini, *TPC* hakuna maji na wanawake wanatoka sehemu za mbali kuja kutafuta maji. Lakini katika vitabu vya maendeleo, Mkoa wa Kilimanjaro nimeona wametenga shilingi milioni mbili na shilingi milioni 26 kwa ajili ya *rural water supply and sanitation,* sasa najiuliza hivi fedha hizi zitatosha kweli kwa Mkoa wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, katika Jimbo la Hai, kijiji cha Mtakuja kuna tatizo kubwa la maji, wakaazi wa pale kuna maji wanayokunywa nafikiri yana *chlorine* nyingi sana lakini Serikali haijafanya utafiti lakini maji yale yanawafanya wananchi wale wakinywa maji yale wanakuwa vilema. Mheshimiwa Mbunge wa Siha amekuwa akilisemea suala hili kwenye Halmashauri lakini naona Serikali bado haijafanya utafiti wa kutosha na wananchi wale wanakuwa vilema na Serikali iliyopo madarakani haionyeshi juhudi za kuwasaidia wapiga kura wale ambao Kata hiyo Diwani wake ni wa CCM lakini bado hamuwaangalii watu wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo, sasa hivi wananchi wengi wamekuwa na elimu wamekuwa wakinunua maji ya kunywa ya chupa lakini maji haya yana kodi kubwa sana. Hivyo naiomba Serikali itoe kodi katika maji ya kunywa na hii itaisaidia Serikali kwa upande mwingine kwa sababu watu wakinywa maji safi na salama, magonjwa ya kuhara kama vile kipindupindu na *typhoid* hayatakuwepo na itaipunguzia Serikali mzigo wa kununua dawa kwa ajili ya wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wetu, hospitali tunayoitegemea ya Mkoa ni ya Mawenzi. Kama mlivyoelezwa kwamba hakuna *theatre* na mtu akiumia kidogo inabidi aende kwenye Hospitali ya Rufaa lakini Moshi kuna Hospitali Teule ya *St. Joseph.* Kwa kipekee naomba nimshukuru na nimpongeze Sista Lyimo kwa juhudi anazozifanya lakini pale *St. Joseph* amejenga wodi na nimeshazungumza mara nyingi na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba katika hospitali ya St. Joseph wanahitaji vitanda 50 pamoja na mashuka. Kwa hiyo, ni tegemeo langu kwa sasa hivi Waziri Mkuu anaweza kuielekeza Wizara ya Afya ili waweze kupeleka vitanda katika Hospitali Teule ya *St. Joseph* kwa sababu kwa namna moja au nyingine inasaidia kwa kiasi kikubwa wananchi wa Moshi *especially* akina mama na wale wanaoumia vidonda vidogovidogo wanaohitaji kushonwa na kadhalika wanaweza wakahudumiwa katika hospitali ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie suala la elimu. Pamoja na jitihada za Serikali na wananchi kujenga shule na kuhakikisha kwamba elimu inaboreka lakini mpaka sasa hvi tumeshuhudia wanafunzi wengi wanamaliza darasa la saba na hawajui kuandika wala kusoma. Elimu hii, mfano watoto wa darasa la kwanza mpaka la tatu wengi ni wadogo sana, wengi wao wana miaka sita mpaka nane lakini kwa harakaharaka, naomba niyataje masomo ambayo wanasoma watoto wa darasa la kwanza mpaka la tatu, wana masomo kumi na tano. Kuna Hisabati, Kiswahili ambacho wanasoma na kuandika, kuna *English, Science*, Historia, Jiografia, Ujasiriamali, Uraia, Stadi za Kazi, Michezo, Dini na sasa

hivi wameongezewa TEHAMA. Wote tunajua miundombinu ya shule zetu, sasa hii TEHAMA wataifanyaje? Shule nyingine hazina madawati, hazina umeme, hakuna Walimu wa kutosha na masomo haya ni mengi sana kwa watoto wadogo. Mimi nashauri kwamba darasa la kwanza mpaka la tatu turudishe KKK yaani Kusoma, Kuandika na Kuhesabu na mtihani wa darasa la nne urudishwe sasa wakianza kusoma darasa la nne mpaka la saba wafanye masomo yote na hii itawasaidia ku-*pass* ili wakiendelea kidato cha kwanza tutakuta wanafunzi wetu wameelewa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaomba Walimu pia warudishiwe posho ya kufundisha na watakuwa na motisha. Pia Serikali irejee ile *report* ya Tume ya Mheshimiwa Makwetta jinsi ya kuboresha elimu na kuongeza posho za Ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa harakaharaka, naomba niongelee kidogo barabara za mji wa Dar es Salaam. Kwanza niipongeze Serikali kwa kupanua barabara kuanzia Mwenge mpaka Bagamoyo. Hili ni jambo zuri kwa kiasi kikubwa nategemea inaweza ikapunguza msongamano. Lakini kuna ile mitaro ambayo imejengwa kandokando ya barabara kuu ambayo inatoka Mwenge mpaka ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru lakini nitaunga mkono hoja wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu atakaponieleza kama atawapa vitanda Hospitali ya *St. Joseph*.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge nilisema baada ya Lucy Owenya nitamwita Mheshimiwa Riziki atafuatiwa na Mheshimiwa Mtanda.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa mimi kupata nafasi hii. Pili, nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia kupata afya njema na mimi kuweza kupata nafasi ya kuchangia katika hoja iliyokuwa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaiunga mkono hoja mpaka nipate ufafanuzi utakaoniridhisha kwa hoja zangu ambazo nitazitoa na mimi nitaweza kuunga mkono hoja baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Lindi na Mtwara ni kichaka cha Wapinzani kuja kutuchamba na kutudhalilisha kuonekana maskini na duni, hizi ni njama makusudi ziliandaliwa ili ionekane Mikoa maskini na duni halafu wao wazunguke tena kuja kutuchamba Mikoa ya Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia nidhamu mbovu na matumizi mabaya katika Halmashauri zetu. Nilikwenda kukagua katika Halmashauri ya Kilosa na bahati nzuri Mwenyekiti wangu Augustino L. Mrema alilizungumza na mwaka 2010 nilizungumza kwamba

wabadhirifu wanaofanya wizi katika Halmashauri, Lindi siyo kijiwe. Leo hii nataka nizungumze njama zinazotengenezwa na mtandao kudhoofisha maendeleo katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda Kilosa tumekuta wizi mkubwa umefanyika. Ndugu Joachim Materu ameiba shilingi 577 na milioni 604 katika kuchukua wafugaji kutoka Ihefu kuwapeleka Kilosa. Akapelekwa Polisi ili apelekwe Mahakamani, lakini njama za makusudi zikafanywa wakampeleka LIndi. Hii ni njama ya makusudi ya mtandao kudhoofisha maendeleo Mikoa ya Lindi ili warudi tena watuone sisi ni watu dhaifu, hatuna mabadiliko lakini ni makusudi yanafanywa. Bwana Materu baada ya kujiona ameingia katika Manispaa na mimi huwa naingia pale kama Diwani amekimbia, ameingia Ofisi ya *RAS*. Namwomba Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Lindi aliangalie hilo kwani Lindi siyo kichaka cha wezi, tunashukuru tumeletewa Mkuu wa Mkoa ambaye yuko makini na nina imani kuwa Mheshimiwa Mwananzila atalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ndugu Eunice Maro alikuwa Mhasibu, ameiba shilingi milioni 262 akaingiza katika akaunti aidha ni ya rafiki yake siwezi kuelewa lakini akaunti namba hiyo ni hii, katika benki ya *NMB,* Namba 206660017 na amefanya wizi mkubwa sana…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge tutaomba ukabidhi hiyo *document*.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakukabidhi tena nataka na kopi ili na wengine wazipate.

Eunice Maro akapelekwa Mkinga, amegundua ile ni Halmashauri mpya, ndiyo kijiwe kipya yaani Komba mpya na mwizi mpya, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umefanyika wizi mkubwa katika Ofisi za Kilimo Kilosa, Ndasikoi ameiba Kilosa amepelekwa Ngorongoro, kijiwe kile. Hii ni njama ya makusudi ya kudhoofisha. Pia Ndugu Macha ameiba, ndiyo, na amepelekwa Nanyumbu...

**MWENYEKITI:** Hebu rudia tena hayo majina!

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Wizi mkubwa uliofanyika Kishapu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge hebu rudia kidogo hayo majina hatujayaelewa vizuri.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Tulia Mwenyekiti. Wizi mkubwa uliofanyika Kishapu wa shilingi bilioni sita (6) amepelekwa Babati na amekimbizwa haraka haraka amepelekwa sehemu nyingine. Huu ni mtandao na unafanywa makusudi kuhakikisha wanadhoofisha maendeleo ya Serikali yasionekane. Wizi ulifanyika Ilala na Kinondoni, Ngowi akapelekwa Kilwa, Shirima akapelekwa Kilwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuweni makini kwa hili, ni mchezo mchafu unafanywa na mtandao ili kufanya maendeleo ya kilimo yasionekane, maandeleo ya *TASAF* yasionekane, maendeleo ya ujenzi yasionekane, lakini matokeo yake wanageuka wanasema mnaona nyie Lindi, ni watu maskini sana, ni watu duni sana, ni usumbufu na fujo ya makusudi. Naomba Serikali iliangalie hili, Lindi siyo kichaka cha wezi, Lindi siyo sehemu ya kuja kutudhalilisha. Tupo pale na heshima zetu, tunajitegemea na si Mkoa ambao una njaa. Lindi hatuombi chakula, lakini hii ni njama ya makusudi ili Kilimo Kwanza kisiende Lindi, maendeleo ya Lindi yasisongee mbele. Hivyo mimi siungi mkono hoja mpaka kwanza Materu anatolewa Lindi, ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasema tena siungi mkono hoja. Page Na. 37, wameamua Mkoa wa Lindi na Mtwara umeme usiende vijijini. Umeandikwa programu kabambe ya kupeleka umeme katika Mikoa 16 katika maendeleo ya vijiji, Lindi na Mtwara hazipo, kulikoni! Gesi inatoka Songosongo, Mnazi Bay, lakini Lindi na Mtwara hazimo. Sitaunga mkono maana udhaifu kama huu ndio unaofanya Wapinzani watuone sisi watu wa Lindi kama hatujiwezi, hatuna mazingira ya maendeleo, kumbe ni juhudi za makusudi na hii inafanywa na Maafisa Mipango ambao wako juu katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Wachaga. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema sitaunga mkono kwa sababu nyingine ya *SAGCOT (Southern Agriculture Corridor of Tanzania),* Mkoa wa Lindi una hekta milioni moja (hkt 1,000,000) ambazo hazijatumika…

## MWONGOZO WA SPIKA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo!

**MWENYEKITI:** Mwongozo!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Dada yangu Lulida nafikiri ameteleza. Lugha za humu ndani za kibaguzi hazitakiwi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hatutumii makabila, dini, katika kuainisha hoja humu ndani. Tulielewa alipokuwa anatoa hoja za majina ya akina Ngowi na Macha kuhusiana na wizi binafsi lakini siyo makabila yao. Kwa hiyo, ningeomba ule Uchaga siyo lugha yetu, Uchaga, udini na ukabila ndani ya Bunge siyo tabia yetu.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi. Mheshimiwa Lulida, naomba uondoe Uchaga. Wewe endelea na hayo majina lakini suala la kabila, Wachaga hilo naomba ulifute kwanza.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitafuta usemi wangu.

**MWENYEKITI:** Sijakusikia.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Nimefuta usemi wa Uchaga lakini nilifanya vile kwa sababu…

**MWENYEKITI:** Aah, Mheshimiwa Lulida futa hilo neno la Uchaga endelea na hayo majina.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa naomba muda wangu uniongezee.

**MWENYEKITI:** Muda wako unalindwa hauna tatizo.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Nimesema kuwa suala la Uchaga halipo lakini nilitaja majina ili angalau ionekane mtandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo ni mtambuka na Mkoa wa Lindi tuna hekta milioni moja (Hkt. 1,000,000) ambazo tunataka kuziendeleza katika kilimo na unapotaja *Southern Agriculture Corridor* unaitaja Lindi Mtwara na Ruvuma, lakini katika maendeleo haya Mikoa ya Lindi na Mtwara haikuwekwa. Inanipa kigugumizi nakubali vipi hoja hii wakati Mikoa ya Lindi na Mtwara ambayo tunahitaji kupata maendeleo ya kilimo haimo? Ili niweze kufurahi na niweze kumuunga mkono Waziri Mkuu, naomba na mimi Waziri Mkuu aniunge mkono kwa kuiingiza kwenye mpango wa *SAGCOT* Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Mkoa wa Lindi ni wa mwisho katika kupata bajeti ndogo. Nimelizungumza suala hili la bajeti ndogo katika miaka yangu sita (6) ambayo nimekuwa katika Bunge hili lakini tatizo nimeligundua kuwa Maafisa Mipango ambao wako Lindi hawajawa mahiri katika kutuletea

marekebisho ya mipango yetu na kuiweka katika mazingira bora. Leo mpaka Mikoa ambayo imegawanywa mara mbili ukiunganisha nguvu wanapata shilingi bilioni 30, Lindi ni Mkoa wa mwisho unapata shilingi bilioni 14. Kwa hili nimeshindwa kuunga mkono. Kwa nini? Barabara za Mkoa wa Lindi huwezi kulinganisha na Mkoa wowote Tanzania hii.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Aah, Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na muda wangu ulichukuliwa.

**MWENYEKITI:** Ulishaongezwa!

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikupongeze wewe binafsi kwa kazi kubwa unayoifanya ya kuliongeza Bunge hili. Nina imani kabisa wananchi wa Litembo, Madaba, wameridhika na uongozi wako na wananchi wa Peramiho kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nikushukuru na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kupata fursa leo ndani ya Bunge hili ili nami niweze kuchangia mjadala wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuteua vijana wenzangu kuwa Wakuu wa Wilaya na mimi nina imani kubwa kabisa juu yao. Niwapongeze Waheshimiwa Wabunge ambao wameteuliwa kuwa Wakuu wa Wilaya, naomba wafanye kazi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Mchinga kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa na operesheni zile nyingine nyingine, kwa hakika hazikufanya kazi stahiki kule katika jimbo la Mchinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pia kwa kusema hata mimi ninasikitika sana kwa sababu huu mtandao huu ndio unaodhoofisha maendeleo ya Mkoa wa Lindi. Leo hatuwezi sisi kushawishika kuwe na ndoa za usiku, mchana tupewe talaka kwa kukubali matakwa yao ya kuwaunga mkono. Miaka yote hiyo walikuwa wapi? Wanakuja leo ambapo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imejizatiti kabisa kutekeleza Ilani yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu ninayo Ilani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Nimesoma ukurasa wa kwanza hadi wa mwisho, neno Lindi limetajwa mara moja lakini ninayo Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, neno Lindi limetajwa mara nane (8) katika ilani hiyo. Hivi anayemtakia mema mwenzie kati ya hawa wawili ni nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara Ndundu – Somanga kilomita sitini (60) sasa hivi tumebakiza kilomita thelathini (30). Barabara ya Mtwara – Masasi kilomita 200, Ilani inasema na tayari kazi hiyo inafanyika. Haya ni mafanikio makubwa. Pia nikumbushe pale Mtwara sasa hivi tuna ofisi ya Msajili wa Ardhi, hatuna shida tena ya kwenda maeneo mengine kusajili ardhi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nikuhakikishie na kulihakikishia Bunge hili na Watanzania wote kwamba sasa dalili ya maendeleo katika Mikoa ya Lindi na Mtwara imeanza kupatikana na tuna hakika Chama chetu cha Mapinduzi kitatuvusha kwenda kule tunakostahiki kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapolia hushiki kichwa cha mwenzio. Sisi watu wa Lindi kilio chetu tutakimaliza wenyewe kwa kushirikiana na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo ya utangulizi, naomba sasa nirudi kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hiyo ilikuwa ni bakshishi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na mambo mengine lakini nimesoma Kitabu cha Maendeleo *(Volume IV),* fedha iliyotengwa kwa ajili ya maendeleo katika Mkoa wa Lindi ni shilingi 14,279,779,000. Maana yake ni kwamba sisi Mkoa wa Lindi ni watu wa mwisho katika

kutengewa fedha za maendeleo katika bajeti ya mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo haiondoi ukweli kwamba, bado tunayo mambo mengi tumefanyiwa. Hata hivyo, katika bajeti ya mwaka huu nasisitiza bajeti hii bado watu wa Mkoa wa Lindi haijatuangalia kwa jicho la karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninukuu Mikoa michache tu; Mkoa wa Mara shilingi bilioni 31, Mkoa wa Kilimanjaro shilingi bilioni 20, Mkoa wa Iringa shilingi bilioni 16, Mkoa wa Dodoma shilingi bilioni 32, sisi na watu wa Rukwa ndiyo wa mwisho lakini sisi ni wa mwisho zaidi kuliko watu wa Rukwa. Hili halieleweki, halikubaliki na tunaomba Serikali sasa ijidhatiti kwenye maendeleo yale ambayo yanaweza kutupeleka mbele zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo, yako baadhi ya mambo mawili, matatu, ninaomba sasa nijielekeze kwayo. Jambo la kwanza ni juu ya suala zima la Viwanda vya Saruji katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Katika mipango mikubwa ambayo Rais wetu ana nia njema ya kutuletea maendeleo na kuwawezesha vijana wa Mikoa ya Mtwara na Lindi, ni kuhakikisha kunajengwa kiwanda kikubwa cha saruji pale Mtwara. Tatizo kubwa ambalo limejitokeza, ni mgogoro wa ardhi baina ya mwekezaji huyu Dangote na mwekezaji Sun Lodge ambaye kwa sasa ninaambiwa amekwenda Mahakamani kuishtaki Serikali eti kwa kuwa tu Serikali kupitia Rais wame-*revoke* ule umiliki wa ardhi. Sasa najiuliza na Waziri wa

Sheria atuambie, hivi ni nani mwenye uwezo wa kumshtaki Rais? Ni Katiba gani hiyo Rais analeta jambo la msingi kwa maendeleo ya watu wake atokee mwekezaji amshtaki? Nadhani hapo lazima tupewe ufafanuzi kwa sababu ninaamini kabisa kama Rais amefanya kwa nia njema basi ni lazima tumuunge mkono ili wananchi wa Mikoa ya Mtwara na Lindi bei ya saruji iweze kuteremka kwani mwekezaji huyo atakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 6000 kwa siku, hivyo bei ya saruji itateremka, vijana watapata ajira. Kwa hivyo, naomba Serikali ilifanyie kazi suala hili na kwa ukaribu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili, pale Lindi tunajenga Kiwanda cha Saruji na nia kubwa ni kupambana na tatizo la ajira kwa vijana, kuwawezesha akinamama na Watanzania wale wa Kusini ambao katika kipindi cha nyuma tulikuwa tunasema wamesahaulika. Sasa kama tumeanza kwa *speed* kubwa ya kuleta maendeleo Mikoa ya Kusini, ni lazima tuhakikishe viwanda vinajengwa pale Lindi ili watu wa Lindi waweze kupata fursa zile ambazo watu wa maeneo mengine wanazipata. Tatizo letu pale ni umeme. Umeme uliopo ni *KV 33* ambao hauwezi ku-*support* ujenzi wa viwanda. Tunachohitaji walau sasa ni Serikali kupitia tamko lake, kupitia Ilani ya kuleta umeme wa gesi kutoka *Mnazi Bay* kuupeleka pale Lindi ili tufikishe *KV 133* ili Kiwanda cha Saruji kiweze kufanya kazi kwa ufasaha na wananchi wa Lindi waweze kupata matunda pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hilo la umeme ni kubwa ingawa naishukuru Mamlaka ya Umeme Vijijini

*(REA)* kwa kukubali kupeleka umeme kwenye vijiji vya Kilangara, Kitomanga, Mipingo, Rutamba, Milola, Kilola Mbwani na Kijiweni. Unaposema Chama changu kinawaacha wananchi wa maeneo haya, una maanisha nini? Changamoto zipo, nasema Serikali ya CCM tupambane nazo kuhakikisha kwamba wananchi wa maeneo haya wananufaika na wananeemeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la gesi. Lazima rasilimali gesi iwanufaishe wananchi ambapo gesi hii inatoka na hili tulishakubaliana. Tuliishakubaliana tozo, nachosisitiza hapa kwa kuwa shilingi trilioni tatu (3) za gesi sasa zinatoka Kaskazini mwa Lindi, tozo hiyo pia iwaguse wananchi wa Mkoa wa Lindi. Hilo halina mjadala kwa sababu ninaamini kabisa Serikali imenisikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tunayo haja kubwa ya kuanzisha Kiwanda cha Gesi pale Lindi. Tukiweka Kiwanda cha Gesi na Wanorway wameshakubali kuonesha ushirikiano, tutawafundisha vijana wetu pale kwa sababu Mheshimiwa Mwenyekiti kwa taarifa yako sasa hivi vijana wengi kutoka Nigeria wameshaingia Mtwara, wanajiandaa kufurahia rasilimali gesi ya Mtwara. Hili haliwezekani! Kuna Waziri, Ofisi ya Rais, Uwezeshaji, wawezesheni sasa wale vijana wa Mtwara na Lindi wajiandae ili waweze kufaidi hii rasilimali gesi! Namwomba sana Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, kwa umahiri na uwezo wake wa kazi, alifanyie kazi, tuwe na Kiwanda cha Gesi ili vijana wetu waweze kupata ajira kwenye kiwanda kile na wasiwe wasindikizaji lakini pia wawezeshwe kulima matunda, mbogamboga, ili waweze ku-*supply* vitu hivi pale

kiwandani. Kwa hiyo, hayo ni baadhi ya mambo ambayo nilisema tuyazungumzie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, tulikubaliana kuhusu Daraja la Mchinga…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nasisitiza daraja la Mchinga kwa sababu niliahidiwa, nashukuru kwa kunipa fursa hii. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nitumie nafasi ya awali kuungana na Mheshimiwa Mtanda, ni kweli unatuwakilisha vizuri. Sisi akinamama wenzio tunajivunia na endelea hivyohivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, nimpongeze Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mgimwa, aliwasilisha vizuri bajeti yake na hasa alitumia taaluma kujibu maswali, alitumia taaluma vizuri kwelikweli. Mungu akubariki sana Baba yangu na tena akuongezee umri. Nimpongeze na Naibu Waziri, Mheshimiwa Saada Mkuya. Mama alijiamini, kwa mara ya kwanza anasimama lakini mlimuona alivyofanya kazi nzuri. Nawapongeza sanasana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sipendi nimuache Waziri Mkuu wangu. Nampongeza sana Kaka yangu. Nina

imani na yeye, kazi zake ninazitambua pamoja na timu yake katika ofisi yake na Wizara ambazo ziko chini yake. Kweli kazi ni nzuri, Mungu awabariki na awatie nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi na mimi naomba nizungumze machache yanayonisibu. Nakuomba sana unisikilize na nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote wanisikilize. Naanza na suala la maombi ya Mkoa wa Singida kuongezewa fedha kwenye ujenzi wa Hospitali ya Rufaa. Katika jambo la kiungwana alilofanya Mkuu wa Mkoa wa Singida, yapo mengi lakini pamoja na hili, Mheshimiwa Dkt. Parseko Kone, amefanya kazi kubwa sana. Ameanzisha ujenzi wa hospitali kwa fedha za kutafuta mwenyewe na bado ametafuta vifaa vya hospitali hiyo vyote vipo. Tunang'ang'ana sana na maombi haya ili vifaa hivyo visije vikaharibika. Mheshimiwa Waziri Mkuu nafahamu uungwana wako, nakuomba usikilize kilio cha Singida. Tuliomba shilingi bilioni 3.8 umetupa shilingi bilioni 1.8 Mheshimiwa Waziri Mkuu tupe shilingi bilioni mbili (2) zingine tumalizie majengo tuliyoanza. Tukimalizia majengo hayo Hospitali hiyo itaanza kufanya kazi sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampigia magoti Mheshimiwa Waziri Mkuu, ombi hili siyo la Diana Chilolo, ni ombi la wananchi wa Mkoa wa Singida chini ya Dkt. Parseko Kone. Unataka tulie vipi Mheshimiwa Waziri Mkuu? Majengo yako pale, tena yalishaanza na ni mazuri kabisa. Ukitupa shilingi bilioni mbili (2), majengo yatakamilika na Hospitali itaanza na vifaa tulivyopewa vitafanya kazi. Siyo vifaa tu, niwaambie Mkuu wa Mkoa

huyu ametafuta mpaka na Madaktari. Kama siyo kuisaidia Serikali ni nini jamani? Madaktari ameshawapata. Jamani wanasema jikaze uinuliwe. Huyu baba kajikaza, Mkoa umejikaza, Mkoa umefanya kazi, tunaomba tukipata shilingi bilioni mbili (2) hospitali hii itafanya kazi na haisaidii watu wa Singida tu, bali Kanda nzima itatibiwa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulituma maombi maalum ya shilingi bilioni 14, yote yametupiliwa mbali. Ndiyo haya ambayo anasema Mheshimiwa Mtanda, Mikoa ya mwisho. Ndiyo, Singida mnasema ni Mkoa wa mwisho kiuchumi, sasa mtatuinua vipi? Mnapoona wenzenu tunajitahidi basi mtuone na hata hayo maombi maalum tunayotuma myasikilize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kabisa, mimi Waziri Mkuu huyu ninamfahamu, ni muungwana mno. Hata na timu yake, wako na akina mama pale ni watu wa huruma, ninaamini watakuwa wamesikia kilio changu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumaliza hilo, nataka nizungumzie kuhusu soko la alizeti Singida. Mimi naendelea kumpongeza Mkuu wa Mkoa kwa kweli anajitahidi sana, yaani anafanya kazi Singida kama vile anafanya Simanjiro, nyumbani kwao. Ameona wananchi wa Mkoa wa Singida hasa wakulima wa alizeti jinsi wanavyodhulumika, wanunuzi wa kati, hawa walanguzi wanafuata alizeti nyumbani kwa wakulima, wananunua shilingi 250/=, shilingi 300/=, lakini baba wa watu akaanzisha Vyama vya Ushirika, amevifufua, tulikuwa hatuna hata kimoja, amevifufua Vyama vya

Ushirika 81 ambavyo tayari ameshaviwekea utaratibu, vinapewa fedha na mabenki. *CRDB, NMB* wako tayari kuvipa Vyama vya Ushirika fedha ili viweze kununua alizeti tena kwa bei ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilianza na shilingi 500/= leo hii nimepiga simu nimeambiwa vinanunua kwa shilingi 700/=, lengo ni kumnusuru mzalishaji, tukimwekea mazingira mazuri mzalishaji, zao hili litalimwa sana na tutaingiza pato la nchi vizuri. Tena amepata mwekezaji kutoka Canada na anakuja kujenga kiwanda pale na anasema atakiachia Vyama vya Ushirika bure, niambie busara hizo zinavyotumika. Leo wanapatikana wenzangu wanunuzi wachache Singida wanapinga kauli hii jamani, kauli ya Mkuu wa Mkoa? Tena Mkuu wa Mkoa wamem-*quote* vibaya tu, hajapinga biashara huria iko pale pale. Alichosema wasiendelee kwenda kununua kinyemela kwa wakulima, wanunuzi wote wakutane gulioni, Vyama vya Ushirika vimefungua masoko hukohuko vijijini, wakutane huko washindane bei. Wanunuzi mmoja mmoja wanaruhusiwa kununua na Vyama vya Ushirika vinaruhusiwa kununua na yule mkulima atakayekosa muda wa kununua anaruhusiwa kuacha pale kwa utaratibu wa stakabadhi ya mazao.

Ndugu zangu ninaomba Wanasingida, mimi ndio mama wa Mkoa Singida mnisikie, ninaongea kwa huruma kabisa, lengo la Mkuu wa Mkoa ni kumnusuru mkulima asiendelee kupunjwa na biashara huria iko palepale. Hata wale akinamama wanaouza alizeti barabarani, wanaruhusiwa waendelee kuuza, hakuna ugomvi hapa na Mkuu wa Mkoa. Tusilumbane na

Mkuu wa Mkoa wetu, tunamvunja moyo. Namaliza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee Mfuko wa UKIMWI. Tulishazungumza suala la kuanzisha Mfuko wa UKIMWI hapa. Nataka nijue kigugumizi kiko wapi? Kwa nini mfuko huu usianzishwe? Jamani lazima tujenge mazingira ya kujiandaa. Siku mhisani akiacha kutusaidia tunakuwa na maandalizi. Tena tuna bahati Tume ya Kudhibiti UKIMWI, Mwenyekiti Mtendaji Dkt. Fatma Mrisho, ni mama muungwana sana, mstaarabu sana, ni mwadilifu na makini, amewafanya mpaka watendaji wa taasisi hiyo wana akili na busara kama zake. Tena huyu mama muongezeeni siku. Mheshimiwa Waziri Mkuu, huyu Daktari mimi nampigia debe, mmuongezee kazi. Kama muda umeisha, mmuongezee miaka mingine, bado akili zake zinafanya kazi na yuko makini kwelikweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi mishahara waongezwe, mishahara iongezeke kwa vile ni midogo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Naanza kwa kuunga mkono hotuba hii na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anayoifanya na

wote ni mashahidi na kweli ni mtoto wa mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianzie alipomalizia Mheshimiwa Diana Chilolo kuhusiana na tatizo la UKIMWI, ni janga kubwa na naipongeza Serikali pamoja na wadau mbalimbali kwa kuweza kuwa kati ya nchi chache duniani ambazo zimepunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa asilimia 25. Hilo naomba tujipongeze, ni juhudi kubwa kabisa ambazo zimefanywa. Kwa kuongezea juhudi hizi kama alivyosema Mheshimiwa Diana Chilolo, napenda kufahamu ni lini mfuko wa UKIMWI utaanzishwa. Mfuko huu umesemwa toka Sera ya UKIMWI ya mwaka 2001. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, Bunge lijalo Muswada wa Sheria uletwe Bungeni hapa tuanzishe Mfuko huu kwa sababu tunaona wafadhili wengi wanaendelea kujitoa na sasa hivi tunajua watoto wengi yatima waliokuwa wanahudumiwa na Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI (*Global Fund*), mradi ule umeisha, watoto hawana huduma. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu hilo liletwe kikao kijacho la sivyo Wabunge tuna haki ya kuleta Muswada wa Sheria hapa Bungeni kama Serikali itachelewa kuuleta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la lishe. Takwimu zinasema watoto 47,500 hapa nchini wa chini ya miaka mitano kila mwaka wanakufa kwa utapiamlo. Utapiamlo unasababisha asilimia 42 ya watoto chini ya miaka mitano (5) kudumaa na wengi wana upungufu wa damu. Tunazungumzia suala la watoto kumaliza darasa la saba hawajui kuandika na kusoma, sababu mojawapo inaweza kuwa

inachangiwa na lishe duni na utapiamlo mkali ambao watoto hawa wanakabiliwa nao. Tuwekeze kwa watoto kwa sababu ndio Taifa la kesho. Sisi hapa tumo humu ndani kwa sababu tumelishwa vizuri tukawa na akili. Kama una lishe duni huwezi ku-*concentrate* na masomo. Tusizungumzie tu upungufu wa Walimu, madarasa lakini tuzungumzie tatizo kubwa linalotukabili na mimi naipongeza Serikali ya Chama changu, Chama cha Mapinduzi kwa kuliona hili na kuweka mkakati wa kupambana na utapiamlo na kuhakikisha kunakuwa na uhakika wa chakula nchini hapa kwa kila kaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo. Kilimo ni uti wa mgongo na hilo linaendana na uhakika wa chakula nyumbani. Nchi hii inahitaji kujitosheleza kwa chakula na Mkoa wangu wa Iringa ni Mkoa mmojawapo ambao unazalisha chakula kwa wingi lakini mara nyingi tunakabiliwa na upungufu wa masoko. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba uiwezeshe Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko iweze kununua mazao ya wakulima na pia kuweza kutumia kinu kilichoko katika Mkoa wa Iringa ili kiweze kusagisha na kupunguza mfumuko wa bei ya chakula. Kama kitatumia kinu kile, nina uhakika wananchi wa Mkoa wa Iringa wataweza kuuza mahindi yao kwenye Bodi ya Nafaka na baadaye pia tutahakikisha kwamba unga unasagwa na kupunguza mfumuko wa bei ya chakula ambao huko mpaka kwenye mikoa inayozalisha kwa wingi. Iweje Mikoa inazalisha mahindi kwa wingi lakini bado inakumbwa na mfumko wa bei ya chakula sokoni? Hilo ni jambo la muhimu sana, naomba uliangalie na na-*declare interest* kwamba

mimi ni mjumbe wa Bodi ya Nafaka wakati ninapoipigia debe hapa. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu utupe shilingi bilioni saba (7) tuanze kusagisha mwaka huu mahindi ili tuweze kuhakikisha kwamba tuna uhakika wa chakula na mfumuko wa bei unapunguzwa na kuhakikisha kwamba walanguzi wanaacha kununua mahindi yetu kwa bei ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo hapohapo, nashukuru kwamba Serikali imesema wataalamu wa kilimo vijijini wawe ni mfano wa kuigwa kwa kuwa na mashamba ya kilimo, mashamba ya mfano lakini naomba wapewe pembejeo. Hivi tunavyosema walime tumewaandaaje, wapewe pembejeo zote zinazowawezesha kulima kwa mfano maana yake hawawezi kulima kwa fedha zao za mfukoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu. Naungana na wenzangu wanaosema fedha zile zilizorudishwa, zile za Rada, ziende kwenye ujenzi wa madarasa, nyumba za Walimu pamoja na hosteli kwa watoto wa kike kama unataka kupata elimu bora. Hosteli zitasaidia lakini na madarasa yatakuwa ni ya kudumu, vitabu vitachanika, vitaisha, Serikali inaweza kutafuta fedha ikanunua vitabu, lakini yale majengo yatakuwepo ya kudumu kizazi na kizazi kitajua ile fedha iliyoletwa ilijenga madarasa, ilijenga nyumba za Walimu, Walimu wetu wataweza kuwa na uwezo wa kukaa vijijini na watafundisha vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hilo, naiomba Serikali iangalie vizuri pia mitaala. Hivi

inakuwaje mtoto anayesoma kijijini hasa yule wa Sekondari analinganishwa kwenye maksi za kushinda na mtoto aliyesoma mjini? Tuweke asilimia, wale wanaosoma mjini ambao wana uhakika wa kila kitu wapewe asilimia kubwa ya *pass mark*, wale wanaosoma vijijini na mimi nimesoma kijijini, wale wanaosoma vijijini wapewe maksi za chini, hawana taa, tuangalie wale wanasoma gizani. Nyumbani kwa mama, bibi mzee hana hata kibatari halafu siku ya mtihani wote tunawashindanisha sawa, sio haki, tuangalie hivyo vigezo viwekwe.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua hiyo ni kengele yangu ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kabisa Serikali kwa kuangalia suala la utalii, lakini napenda Bodi ya Utalii iwezeshwe kwa kupewa rasilimali ili iweze kutangaza vizuri vivutio vya Tanzania. Mkoa wa Iringa ni Mkoa ambao ndio wenye Mbuga ya Taifa kubwa hapa Barani Afrika, Mbuga ya Ruaha *(Ruaha National Park).* Tunaomba barabara ya lami iharakishwe kujengwa kutoka Iringa Mjini mpaka Ruaha *National Park* ili tuwavutie watalii wengi. Naomba Kiwanja cha Ndege cha Nduli kijengwe ili tuweze kupata watalii na sisi tufaidike na matunda ya utalii kama inavyofaidika Mikoa mingine au sehemu nyingine. Hii pia inaendana na vivutio tulivyonavyo, vivutio vya Isimila ni mambo ya kale, ni ya utalii ambayo yanaweza kuvutia watalii wengi na pale mjini kuna vivutio vingi vya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala zima la Benki ya Wanawake. Benki ya Wanawake iliundwa kupitia Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) ili iwakomboe wanawake vijijini. Naomba hii benki, hizi fedha zisiishie Dar es Salaam peke yake, ziwahusishe pia na wanawake wa vijijini wakiwemo wanawake wa Mkoa wa Iringa na kama Benki hii ina tawi moja basi kuwe na madirisha ya wanawake katika benki za *NMB* na *NBC, CRDB* ambako fedha zile zitapitishwa, wanawake wengi wa vijijini waweze kufikiwa ambao ndio wakulima wakubwa wa mazao ya chakula. Tunapenda na sisi tufaidike na hizo fedha tujue kwamba hii benki ni mkombozi wa wanawake wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kumpongeza Rais wangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika uteuzi ambao amefanya kwa kuwateua wanawake wengi kuwa viongozi, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Mawaziri na sisi tunamhakikishia hatutawaangusha wanawake, watafanya kazi na mnawaona humu wanavyofanya kazi kama jeshi la mwamvuli akiwemo Mkuu wa Mkoa wangu wa Iringa, mkoa ambao una viongozi wengi wanawake na umeonyesha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Naunga mkono hoja, ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mwongozo, Mheshimiwa Lwanji!

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (7).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, isome!

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Kanuni ya 68(7) inasema:-

*"Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye kadri atakavyoona inafaa"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali wakati Mheshimiwa Riziki Lulida akichangia alitakiwa na *Chief Whip* kufuta neno "Wachaga" lakini kabla hajamweleza hivyo, naona kama alikiuka Kanuni ya 64(f) ambayo inasema:-

*"...hatamsema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwingine yoyote".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa inasema hatamsema vibaya au kifungu kinachofuata kinachosema:-

*"...hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lilitumika neno kwamba "Mheshimiwa Mbunge anazeeka vibaya". Sasa ili kuweka rekodi sawa, sidhani kama Mheshimiwa anazeeka vibaya kwa sababu alikuwa anachangia na kwa kweli kipindi hiki ni *very sensitive* kwa sababu watu hapa tunagawana kilicho kidogo, kwa hiyo *tempers* zinaweza ku-*flay* hapa. Sasa sioni uhusiano wowote wa Mheshimiwa kuzeeka vibaya na neno Wachaga. Naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, kwa mujibu wa Kanuni uko sahihi na umeomba mwongozo, lakini pia Kanuni zinatukataza kurudiarudia. Sasa katika suala la mwongozo ambalo lilikwishatolewa na Waziri wa Nchi, kuhusu matamshi ya Mheshimiwa Riziki Lulida kufuta kauli ya kulitaja kabila la Wachaga, akiunganisha na maelezo yake, hilo lilishatolewa mwongozo na lilishafutwa. Kwa hiyo, wewe pia unavunja Kanuni kwa kulirudiarudia neno hilo. *(Makofi/Kicheko)*

Katika lile la pili ambalo umeliibua upya, mimi kama Kiti sikumbuki kusikia neno hilo likisemwa lakini haitufungi, sijui kama alikuwa anamwambia Mbunge gani mjinga kwa sababu sikuona kama akielekeza mashambulizi kwa Mbunge yeyote. Hata hivyo, nafikiri kwa mwongozo wangu nitumie nafasi hii kuwaomba

Makatibu wakapitie *Hansard* na kuona mazingira ya neno hilo kama yalikuwepo, kama hayakuwepo basi Kiti kitatoa mwongozo kulingana na neno hilo lakini kama itakuwa mazingira hayo hayakuwepo na sisi tutakuomba kwa mujibu wa Kanuni na wewe ufute kauli yako kwa sababu itakuwa ni kauli ambayo haikutolewa ndani ya Bunge hili.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndio mwongozo wangu ninaomba sasa...

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niweke sawa rekodi yangu kwamba nilisema dada yangu Lulida ameteleza. Ndivyo nilivyosema, siwezi kusema amezeeka au kitu gani. Nilisema tu kwamba lugha ya kutumia ukabila na udini ndani ya Bunge hairuhusiwi. Naweza kuvumilia kutamka majina ya Macha au nini kwa sababu wamefanya makosa kwa majina yao lakini sio kwa ukabila wao. Ndio nilichosema. Kwa hiyo, nafikiri katafuteni *Hansard* halafu mtathibitisha haya maneno yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nafikiri nimelifafanua vizuri. Nimeeleza hapa kama Kiti sikusikia neno hilo na ndio maana nimetoa mwongozo hapa

*Hansard* itaenda kutafutwa na kama itagundulika neno hilo halikusemwa, Mheshimiwa Lwanji atawajibika na yeye kufuta hiyo kauli yake humuhumu ndani ya Bunge lakini kama neno hilo litakuwa limesemwa, Mheshimiwa Lwanji ataendelea na maamuzi ya Kiti na wewe umeshaomba mwongozo ndio nimetoa mwongozo hivyo. Kwa hiyo, hututakiwi kuendelea kubishana na mwongozo wa Kiti changu tena.

Waheshimiwa Wabunge kwa hiyo muda wa kuhitimisha shughuli za Bunge umefika, Mheshimiwa Lwanji nimekwishakujibu, Wabunge waliotakiwa kuchangia kwa asubuhi ya leo wameshachangia na naomba tu labda kwa maandalizi ya Waheshimiwa Wabunge watakaochangia mchana niweze kuwataja ili waweze kujiandaa. Wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis atafuatiwa na Mheshimiwa Vicent Nyerere, Mheshimiwa David Homeli Mwakyusa na wengine wataendelea kufuata.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tu niwape taarifa kwamba hii orodha kama ilivyo lakini kiongozi anayekaa hapa Mezani anatakiwa kuzingatia yale niliyoyasema jana. Atazingatia uwiano wa Kambi ya Upinzani na Kambi ya Chama Tawala, atazingatia pia ndani ya Upinzani Vyama vilivyoko ndani ya Kambi ya Upinzani, atazingatia Muungano Bara na Visiwani, atazingatia pia jinsia. Sasa nimekuwa nikipata hapa vi-*note* vinakaribia hata kufika mia moja, kila mtu ananiambia ana udhuru, kila mtu ananiambia achangie sasa, kila mtu ananiambia kwa nini mimi huniiti. Kwa hiyo, naomba jamani mtusaidie tu kutupa ushirikiano kwenye Kiti, watu wote walioomba

kuchangia watapata nafasi, lakini tutazingatia hayo niliyoyasema na sasa nasitisha shughuli hizi za Bunge mpaka 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Sylvesta M. Mabumba) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Naomba niwataje ambao wataanza sasa hivi kuchangia. Tutaanza na Mheshimiwa Vicent Nyerere, atafuatiwa na Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis na Mheshimiwa David Mwakusya ajiandae. Mheshimiwa Vicent Nyerere.

**MHE. VICENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote na Manaibu Waziri walioteuliwa. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake. Mwanzoni nilidhani Mheshimiwa Waziri Mkuu sio msikivu, lakini ni msikivu sana kwa sababu amechukua hoja zetu za mwaka jana na amezifanyia kazi mwaka huu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameomba Shilingi trilioni 3.116 kwa ajili ya Wizara yake, ni fedha nyingi sana kama zitatumika vizuri. Lakini kama zitatumika kwa mtindo ambao unatumika sasa hivi, hata *impact* yake haitaonekana. Nidhamu ya wafanyakazi wa Serikali hasa wanaotumia fedha hizi,

Sekretarieti za Mikoa na viongozi wengine wa Serikali bado ni mbaya sana. Mfano mdogo ni Mkoa wa Kagera. Mimi niko kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali.

Mkoa wa Kagera tumekwenda kukagua hesabu za Serikali tukakuta kuna wodi ya wagonjwa ambayo iko tayari, haitumiki zaidi ya mwaka mzima. Inahitaji Shilingi milioni 128 peke yake kwa ajili ya kununua vitanda, magodoro na vifaa tiba. Lakini viongozi wa Mkoa ukaamua kujenga ofisi mpya ya Mkoa yenye thamani zaidi ya Shilingi bilioni 10. Bilioni moja tayari imeshatumika kwenye msingi. Sasa nashindwa kuelewa, hivi vipaumbele vya wananchi huwa ni vipi? Nilidhani watu wa Kagera walikuwa wanahitaji zaidi wodi ya wagonjwa kuliko Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ipo, *okay,* ni ya zamani. Lakini bado inaweza ikarekebishika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba sana fedha hizi kama utaweza kuwabana watu wako, bahati nzuri Wakuu wa Mkoa wako hapa, utaweza kuwabana wakazitumia kwa nidhamu *impact,* itaonekana. Lakini kama ni hivi wanavyofanya, hakuna chochote kitachooneka. Kila mwaka tutapitisha fedha nyingi na hakuna kinachofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana pia lile wazo letu kuhusu magari. Umetoa mwongozo mzuri sana kwamba magari ya Serikali yatumike wapi, yenye CC kiasi gani. Lakini tutaona utukufu wako kama hata haya yaliyopo yakauzwa ili tukanunua haya ambayo unayahitaji. Lakini hii kusema tu mwaka huu mwaka

kesho utasema bado watanunua, mimi nadhani haya yangeuzwa halafu tukanunua mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukiangalia aya 46 ukurasa wa 29 ameongelea kuhusu viwanda, naomba kunukuu. Inasema: "Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mchango na umuhimu wa sekta ya viwanda katika kuleta maendeleo endelevu kuongeza ajira na kuongeza thamani ya mazao." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ni njema sana, lakini wawekezaji wa viwanda hawako kwa ajili ya kuongeza ajira. Leo asubuhi kwenye Kauli ya Waziri kuhusu viwanda vya samaki na bei ya samaki, nimesikitika sana kauli hizi za Mawaziri, ni vizuri wakati mwingine waje kutuuliza sisi ambao tuko *field* huko. Namshukuru mama yangu Mheshimiwa Kabaka, tumekuwa tukifuatilia suala hili kwa muda mrefu kidogo. Majibu tunayoyajua sisi na hiki kilichoandikwa hapa ni tofauti. Hii *address* ya Umoja wa Wauza Samaki Ulaya na maendeo mengine. Lakini wenye shida ni wavuvi wa visiwani. Wenye viwanda vya samaki ambao wako Tanzania, wana viwanda vingine Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya wafanyakazi wa viwanda wamepewa mikataba ya ajira ya kudumu, kwa hiyo, lazima wafanye kazi. Sisi kwetu wanafanywa kama vibarua. Bei ya samaki wanaamua wao wenyewe kuifanya iwe chini kwa upande wa Tanzania ili wavuvi wetu wakauze Kenya ili viwanda vile vifanye kazi. Tunaua ajira. Waziri wa Kazi na Ajira ni shahidi na ameshakuja kwangu Musoma na bahati nzuri ametoka

kule kule. Hawataki kutoa mikataba ya ajira kwa wafanyakazi kwa viwanda vya samaki. Lakini Kenya wamelazimishwa, wametoa na wanafanya kazi hii vizuri na ni hao hao wenye viwanda kule na huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri anatuambia kwamba ameongea na Balozi wa Ubelgiji. Hivi Balozi anakwenda sokoni kununua samaki, Usalama wa Taifa wapo wanaangalia, ni Antanovu ngapi zinaruka kutoka Jomo Kenyatta *International Airport* kwenda *Tel Aviv* kupeleka samaki wanaotoka Tanzania na wanapitia Kenya? Nenda kaulize kampuni ya *MAISC, frozen fish* zinakwenda ngapi Ulaya? Hapa tunapewa majibu mepesi kwamba bei imeshuka kwa sababu wananunua nguruwe na kuku, sio kweli. Mimi nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri tukitoka hapa asione aibu. Mimi ni mpinzani, lakini kwa ajili ya kuisaidia nchi hii. Aje tumwonyeshe namna gani wengine wanafanya kazi hii.

Leo nimepata simu nyingi sana kutoka Visiwani. Hawa hawa wenye viwanda upande wa Kenya wako tayari kununua samaki kwenye visiwa vya Ziwa Viktoria. Visiwa vya Kwelu, Malelema, Gosba, Siza na Kwa Juma, kwa Sh. 5,500/= bei ya Kisiwani na wanapeleka kwenye viwanda vya Kenya. Wao wanauza soko lipi?

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninapenda tu na kwa kuwa hawa wako chini yako wasituogope, wawe wanakuja kwetu, tuwaelekeze namna gani kwa sababu tumekwishajitayarisha mwaka 2015 namna ya

kuendesha nchi hii. Tutawasaidia kwa kipindi hiki kilichobaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa wenye viwanda sio marafiki zetu kama mnavyofikiria. Ni vizuri kuwekeza kwetu, lakini tuangalie vijana wetu. Sasa hivi ukisimamisha ajira za uvuvi wa samaki kama migomo itaendelea na madereva wa magari ya samaki, wavuvi visiwani, wauzaji wa mafuta na wafanyakazi wa viwandani, ajira zinakwenda kupotea nyingi sana. Sijui Mheshimiwa Kabaka amejipangaje katika hili. Hawa wote wakirudi mjini hapatakalika, wanakwenda kuwa wahalifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu ameongea vizuri sana kuhusu bandari, katika hotuba yake aya ya 65 ukurasa wa 21. Nia ni nzuri sana lakini kuna hawa wenzetu waliopewa dhamana hii kuisaidia bandari waliofungua *ICD*. Hawa ni tatizo. Wamekuwa na *hidden charges* nyingi kwa sababu unapoleta kontena pale huwa kuna gharama kulitafuta kontena kama limechanganywa na unataka kulitoa. Lakini iwe unatafuta kontena au haulitafuti, ile gharama ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunavyoongea, kuna tani nyingi sana, bandari ziko kwenye *ICD* kwa sababu ya urasimu. Tuliwaomba wafanye kazi masaa 24 kwa siku saba, wanafanya siku tano. Wale ambao ni Waislamu wenzetu wakiingia Msikitini hawafungui, Jumamosi wanafanya nusu siku, Jumapili hawafungui kabisa. Siku hizi zote wanazi-*charge* kama umechelewa kuchukua mzigo wako. Sasa mwagizaji wa mizigo anachokifanya, gharama anayowekewa na *ICD*

anakwenda kuweka kwa mlaji wa mwisho na tumekuwa na *regulatory authorities* nyingi hazifanyi kazi zake. *Overall SUMATRA* wamebaki wanakimbizana na madaladala, wanaacha *charges* nyingi za *ICD* zinaongezwa kwa wateja, na zinakwenda moja kwa moja kwa walaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis na Mheshimiwa David Mwakyusa ajiandae.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie katika hotuba ya Waziri Mkuu. Napenda kugusa mambo mawili au matatu kutokana na muda na pia napenda kusisitiza kwa Waziri Mkuu kwamba mambo ambayo nayasema, tayari niliyasema, lakini mpaka sasa tunaona kwamba yana madhara na yanasababisha fujo kwa upande wa Zanzibar, lakini hayajafanyiwa kazi. Kwa hiyo, kabla ya kuendelea, ningependa kuyatilia msisitizo kwamba yanahitaji yafanyiwe kazi kama inavyotakiwa na vile ambavyo tunaongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Muungano. Kama utakumbuka katika Bunge lako la Tisa aliyekuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini alileta kumbukumbu za *Hansard* ndani ya Bunge na kusema kwamba baada ya kuwa na minong'ono mingi ambayo ilikuwa huko nje inaendelea kwamba suala la mafuta na gesi ni suala lililoingizwa kinyemela katika masuala ya

Muungano na *documents* ya mambo ambayo ni ya Muungano ya mwanzo yaliyokuwepo, suala la mafuta halikuwa suala la Muungano. Katika kumbukumbu hizo, aliyekuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini pia alizungumzia kwamba suala hili liliingizwa katika Muungano, limejadiliwa ndani ya Bunge lako Tukufu, Wabunge wakalipigia kura na kuidhinishwa kwamba lirudishwe kwenye masuala ya Muungano. Lakini leo hii Wazanzibar bado wanasikitika, Wazanzibari bado hatujaridhia suala hili kuwa katika mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninukuu kwenye Katiba ya Zanzibar Ibara 132 (1) na (2) ambayo inasema:-

(1) "Hakuna Sheria yoyote itakayopitishwa na Bunge la Muungano ambayo itatumika Zanzibar mpaka Sheria hiyo iwe kwa ajili ya Mambo ya Muungano tu na ipitishwe kulingana na maelekezo yaliyo chini ya vifungu vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

(2) Sheria kama hiyo, lazima ipelekwe mbele ya Baraza la Wawakilishi na Waziri anayehusika."

Kwa hiyo, sidhani kama imepelekwa katika Baraza la Wawakilishi na Waziri anayehusika na Wazanzibar kupitia Wawakilishi wao kwamba wameridhia suala hili liwe miongoni mwa mambo ya Muungano. Vilevile Wazanzibar hatufurahishwi na hili na pia tunataka tuone katika maazimio ya Wajumbe wa Baraza la

Wawakilishi wanaazimia kwamba, hili suala lisiwe miongoni mwa mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakumbuka vizuri, hotuba yetu ya Kambi pia ukurasa wa 51 imetaka ufafanuzi wa jambo hili, kwamba, Bunge limesema hili suala limepitishwa kihalali na hakuna tatizo lolote, lakini tunaona bado linakuwa tata. Kambi ya Upinzani inataka Serikali itolee ufafanuzi. Siyo mara ya kwanza suala hili tunalitaka Serikali kutoa ufafanuzi kuhusiana na mafuta ya Zanzibar na masuala ya gesi, hata ukija kwenye mikataba ambayo imesainiwa. Mimi napendekeza kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ambayo nahisi yafanyike katika mikataba ambayo inasainiwa au inahusika na masuala ya mafuta *TPDC* hawahusiki kabisa, hawana *mandate* yoyote katika masuala ya Muungano na mafuta ya kule. Kwa hiyo, tunakuta vitalu namba 9,10,11 na 12 vimesitishwa kufanya uchunguzi wake katika uchimbaji wa mafuta kwa sababu wanasubiri vikao. Vikao hivi mpaka sasa hivi haipungui miaka kumi vinaendelea kukaliwa; hivi vikao vya kupunguza kero za Muungano.

Miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa ni hayo. Suala hili siyo chini ya miaka kumi Serikali haijatoa jibu. Hivyo, tunapendekeza kutatua hili tatizo kwa muda mfupi kama Wizara husika, kwamba haiwezekani Waziri wa Muungano anaposaini mikataba asaini kama yeye wakati suala hili ni la Muungano na kama basi mmeamua kuwa hivyo kwa kutatua kwa muda mfupi,

napendekeza kwamba Mawaziri wote wawili kutoka Zanzibar na Bara, wahusika katika Wizara hii nao wawe wanahusishwa katika kusaini mikataba hiyo kwa faida ya watu wote na siyo kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunasubiria suluhisho la muda mrefu ambalo sisi tunapendekeza mafuta yasiwe suala la Muungano, na gesi pia ibaki kuwa kila mmoja anachimba kivyake na vilevile Zanzibar kuwe kuna Taasisi au Mashirika ya masuala ya uchimbaji wa mafuta kwa Zanzibar peke yake na kwa upande wa Bara nayo iwe kama hivi ambavyo tunaiongelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuongea na ambalo nimeshawahi kuongea na napenda nilirudie kwa kuwa linaendelea kuleta madhara kwa upande wa Pemba, Bunge lililopita kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu nilichangia kwamba kuna eneo la Jeshi ambalo wao wanaita *Mess. Mess* ipo katikati ya makazi ya watu. *Mess* hii haipo katika Kambi yake ya Alhamis kule macho manne. Juzi niliongelea mambo mbalimbali ambayo yangeleta madhara na kuitaka Serikali ihamishe *Mess* na kurudisha katika Kambi yake ya Alhamis. Wanajiita wasikivu, lakini wametia pamba za masikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme kwamba wiki iliyopita katika *mess* ya Jeshi la Polisi kule Pemba, kulikuwa kuna maonyesho ya Bibi Kidude na kiingilio kilikuwa Sh. 1,000/= kwa kila ambaye anaingia. Kwa kuwa yapo katikati ya makazi ya watu, kuna

mtoto wa miaka 14 ambaye angependa kuona, hakuwa na pesa akabaki anachungulia.

Askari wa Jeshi la Polisi wakaamua kumu-*arrest* huyu mtoto wakampiga na kumpeleka Hospitali ya Mkoa wa Pemba, na hospitali anaonekana mtoto yule ana madhara na amepewa *transfer* na hivi ninavyoongea mtoto huyu yupo katika Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja kule Zanzibar kwa kupata mashumbulizi na maumivu ambayo aliyapata kutoka kwa Jeshi la Polisi baada ya kuwa anachungulia *show* hiyo kwa kukosa kiingilio cha kuingia. Kwa hiyo, hayo ni miongoni na madhara ambayo yanaletwa kwa Serikali kutosikiliza maoni yetu ambayo sisi tunayaongea na kutaka Serikali iyafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suluhisho katika hili na napenda kulirudia tena, Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba ulisikilize hili na ulifanyie kazi. Tunataka ile *mess* irudi katika Kambi za Alhamis iendelee kuwa katika eneo ambalo halitawa-*interfere* wananchi na shughuli zao za kawaida na haitakuwa kero kwao kwani kwa sasa tunaona kwamba imekuwa ni kero na wananchi wanapata taabu na masikitiko mengi na tuna orodha ya masikitiko ya matatizo ambayo wananchi wanalalamika kuhusiana na *mess* kuwa katikati ya maeneo ya watu kutokana na mambo ambayo wanayafanya hayaendani na sehemu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda niliseme, kabla ya kutoa mfano mzuri wa leo asubuhi, kwa kweli nimesikitwa na majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi. Wakati Mheshimiwa Zitto

ameuliza swali la nyongeza humu ndani, nadhani labda tupewe semina kuhusu kitu gani kinatakiwa kijadiliwe ndani ya Bunge kama Wabunge tunaowawakilisha wananchi. Tuliapa kwa kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano na kutenda haki na kuwa waadilifu katika kazi zetu. Leo anauliza swali la kitaifa swali ambalo linawasaidia watu wa upande wa pili katika kupata nafasi mbalimbali za uwakilishi nchini, nasikitishwa Waziri amelijibu swali kisiasa zaidi kuliko vile ambavyo alikuwa anapaswa kulijibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni kweli kwamba hakuna...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa, Muda umekwisha, ahsante. Naomba kumwita Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, halafu tutaendelea na Mheshimiwa Martha Mlata baadaye.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumzia habari za ushirika hapa nchini, historia inatukumbusha kwamba Rungwe ni moja ya Wilaya anzilishi katika harakati za ushirika. Kutoka wakati wa Ukoloni, kulikuwa na Chama kinaitwa *Rungwe African Cooperative Union* ambacho kilibadilishwa jina kikawa *Rungwe Cooperative Union*

baada ya uhuru. Kwa kipindi chote hicho *RUCU* imejikita katika ustawi na maendeleo ya zao moja tu zao la kahawa. Wamekuwa wakishughulika katika kuhakikisha tunapata miche bora, kupambana na wadudu dhurifu na kueneza elimu kwa wakulima kuhusu uchumaji ulio sahihi na ukaushaji wa kahawa. Lakini kizuri kupita yote ni kwamba, soko lilikuwepo na Soko la Uhakika ndiyo wananchi walikuwa wanafaidi.

Mwananchi mwenye kahawa alikuwa anakwenda anauza halafu ikipelekwa kwenye mnada pesa za ziada zilikuwa zinaletwa, malipo ya pili au ya tatu yalikuwepo; tulikuwa tunaita mabaki. Napenda kukiri kwamba mchango wa kahawa katika maendeleo ya Wilaya ya Rungwe ni mkubwa, baadhi yenu ambao mmewahi kubahatika kufika Tukuyu ambapo ndiyo Mji Mkuu, ukiona magorofa upande wa kushoto yalijengwa na ushirika wetu, na naweza kudiriki kusema kwamba elimu niliyonayo *RUCU* ilisaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunakumbuka kwamba Serikali katika miaka ya sabini ilifuta ushirika na zao la kahawa liliathirika sana, huduma za ugani zikapotea, kukaanza kukosekana kwa madawa, lakini soko pia lilikuwa halitabiriki. Mashamba yakaachwa bila huduma na uzalishaji ukashuka na umaskini ukaingia. Ushirika uliporejeshwa ukakuta bei zilizokuwepo zilikuwa duni sana kwa miaka mingi, lakini katika kipindi cha mwongo huu tulionao miaka kumi hivi, bei ya kahawa katika Soko la Dunia imekuwa nzuri sana na hii imehamasisha wakulima, kwamba mashamba ambayo yalikuwa yameachwa sasa hivi

yamefufuliwa na mashamba mapya pia yameanzishwa. Mavuno yamekuwa mazuri kwa sababu ya bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini miaka ya hivi karibuni kumeingia mtindo wa kununua na kuuza kahawa mbichi, wengine wanaita kahawa mbivu, lakini kwa lugha ya kimombo inaitwa *red sherry,* ni kahawa ambayo unaichuma na kwenda kuiuza, utaratibu huu ni mgeni kwa watu wa Rungwe. Kwa bahati mbaya sana utaratibu una baraka za Serikali. Nasema hivyo kwa sababu makampuni ambayo yamepewa vibali, vinatoka Bodi ya Kahawa Tanzania *(Tanzania Coffee Board)* ambayo ni ya Serikali. Hii imeleta madhara makubwa sana katika *Industry* nzima ya kahawa katika Wilaya yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyojua, kahawa haiivi yote katika mti au miti kwa wakati mmoja. Inaiva kwa awamu, kwa hiyo, ni utaratibu wa kawaida kwa mkulima kuchuma ile iliyoiva na kuikoboa na kuisafisha na kuikausha na anaiweka kando, halafu akipata nyingine mpaka anakuja anapata gunia anauza na kupata mshiko wake. Lakini kilichotokea sasa baada ya utaratibu huu kutuvamia wa kuuza kahawa mbivu ni kwamba mkulima anachuma kidogo, anakwenda anamwuuzia huyu mnunuzi na kiasi anachopata ni kidogo sana kwa sababu ananunua kati ya Sh. 500/= na Sh. 800/= kwa kilo na hakuna bei ambayo unaweza ukai-*quote* kwa sababu inategemeana na wanavyokubaliana na huyu mnunuaji. Kwa hiyo, anachopata ni kiasi ambacho kinamsaidia kunywa pombe tu siku hiyo, na mwisho wa

msimu hana pesa kwa sababu hizi alikuwa anapata kidogo kidogo zinatumika siku ile ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kunakuwa na wizi mwingi sana wa kahawa mashambani na ni kitu cha kawaida kwa mkulima kuamka asubuhi akakuta matawi ya miti yake ya kahawa yamekatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni ambayo yanapewa vibali, wanakwenda moja kwa moja kwa wakulima, wana mtandao wao, wameweka mabango na bei wanakubaliana na mkulima mmoja mmoja, hawapiti Halmashauri. Halmashauri haina habari leo watakwenda wapi, na kwa sababu hiyo, hawapati ushuru. Tumefanya utafiti na kuwapitia wakulima wetu mmoja mmoja na kumwuliza anauonaje huu utaratibu? Asilimia 94.4 wakasema huu utaratibu hauwafai, na msimamo wa Halmashauri ni kwamba utaratibu huu usitishwe mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mifugo, Kilimo na Maji na mara zote tumekuwa tukiishauri Serikali na kuisisitiza kwamba Serikali iweke mazingira wezeshi ambapo kila zao liongeze thamani. Tumesema hayo kwa pamba, korosho, tumbaku, ngozi, samaki na kadhalika. Sasa najiuliza, ni busara gani ilielekeza kulichagua zao la kahawa peke yake kuruhusiwa kuuzwa bila ya kuwa *processed*? Sioni busara, najua kuna kanuni iliyotolewa na Bodi ya Kahawa, lakini iliwekwa kwa manufaa ya nani? Kwa vyovyote vile, siyo kwa manufaa ya mkulima, labda kuwanufaisha watu wengine, hatma

yake ni kuwafanya wakulima wa Rungwe kuwa fukara na manamba katika mashamba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kwamba lalamiko hili siyo mara ya kwanza kulisikia, nimetumwa na watu wa Rungwe kwamba Mheshimiwa Waziri atumie mamlaka aliyonayo kisheria, kikatiba kusitisha kanuni hii mara moja na ikiwezekana tamko litolewe kabla hatujamaliza Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni la barabara katika Wilaya ya Rungwe. Wilaya ya Rungwe ina barabara moja tu ya lami. Ni barabara ambayo inatoka Dar es Salaam mpaka Malawi, imekuwa bahati tu Mji wa Tukuyu ukawa katika eneo hili, na sidhani kama hii barabara ilikuwa inakwenda Tukuyu. Mtandao mwingine uliobaki ni barabara za udongo. Labda wenzangu hamfahamu, Rungwe ni Wilaya ambayo imebarikiwa kuwa na mvua nyingi sana karibu miezi minane mvua inanyesha, na tuna misimu miwili ya kuvuna. Ina maana kwamba Mungu katuepushia baa la njaa na tunashukuru sana kwa hilo. Lakini mvua siyo rafiki wa barabara hususan za udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri yetu inatumia pesa nyingi sana ili barabara hizi ziweze kupitika. Nina ombi maalum kwamba pale zinapogawiwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara, hili likumbukwe ili na sisi tupate mgawo ambao unakidhi haja yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa Saba mwezi Aprili, niliuliza kuhusu barabara mbili, mojawapo

inatoka Ikuti katika Jimbo langu, inakwenda Luswiswi na Itumba katika Wilaya ya Ileje, inaishia Itemba katika Wilaya ya Mbozi. Hoja ilikuwa, ni lini tutajengewa lami katika barabara hii? Jibu la Serikali lilikuwa fupi, lakini lilieleweka, nikawaambiwa Serikali haina pesa.

*(Kengele ya Pili ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakyusa nashukuru, muda umekwisha. Sasa namwita Mheshimiwa Martha Mlata na Mheshimiwa Clara Mwatuka ajiandae.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza kabisa, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili ya siku ya leo, lakini pia niwatake Wabunge wenzangu pamoja na Watanzania wa imani zote tuendelee kuiombea nchi yetu ili iendelee kuwa na amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, pia namshukuru sana na kumpongeza Rais kwa kupanga na kusuka upya Baraza la Mawaziri, lakini pia kuteua Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Nawapongeza Wakuu wa Wilaya wote walioteuliwa hususan Wabunge wanawake, lakini kwa karibu zaidi rafiki yangu na jirani yangu hapa Mheshimiwa Lucy Mayenga kwa kuwa namfahamu, ninaamini ataweza, nami nitaendelea kukuombea ili kazi yako iwe nyepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwanza kabisa, kwa kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa jinsi ambavyo imekuwa sikivu, kwa

sababu tangu mwaka 2006 mpaka bajeti ya mwaka huu imeweza kuwakumbuka wasanii na kuweka mikakati mizuri na kuwatangazia maharamia wote wa kazi za wasanii kwamba kiama chao sasa kimefika. Hivyo naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpangilio wote wa kuweka *stickers* za *TRA* nilikuwa naomba liongezewe jambo la kazi za sanaa za mikono kwa maana ya vinyago, Tingatinga, kazi za uchoraji na ufundi wa batiki na *tie and die* nafikiri tutakuwa tumewatendea haki wasanii wote. Pia naomba mchakato huu kwa ahadi ile, basi mwaka kesho Januari kazi hiyo ianze na ningeshukuru sana kuona kwamba *sticker* ya kwanza inaanza kwenye *album* yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naomba nirudi Mkoa wa Singida. Wananchi wa Mkoa wa Singida sasa hivi wamekuwa na maendeleo ya kasi kutokana na mazao yatokanayo na kilimo. Tunamshukuru Waziri Mkuu ambaye alileta Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu nikiwa mdogo nimeona kwamba kulikuwa na zao la biashara, lakini lile likapotea, ikaja pamba, sasa hivi inasuasua. Lakini zao ambalo nimeliona ni zuri na ambalo limewafanya wananchi wengi wametoka katika ule ufukara wa kukithiri ni zao la alizeti. Kwa kweli tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa zao lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza wananchi wote wa Mkoa wa Singida kwa kilimo cha alizeti na waongeze kasi. Tatizo kubwa ambalo linatatiza sasa ni soko. Ninaomba radhi kwa sababu Serikali ikiteleza, ni lazima sisi Wabunge tuseme ili ikae sawa sawa. Kuna tamko ambalo limetolewa na Mkuu wetu wa Mkoa kwa nia nzuri na kwa moyo thabiti kwa ajili ya kuweza kudhibiti bei ya mazao hasa kwa bei ya zao la alizeti kwa wakulima. Lakini tamko lile halikuja kwa wakati muafaka. Hivi sasa ninavyoongea wananchi wa Mkoa wa Singida wapo kwenye televisheni wanaangalia nini hatma ya tamko lile kwa sababu linapelekea mtu kwenda jela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuongea mengi, ninakuomba Waziri Mkuu uje Mkoa wa Singida uzungumze na wakulima wa zao la alizeti, uzungumze na wafanyabiashara wanaokamua mafuta wa viwanda vidogo vidogo, uzungumze na wale wote wanaofanya biashara ya zao hili ili tuweze kuweka muafaka twende kwa pamoja kwa sababu Mkoa wetu sasa hivi unashamiri. Singida sasa hivi vijana hawakimbilii Mijini, wamebaki Vijijini kwa ajili ya zao lile, wameweka jenereta, wameweka *DSTV,* nyungo zao, wanaangalia ulimwengu mzima mambo yanavyokwenda kwa sababu ya zao lile. Lakini mtafaruku unaokuja sasa ninapata wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, naomba niende katika hotuba ya Waziri Mkuu katika ukurasa wa 68. Ninakupongeza kwa sababu umeweza kuzungumzia namna Serikali itakavyoweza kukata na

kupunguza matumizi ambayo hayana tija kwa Taifa letu hususan upande wa magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikijiuliza, mbona kulikuwa na waraka enzi za Mzee Ruksa, Rais wetu Mstaafu Mzee Mwinyi, kulikuwa na waraka uliowataka wafanyakazi wote wa ngazi fulani wa Serikali wauziwe magari halafu wao watakuwa wanawekewa mafuta? Nafikiri Serikali ilifanya vile, watu waliuziwa magari, lakini cha kushangaza magari yale yaliwekwa pembeni, walichukua magari wakaanza kufanyia shughuli zao. Kilichofuata, waliendelea tena kupanga bajeti ya kununua magari kwa matumizi tena ya ofisi. Nikawa najiuliza, waraka ule ulishafutwa? Je umepitwa na wakati au unatekelezwa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno ya Waziri Mkuu katika ukurasa wa 68, naomba turejee waraka ule ili waraka uweze kufanya kazi, watu wauziwe magari, iwe rahisi kupunguza matumizi ambayo hayana lazima katika ofisi, kwa sababu mtu atalitunza gari lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi pekee katika nchi za Afrika Mashariki inayotumia magari kwa matumizi ambayo siyo ya lazima. Mimi huwa najisikia aibu sana hata tunapokuwa kwa mfano kwenye sherehe labda za kitaifa Uwanja wa Taifa, Mabalozi unaona wanaingia kwenye magari, wanakuja kwa pamoja wa nchi mbalimbali wanakuja uwanjani, lakini sisi tunashindana kupanga magari pale wakati Wahisani wetu wako pale. Hivi wanatuangaliaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dhana hii hebu tupunguze matumizi haya ya magari. Mimi nashukuru kwamba unashuka kwenda kwenye CC 3000 mpaka 2000. Ni kweli kuna watu ambao wanahitaji magari makubwa, sitaki kuwapendelea, lakini wapo watu ambao wanahitaji magari ambayo yanaweza yakawasaidia kutokana na kazi zao. Kwa hiyo, kila mtu apewe gari kutokana na kazi anayoifanya na wadhifa wake. Naomba hili lizingatiwe na kwa sababu wewe mwenyewe ulilianzisha ukatoka kwenye V8 ukashuka ukaenda mpaka *GX* lakini nashangaa walioko chini yako hawakukufuata na wala hawakutekeleza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba mpango huu ambao wewe umeusema utimizwe na wafuate ili azma yako ya kupunguza matumizi ambayo hayana ulazima iweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia suala la mikataba ya barabara. Ukipita katika barabara yetu kama unakwenda Shelui, ile barabara imeharibika sana. Mimi sielewi aliyejenga pale, hivi kweli bado tu yupo anaangaliwa? Hatakiwi! Mara moja aende akarekebishe pale. Kuna ajali mbaya sana zinatokea maeneo yale, na ni hatari sana hasa wakati wa usiku. Naomba Waziri Mkuu aende akatembelee pale, yeye mwenyewe akajionee. Naamini walio chini yake watafanya juhudi za makusudi kwenda kurekebisha eneo lile ambalo limeharibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia fedha za *radar*; naomba Halmashauri zote zipatiwe mgawo. Hakuna kusema kwamba tunanunua sijui vitabu, vitabu vya nini? Hawa Wazungu kwa nini watupangie matumizi ya hela? Si ilikuwa ya kwetu? Kwanini wanatupangia kununua vitabu? Kwanini tusinunue madawati au tujenge nyumba za Walimu ili waweze kuishi kule. Ninashauri kwanza kwenye Halmashauri zote, Halmashauri itaamua kwamba inapata shule moja ama ni darasa moja haijalishi, lakini naomba fedha hizi zisije zikatengwa zikaonekana zinakwenda kwa watu wachache. Tumerudishiwa kwa sababu zilikiuka maadili. Naomba fedha hizi zisije zikaendeleza ile dhambi iliyopelekea hela hii ikarudi. Ninaomba zitumike katika barabara kwa faida ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kengele karibu inagonga, niwaombe wananchi wa Singida watulie kwa sababu Serikali inawajali Watanzania na mambo yote yatakuwa safi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, nakushukuru sana.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Clara Mwatuka, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Mwambalaswa na Mheshimiwa Ezekiel Wenje wajiandae.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona iko haja ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia afya njema mpaka kufikia siku hii ninaposimama hapa kuchangia katika bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ipo mbele yetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwatuka, hamia *microphone* nyingine, hiyo inapiga kelele kidogo.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka jana katika hotuba ya Waziri Mkuu alikuwa amegusia suala la kukuza kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania. Ninavyoelewa, kukuza kilimo ni pamoja na wakulima kwa kuwa ndio wanaofanya kazi ya kilimo na kwamba wanahitaji baadhi ya vifaa vya kuweza kusaidia kukuza kilimo. Baadhi ya vifaa hivi ni pamoja na matrekta, pembejeo ili kuweza kuzalisha na kupata mazao zaidi ya ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wengi ni maskini, kilimo tunachotumia ni kilimo cha mkono cha majembe mafupi ambayo hayaendi mbali. Ningeomba kama kweli Serikali ina nia ya kukuza Kilimo kule kwa sababu Kusini kumekuwa Kusini hasa mkiani, kwamba kila jambo kule, kunakuwa kwa mwisho. Safari hii bajeti hii Waziri Mkuu ameizungumzia hivi, ina maana kwamba ameamua kutukuza, hivyo naomba atuangalie hata kwa macho manne matrekta yapatikane, tukiacha zile *power tiller* ambazo zinatumika tu kwa kubeba mizigo midogo, wanaosomba mchanga, wanaochukua matofali, lakini kwa kulimia zile *power tiller* hazisaidii chochote. Kwa hiyo, tunaomba matrekta yapatikane kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zinapopatikana zinakuwa zinacheleweshwa, zinakuja wakati umepita. Hivi sasa watu wameanza kupulizia mikorosho, *sulphur* au aina yoyote ya madawa haijapatikana. Sasa unapochelewesha na kuleta baadaye ina maana hapa unarudisha maendeleo nyuma. Hivyo, naomba zipatikane kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mpango pembejeo ya ruzuku. Ile mimi sijui wanaopata ni akina nani, kwa sababu bei ni kubwa, mkulima wa hali ya chini hawezi kufikia. Kumbuka mwaka jana ilikuwa Sh. 96,000/= sasa kwa mtu wa chini siyo rahisi apate fedha hizi. Hivyo, naomba tuangaliwe wakulima, maana na mimi ni mkulima, naomba tuangaliwe kwa sababu wakulima pamoja na kwamba tuna udhaifu kwamba tunatumia zana duni, lakini tunachangia katika kodi ya maendeleo na pato la Taifa pia. Sasa tunapoachwa nyuma kwa kweli tunasononeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi, 2010 kulikuwa na mabilioni ya Kikwete walisema wanakopeshwa wakulima. Mimi naona wakulima waliopata mikopo ile ni wale wakubwa, lakini wadogo, wa hali ya chini, hawakupata. Hivyo, tunapakwa asali kidevuni wakati ulimi haufiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, kule kuna zao la korosho ambalo ndiyo tegemeo letu. Sasa zao hili soko lake linasuasua mpaka hivi sasa mimi bado sijaridhika nalo. Nikichukulia makato yanayokatwa ni mengi kiasi kwamba yanapunguza pato lile. Halafu

naomba tulielewe hili, kwanza niulize nani mfanyakazi au mtumishi ambaye anakubali mshahara wake apate nusu nusu? Nafikiri hayupo, kwa sababu unapompa nusu nusu, maendeleo yake hayawezi kufikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la stakabadhi ghalani. Mpango wa stakabadhi ghalani ni mzuri, tena msimu uliopita mwaka juzi mpaka mwaka jana watu walifurahia. Lakini mwaka huu tulionao mpaka hivi sasa kidogo umeleta mtafaruku.

Ukweli ni kwamba mpango huu wa stakabadhi ghalani ingekuwa kwamba kiasi kinachopangwa mkulima anapewa chote halafu wakishauza faida ile *(bonus)* wanapewa, ingekuwa nzuri. Kwa sababu unapokata kwa mfano ilikuwa Sh. 1,200/= ukimpa Sh. 600/= au Sh. 800/= kule nguvu tunakopa kwa wananchi. Mtu hawezi kulima shamba ekari nane au 10 peke yake, anakopa nguvu kwamba akishauza mazao yake ndipo alipe. Sasa unapompa nusu nusu zile zinaishia kulipa vibarua waliosaidia kupalilia. Anapokwenda anunue sabuni, chumvi, ampeleke mtoto shule zile zote zimekwisha.

Sasa kama alikusudia kwamba atanunua bati mbili, tatu, ajenge kibanda chake, hatafikia, kwa sababu zile nyingine haziji kwa wakati wa haraka, wanachukua muda. Sasa zile zimekwisha, zinapokuja zile kidogo ina maana mipango imeharibika. Hivyo, ningeomba waliangalie hili kwamba zipatikane kwanza zile, na makato yale yachukuliwe zile za faida *(bonus)* zile. Nafikiri nimeeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende upande wa elimu. Ndugu zangu hapa ndani tuliopo, bila mwalimu tusingefika hapa. Kuelekeza akili za mtu ni kaz! Mtoto mdogo kumfundisha kutokea mwanzo ajue mama, baba na kuendelea inachukua muda, na ni kazi. Sasa mwalimu anamchukua mtoto kule, hajui lolote, anaanza kumfundisha pale mpaka anafikia hatua hii tulioko hapa, huyo anastahili heshima na kutukuzwa na kujaliwa.

Walimu kwa kweli angalia mshahara wa kima chini Sh. 244,400/= wakati Idara nyingine zinaongezeka zaidi ya pale. Wakati mwalimu anafanya kazi usiku na mchana, akishamaliza masomo mchana, usiku anakwenda kuandaa masomo ya kesho. Halipwi *overtime* huyu. Kwa hiyo, tuangalie sana hawa tuwape nao angalau nyumba, kidogo ingefuta machozi. Lakini nyumba hakuna, mshahara ndiyo huo mdogo, kwa kweli mwalimu hawezi kufanya kazi kwa moyo mweupe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la upungufu wa walimu mashuleni. Hili halileti hasara kwa mwalimu peke yake kwamba wanakuwa wachache hata wanafunzi wanakosa kupata masomo yote yanayohitajika. Unapofika mtihani wanakosa, Serikali haiangalii kwamba masomo mengine hawakufundishwa, matokeo wameshindwa. Ni wameshindwa! Shule hazina maabara hasa hizi za Kata hakuna maabara, hakuna; vitendea kazi vyenyewe havitoshi. Kwa hiyo, suala la elimu liangaliwe kwa macho manne, jamani ni kazi kubwa.

Tunapowanyima hawa kupata masomo haya mengine, ina maana kwamba tunarudisha nyuma elimu. Kwa hiyo, naomba wapatiwe elimu. Sehemu nyingine, nyumba za walimu, kwa mfano, nikiangalia Wilaya ya Nanyumbu walipangiwa madarasa matatu na hela zipo, lakini hakuna hata darasa moja walilojenga. Wamekwenda nyumba za walimu tatu, hakuna. Sasa hawa wanafanyaje? Naomba tuangalie hili, angalau moja moja lingekuwepo, hela zile zipo hazijatumika, zitafanya kazi gani? Kwa nini zisitumike? Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie. *(Makofi)*

Pamoja na haya, naomba niongee kuhusu maji. Maji ni uhai. Sasa tunapokwenda tukakosesha maji sehemu nyingi, watu wanapata shida hasa akina mama. Kule kuna mradi wa maji Mbwinji. Mpango huu umepita sehemu nyingi walipokuwa wanaweka mtaro kwa ajili ya mabomba. Katika kupitisha maeneo yale, walikuta mazao yangali mashambani yakang'olewa. Lakini hawajalipwa fidia ingawaje waliahidiwa kwamba yataangaliwa mapema, wapewe fidia. Mpaka leo hii, sijui nyuma yangu, mwezi huu, lakini mpaka naondoka ilikuwa bado. Naomba watu hawa washughulikiwe kupewa fidia kwa mazao yaliyoharibika wakanunue chakula. *(Makofi)*

Pamoja na maji hayo, Masasi kuna visima vingi ambavyo waliweka matanki, lakini pampu hakuna. Naomba visima vile vishughulikiwe. Maji yale ya Mbwinji yaliyopita yanakwenda Nachingwea na Masasi yamepita mjini, hayo yanakwenda mpaka leo Masasi ndoo Sh. 500/=. Sasa hali kama hii naona Serikali iliangalie, vile visima vilivyopo vishughulikiwe kuwekewa

pampu kufufua, na kule kunapohitaji *motor* zisukume maji, zifanyiwe hivyo ili watu wanufaike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la viwanja, ardhi. Kuna sehemu nyingine…

*(Hapa kengele ya pili ililia kushiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Tunashukuru Mheshimiwa Mbunge. Kengele ya pili.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa leo hii. Lakini pia nakushukuru wewe kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kuipitia vizuri, lakini yale mambo muhimu ambayo nilifikiria yatakuwemo hayakuwemo. Kwa msingi huu, naikataa kabisa hotuba ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar ina Serikali yake. Kama Serikali yoyote, Serikali ya Mapinduzi Zanibar inahitaji fedha kwa ajili ya uendeshaji. Nasema hivi kwa sababu mambo yote ya uchumi wa Zanzibar yameingizwa katika orodha ya Mambo ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara ya 133 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeelekeza jinsi ya kufungua akaunti ya pamoja *(Joint Account).* Lakini kifungu cha 132 kinaelekeza jinsi ya kuunda Tume ya pamoja ya fedha *GFC*. Mnamo mwaka 1996 kama sikosei tulipitisha Sheria ili kuwezesha Tume hii kuundwa. Kutoka mwaka 1996 hadi hii leo ni mwaka wa 16. Lakini Tume hii ya fedha imefanya kazi kwa muda kipindi cha miaka nane. Miaka nane kama utazaa motto, basi utampeleka shule. Tume hii bado haijafikia malengo yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifungu hivi vimo katika Katiba yetu. Utekelezaji wake unasuasua. Sijui ni Serikali ya aina gani inayotekeleza Katiba katika kusuasua. Suala hili la kuunda Tume ya Pamoja ya Fedha ina maana kwamba yale mapato yote yanayohusu masuala ya Muungano pamoja na kutoa gharama zake, basi lazima kuwe na mgao wenye *formula* sawa. Lakini hili limewekwa vikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume hii haifikii maamuzi. Kwa taarifa niliyoipata ni kwamba Zanzibar kupitia Baraza la Mapinduzi limepeleka taarifa zake. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba taarifa hizi zimepelekwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu na zimekwama. Pia zimekwama katika Wizara ya Fedha, sielewi kwa nini zinakwama. Kama Kamati hii imechukua miaka nane haijafikia maamuzi, sielewi kwa Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha zitachukua miaka mingapi? Lakini sielewi ikitoka hapo inakwenda kwa Baraza la Mawaziri, sielewi huko Baraza la Mawaziri itachukua miaka mingapi. Hii

inawasaidia Wazanzibar, na nashangaa viongozi wetu wakuu wanashindwa kuliona hili kwamba hii *joint account* ikiwepo na fedha zikigawiwa sawa, basi Wazanzibar na wao wataweza kujikwamua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar ni nchi ndogo tu, bajeti yake haizidi Shilingi bilioni 600, ni Wizara moja ya Waziri Mkuu. Leo wanaomba waongeze 0.5 katika makusanyo yale ya 4.5 ambayo wanapata kila mwaka, lakini sasa imekwama kwa Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Serikali na imekwama kwa Waziri wa Fedha. Tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kama hilo ni sahihi, alifanyie kazi ili tusizungumze tena suala hili, tumechoka. Hakuna mtu yeyote ambaye halijui, Wazanzibar wamechoshwa na suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapozungumza Wazanzibar msiwatazame chini mpaka juu, wana sababu kama hizi. Ni sababu ambazo zinatupelekea sasa watu hawaaminiani tena. Kwa nini hatutekelezi Katiba yetu? Kifungu cha 133 na 134 vinaeleza. Kwa mujibu wa kifungu hicho hicho 132 (2) (a) tayari Zanzibar imeshachukua jukumu lake, imeshapeleka taarifa zao, lakini bado wenzetu wana kigugumizi. Tunaomba suala hili mlifanyie kazi sana, linawakandamiza Wazanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze suala lingine ambalo bajeti iliyopita nilizungumza kwa hamasa sana, lakini kwenda kwenye *Hansard* sijaliona na leo nalizungumza tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waislam wa Tanzania Bara wanapoteza haki zao za ndoa, taraka na mirathi. Kutoka mwaka 1971 huu ni mwaka wa 41. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria tuliyonayo, *the Law of Married Act of 1971* haikubaliani hata kidogo na Sheria za Kiislam. Tunapozungumza Waislam, tafadhali muwe makini kabisa. Sizungumzii udini, nazungumza haki kwa Mtanzania. Sheria hii ya mwaka 1971 katika kifungu 160 kinasema: "Kama kutakuwa na mwanaume na mwanamke watakaa pamoja ikifikia miaka miwili au zaidi, basi hawa wanatambulika kama mke na mume." Sheria ya Uislam haikubaliani. Hiyo inasema ni zinaa. Nimewauliza hawa Wachungaji ndani ya Bunge hili wanasema, hiyo ni zinaa. Mila na Desturi zinasema ni zinaa. Mimi siwezi kukosea kusema kwamba Tanzania imehalalisha zinaa. Sioni sababu kwa nini nisiseme hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 107 kinasema, kama utamwacha mke wako, haachiki mke huyo mpaka uende Mahakamani kwa vigezo maalum. Uislam haukubali hivyo, ukiacha ndani ya imani yako ukathibitisha umemwacha, ameachika. Leo inafikiaje hakimu anakwenda anasema hajaachika halafu mwishoni anakaa tena ameacha? *(Makofi)*

Tuchukulie kwa mfano, Waislam wamefunga ndoa ya Kiislam, wameachana kwa hiari yao, lakini mmoja akafanya uhuni tu hawataki kugawana mali. Sasa aende wapi kupata haki yake wakati chombo cha kusimamia haki za Waislam hakipo? Namwomba

Mheshimiwa Waziri Mkuu, suala hili la kuunda Mahakama ya Kadhi lifanyiwe kazi mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hili ni jukumu la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kesho atakwenda kujibu kwa Mwenyezi Mungu kwa nini Waislam wanapoteza haki zao? Nasema hili, nampenda Rais wetu, tuanzishe hii Mahakama ya Kadhi. Mahakama ya Kadhi ipo Zanzibar, Waislam wapo Zanzibar, Wakristo wapo Zanzibar, hakuna mgogoro wowote. Mahakama ya Kadhi ipo Kenya, Mahakama ya Kadhi ipo Afrika Kusini, Mahakama ya Kadhi ipo Uganda, Mahakama ya Kadhi ipo Uingereza, Mahakama ya Kadhi ipo Australia, jamani tunaogopa nini kuanzisha mara moja suala hili ili Waislam wakapata haki zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda haraka haraka, nizungumzie kuhusu suala Utawala Bora. Utawala Bora na uwajibikaji ni jambo muhimu sana katika Taifa lolote. Utawala Bora na uwajikaji unajenga nidhamu ya ukusanyaji kodi, unajenga nidhamu ya matumizi bora ya fedha za umma, inajenga nidhamu ya kutekeleza haki na usawa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu kipindi cha kwanza cha Awamu ya Nne cha Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alifanya mabadiliko makubwa ya Baraza lake la Mawaziri ni jambo la kawaida, anaruhusiwa kufanya mabadiliko yake. Lakini sababu ilikuwa ni ufisadi na rushwa ndani ya Bunge hili. Kwa maana hii ni kukosa utawala bora na uwajibikaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipindi hiki cha pili imeonekana amebadilisha tena Baraza la Mawaziri…

*(Hapa Kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi kunipa fursa niweze kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama nikitambua kwamba hili Bunge lilianza zamani hata kabla sijazaliwa na kuna Watanzania wengi walipata fursa kuchangia na kushauri Serikali ndani ya Bunge hili. Wengine mawazo yao yalichukuliwa, wengine mawazo yao yalipuuzwa. Lakini naomba vile vile niendelee kuingia katika rekodi za historia ya kuendelea kushauri Bunge hili na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianzie kwenye suala la *cost of administration* ya Serikali yetu. Nimekaa muda mrefu sana nikitafakari. Mheshimiwa Waziri Mkuu amejaribu kuonyesha viashiria kwamba angalau Serikali inakwenda kuanza kuchukua hatua za kuanza kupunguza matumizi mengine Serikalini, *specifically* wame-*mention* magari. Lakini kama kweli tunataka tusonge mbele, lazima tuchukue *cost measures effectively na seriously*. Sasa leo nilikuwa najiuliza, Tanzania tunapata misaada kwenye nchi nyingi duniani. Tunapata misaada Japan, *USA, Britain*, mpaka

Ufaransa, Brazil, nchi zote. Ukiangalia *Japan, the size of their cabinet*, wana watu 18, ukiangalia *United States current cabinet* ya Barack Obama ina *cabinet secretaries* ya 15, ukiangalia *United Kingdom* ya *Cameroon, in their collision government* ina watu 21, ukiangalia France ina watu 23, sasa sisi tunaopata msaada kwa hawa watu, hiki kiburi cha kuwa na *blotted cabinet* ya *more than 50 ministers* tunapata wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli Serikali hii iko *serious*, inataka kubana matumizi ili pesa ambazo zinatumika visivyo ziende kusaidia mambo mengine kwa Watanzania. Sisi ukiangalia *all laws of wealth creation in this world, states that: "You work hard like a slave today, so that you live like a king tomorrow."* Sisi Tanzania, *we live like a king today, so that we become more beggars tomorrow. This is irrelevant* kwenye *wealth creation.* Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukitaka kujua kwamba matumizi ya Serikali ni *abnormal,* yaani kwenye *economics this abnormal expenditure* leo Wakuu wa Mikoa wote wameletwa hapa kutoka nchi nzima. Wametumia gharama za kuendesha magari, wanakuja, wanalipwa *per-diem* kuja kula kiyoyozi hapo *Speaker's gallery,* wanakuja kufanya nini? Hizi hela *can do something else*. Toka Jumamosi wako hapa. Kwenye Wizara zote, utaona ikifika Wizara ya Ulinzi na Usalama, watu wamejaa pale, ikifika Wizara sijui ya Ujenzi watu wamejaa. Wanakuja kutafuta nini? Kwenye Wizara ya Waziri Mkuu kuna watu ambao ndio *architectures,* wapo wataalamu ndio angalau kama

wangekuja hapa *it could be justifiable,* nyie mmeleta Wakuu wa Mikoa wote hapa, wameacha kazi huko Mikoani, wako hapa wanakula kiyoyozi, *RAS* wako hapa wanafanya nini? Hebu jaribuni kubadilisha *techniques* kama hizi kama kweli mnataka nchi isonge mbele *seriously*. Mimi nawapa *free advice*.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, juzi hapa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, kuna ubadhirifu ulitokea wa Shilingi zaidi ya bilioni mbili, akasimamishwa kazi Mkurugenzi pamoja na kuwa Idara kama kumi. Walisimamishwa kazi! Aliyegundua kwamba zaidi ya Shilingi bilioni mbili zimepotea ilikuwa ni repoti ya *CAG*, sasa *CAG* ni mtaalam, amesha-*establish* kwamba kuna pesa zinapotea, halafu nyie bado Mkuu wa Mkoa anakwenda kuunda Tume. Tume ya nini? Hii Tume bado inalipwa tena pesa za walipa kodi ambazo zingefanya kazi nyingine kule Sengerema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kwa niaba ya wananchi wa Sengerema, mimi natoka Mkoa wa Mwanza, sisi Wabunge wa CHADEMA ni Wabunge wa Taifa, sio wa Nyamagana tu, tunapiga kura kila kona. Ni hivi, wananchi wa Sengerema wamenipigia simu, wanaomba hizi fedha zao zirudi Mheshimiwa Waziri Mkuu na hii Tume haina haja ya kuunda tena Tume, wakati *CAG* ambaye ndio wataalamu walishagundua mambo haya na ikaweka ripoti hii wazi, Tume ya nini tena? Hii ni *dildul*. Pelekeni watu Mahakamani kieleweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia hii ripoti ya Waziri Mkuu, hotuba yake ukurasa wa 18 kuna

kitu wanazungumzia ndiyo *Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania,* kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu anampongeza Mheshimiwa Rais kwamba alikwenda sijui kwenye kikao cha G8 *summit* akafika pale, akawasilisha sijui mipango yetu ya kilimo. Kwa hiyo, wanampongeza sana kwa sababu nchi yetu inakwenda kupewa 1.4 *trillion shillings* kukuza *agriculture.* Sasa kwenye hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu anajaribu ku-*justify* safari nyingi anazofanya Rais kwamba zile safari zina tija. *It is shameful, how can a father be proud* kwa misaada? *What makes a man proud in this world? It is the money earned out of his effort, out of his knowledge and out of his strength,* siyo msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea hata kwenye ule Mpango wa Miaka Mitano uliowasilishwa hapa Bungeni *last time, I expected* kwamba *one of the things* ambazo huu mpango unatakiwa i-*address* ni jinsi gani kama Taifa tunakwenda kuanza kupunguza *dependents on foreign aids and grants* kwa sababu *the only thing that can make a man proud, the only thing that can make a country proud is the ability to create its own source of income* siyo *ability* ya ku-*attract* misaada mingi. *This is shameless*. *This is shameful anyway*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie kwenye pamba. Ni hivi, naomba wananchi wa Mwanza waelewe kwamba sisi kwenye Kata zetu 12 za Wilaya ya Nyamagana hatulimi pamba hata kwenye Kata moja, lakini pamba inayolimwa Bariadi, pamba inayolimwa *in the all Mwanza region* ndiyo inafanya

wafanyabiashara wa Mwanza wanafanya biashara. Pamba ambayo wakulima wanalima Bariadi wakishauza wakapata hela, ndiyo inaendesha uchumi wa Mkoa wa Mwanza na uchumi wa Mji wa Mwanza kwa ujumla. Kwa hiyo, kumekuwepo na malalamiko mengi ya wakulima wa pamba wa Mkoa wa Mwanza. Naomba niungane na Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Mwanza kuhusu msimamo wetu kwenye zao la pamba kwamba bila Sh. 1,000/= haiuzwi pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye samaki. Mheshimiwa Nyerere amegusia hapa zao la samaki na mgogoro ambao upo na kauli ya Waziri iliyotolewa leo. Kauli hii ya Waziri inasema kwamba bei ya samaki inakuwa *determined* na *forces* zinazotokea kwenye hilo Soko la Dunia ambao sisi kama Taifa *we have no controls*. Je, Serikali haioni kwamba sasa ni muda muafaka wa kuweka *subsidies* kwa haya makampuni yanayonunua samaki ili pale bei inapoporomoka kwenye Soko la Dunia, basi huyu mvuvi aliyechukua mkopo benki ili aingie kwenye uvuvi asije akapata hasara akafilisika? Leo kuna watu wamenipigia simu wengine wanasema Mheshimiwa Mbunge sisi tumeshakimbia, tumehama na Mwanza kwa sababu bei ya samaki imeporomoka; tunadaiwa, hatuwezi tukalipa tena madeni. *This is verry serious.* Kwa hiyo, samaki na pamba ndiyo vitu viwili vikubwa vinavyoendesha uchumi wa Kanda ya Ziwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba hii pia muichukulie kwa uzito wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Mheshimiwa Hamad Rashid, alizungumza hapa kidogo kuhusu mwekezaji mmoja na nimepewa vielelezo hapa nakuletea kwenye kiti chako. Kuna mtu anaitwa Mark Rene Rowland, huyu mtu ndio alisema Mheshimiwa Hamad Rashid hapa kwamba ni mtu mmoja raia wa nchi isiyojulikana, ana *passport* tatu za Belgium ziko hapa, ana *passport* mbili za Burundi ziko hapa, ni mtu mkorofi, mtu mwenye kiburi, aliwahi kumtukana mpaka Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu kipindi alikuwa Kamishna wa Madini anajua, aliwahi kumtukana *Zonal Officer* wa madini kule Mwanza, anajua; alishawahi kumwonyesha kiburi Mheshimiwa Waziri Nahodha kipindi yuko Waziri wa Mambo ya Ndani na wakatoa *PI* kwamba huyu mtu arudishwe, baada ya siku chache huyu mtu amerudishwa nchini tena kinyemela hata bila Waziri kupewa taarifa. Ana kampuni inaitwa *Mineral Extraction Technologies Limited,* kampuni ambayo imekwepa kodi na ushahidi upo hapa. Kama tutaendelea kuvumilia wageni wa *style* hii, nchi hii haitasonga mbele. Lazima tuwe *serious* kama Taifa kulinda raslimali tulizonazo kwenye nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifanya tathmini leo kwenye makampuni yote ya kigeni kwenye migodi, wanaofanya shughuli ya *catering* ni kampuni moja tu ya Tanzania ndiyo inafanya kazi ya *catering* kwenye migodi ya *GGM* na migodi mingine sijui nafikiri iko kule Tulawaka. Lakini makampuni yote yanayofanya *catering* ukienda mpaka huko Mtwara wanakotafuta mafuta, makampuni yote yanayofanya *catering* ni makampuni ya kigeni. *(Kengele)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza hiyo?

**MWENYEKITI:** Ni ya pili?

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wenje nilikuwa naomba uwape Wasaidizi wetu ule ushahidi utuletee Mezani. Naomba sasa kumwita Mheshimiwa Charles John Mwijage, atafuatia Mheshimiwa Natse na Mheshimiwa Zainab Kawawa ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naona rafiki zangu wananichokoza, itabidi nianze na bashrafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza suala la migogoro ya bei ya samaki, kama ni kweli katika Ziwa Victoria watu wa Kenya wanakuja kununua samaki, wanalipa Sh. 5,200/=, Sh. 4,800/= naishauri Serikali yangu itumie busara tuwaache Wakenya na Waganda wachukue samaki, hawa watu wa Mwanza bei ikipanda wanunue. Watu wa Mwanza wanasema wanataka kulipa Sh. 2,000/=, watu wa Kenya na Uganda wanasema Sh. 5,000/= basi kama ni kweli, tumalize ugomvi, tuwaruhusu Waganda na Wakenya

wanunue, bei ikipanda Mwanza wanunue. Hiyo bashrafu namba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikipata vi-*message*, sishangai kwa nini watu wananitumia *message* mimi, wanasema oh, mnatamba mmevumbua gesi, mmevumbua gesi, mnatuambia *TCF, TCF* kitu gani? Walionitumia *message* nawajibu; *TCF* ni *trillion cubic feet*. Lakini Trilioni ukimwambia bibi yangu itamweleza nini? Nawajibu wapigakura wangu na rafiki zangu ambao wana imani katika mimi, lakini sio imani tu, mimi ni Mwenyekiti wa kisekta wa Nishati na Madini kwenye chama changu kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, gesi tuliyovumbua trilioni 25 mpaka 28, ukitafuta *equivalent crude oil barrows*, mapipa ya *crude oil* mlingano ni bilioni 3,744. Kama pipa moja utaliuza Dola 100, pesa utakayopata kwa pesa za Kitanzania ni Shilingi trilioni 600, bajeti ya Tanzania ni trilioni 15. Kwa hiyo, tunachozungumza sisi kwenye Kamati na Wanakamati wamenituma ni kuhakikisha kwamba gesi inavunwa na inatumika vizuri. Kuna mtani wangu alitaka kuniua asubuhi anasema, pesa ya gesi imeibiwa. Pesa ya gesi haijaibiwa, walioiba watapambana na TAKUKURU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetumwa kuipongeza na kuiunga mkono bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu nimetumwa kukuunga mkono kwa sababu ulipokuja kwetu, ulipofika kwa wale wafugaji wa samaki, sasa umeme umewashwa

na kule ulikowatuma *TIB* na *PASI* wameahidi kuwaletea mashine ya kutengeza chakula cha samaki. Nakushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na ndiyo maana naunga mkono. *Competitive advantage* ya wafugaji wa samaki ni ile mashine ya kutengenza chakula na namwomba Mheshimiwa Nagu alivyoniahidi, lazima aje nimpeleke Jimboni kwangu kusudi akachangamshe uchumi wa Jimbo langu. Wanamhitaji watu wa Muleba, Kamachumu na wanataka awaletee ruzuku ya mbolea ya samadi. Mheshimiwa Waziri Mkuu naunga mkono hoja bajeti yako. Ulipokuja kwetu, uliahidi umeme. Wamekuja ma-*surveyor* wa *REA* na *TANESCO* ma-*surveyor* wamefika, lakini nguzo hazijaja. Kwa hiyo, nakuunga mkono kusudi *REA* waende Kagoma, Nyakatanga, Buriakashajo wapeleke umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna mambo ambayo sikuyaona katika bajeti yako. Nilitegemea katika kuzungumza kwako utamke malalamiko yangu ya kila siku ya migogoro ya wananchi wangu, hukuyatamka. Naomba uhitimishe kwa kuyatamka na nakuunga mkono. Leo sitarudia, naweza nikalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuunge mkono Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ninakumbuka kwamba katika mazungumzo yetu sisi Wabunge, tuliwahi kuzungumza kwamba Wenyeviti wa Vijiji wangepewa chochote kutokana na kazi wanazofanya. Sijaiona, lakini nina imani kwamba muda ulikuwa kidogo, ulibaniwa muda, utashughulikia Wenyeviti wa Vijiji, sisi hatuna Watendaji. Wenyeviti wa

Vijiji ndio kila kitu, ndiyo Mahakama, Polisi ndiyo kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri kuhusu elimu. Elimu ina migogoro, kama kuna kitu kinaniuma, ni elimu. Mimi kipaumbele changu ni elimu, kipaumbele cha pili ni elimu na kipaumbele cha tatu ni elimu. Nashauri Serikali yangu kama mkiweza leo fanya, mkishindwa tujaribu bajeti ijayo. Mojawapo ya mwarobaini wa Sekta ya Elimu ni kuitoa TAMISEMI. Tuwe na Waziri anayesimamia elimu kusudi akishindwa tumkaange asubuhi. Elimu ipewe Wizara yake tujue mishahara ya walimu, tujue marupurupu yao. Naishauri Serikali yangu TAMISEMI ukubali upoteze elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, usalama wa Kagera. Ndugu zangu Wabunge wenzangu ukitoka Dar es Salaam au Dodoma kwenye kikao cha maamuzi, unakwenda Kagera, ukifika njiani unasimamishwa. Kama unakwenda Kigoma, ukifika njiani unasimamishwa, unaambiwa huku kuna majambazi. Suala la majambazi, suala la usalama katika Mikoa ya Magharibi ni tatizo. Kuna watu mamejenga makambi kwenye hifadhi, kuna watu wanahodhi silaha zenye nguvu. Tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu uliseme suala la migogoro, uliseme suala la majambazi, utafutie suluhu ya hawa watu wanaokaa katika nchi yetu na kufanya uhalifu na unapokuja na zoezi lile la kuwaondoa kuwarudisha kwao uwarudishe. Asiyependa wasirudi, awabakize kwake, lakini mimi nasema warudi. Ni majambazi na tungependa hifadhi zetu zikae na wanyama. Kwenye mifugo, watu wafuge, hatutaki majambazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu nizungumzie kipato cha Kagera. Kipato chetu cha Kagera kiko duni sana, lakini mojawapo ya njia ya kuongeza kipato ni kujali ule mtandao wa watendaji. Watendaji wanao wajibu wa kiutendaji, wahimize wananchi wafanye kazi, lakini wale Watendaji wa Vijiji, Wenyeviti, Watendaji wa Kata, Makatibu Tarafa muwajali maslahi yao, muwape usafiri. Nilikuwa na malalamiko ya Makatibu Tarafa wangu, bahati nzuri Waziri aliyepewa Idara hii ni rafiki yangu, amesema yeye atayashughulikia. Waziri wa Utumishi nategemea Makatibu Tarafa wangu 14 wa Mkoa wa Kagera utawapa masurufu yao kusudi wanisaidie. Wale mimi ndio moyo wangu. Nakushukuru naona unapiga makofi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna suala la ushuru na tozo. Nimezungumzia Watendaji kwa sababu Watendaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu hawakujiandaa vizuri kukusanya ushuru na tozo. Ushuru na tozo umekuwa kero. Naendelea kuomba Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na maelezo ya asubuhi, ule ushuru, tozo *barrier* ziondoke. *Barrier* ziondoke, tujipange. Mimi kwenye Halmashauri yangu nilishiriki lakini yanayotekelezwa siyo yale tuliyoamua. Tulisema wanaokuja kwenye gulio kufanya biashara ndiyo watoe, wanaokwenda kutembea wasitozwe kodi. Mheshimiwa Waziri Mkuu utuokoe tuweze kuwaondolea kero wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye kipato. Kipato cha watu wa Kagera hili nizungumze taratibu. Jana nilikuwa na *lecture* na Mkuu wangu wa Mkoa

mpaka usiku. Bahati mbaya wale ambao hawaongei na Wakuu wao wa Mikoa wakija huku na Ma-*RAS*, tumefanya mambo mengi ya maana. Tunaomba sisi watu Kagera, mturuhusu tuuze ndizi, tuuze kila tulinacho kwenda Sudan ndiko liliko soko. Mtupatie ruzuku. Nilishaomba, nimeona Mama Nagu umepeleka matrekta kwenu, ulete matrekta kwetu tulime mbaazi, alizeti na mihogo, kusudi tupeleke kwenye soko la Sudan, mtuwezeshe zaidi kuliko kuja kutuangalia kwa kutuleta chakula. Inasikitisha*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, tumepata mvua nyingi Kagera, lakini mvua nyingi zimeharibu miundombinu. Madaraja yamekatika, nyumba, mashule yameanguka, wananchi wanahangaika, lakini hii ni ajali kubwa, ni maafa. Naomba mliangalie hili hasa Wilaya ya Muleba mnisaidie, mtusaidie kurejesha miundombinu hii. Mzee Lukuvi barua zimeshaandikwa, Mkurugenzi wangu amezileta Ofisi kwako, zipo. Mnisaidie kutengeza daraja la Chamukwikwi na daraja la Kishara. Mkiweza kutengeza haya, wananchi watazalisha chakula na watapeleka watoto shule. Lakini nireje kuzungumza, nimekuja hapa kuunga mkono bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kusudi yale yote ya Jimbo langu yaweze kutekelezwa, ya Mkoa wangu yaweze kutekelezwa na ya Tanzania yaweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa machache hayo, naishia hapo. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwa muda wa kuchangia tulionao ni mdogo sana, napenda kuanza moja kwa moja kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Tanzania, ni moja kati ya nchi tatu tu za Kiafrika, ambazo zimeingizwa katika Mpango wa *G8;* si jambo dogo, ni jambo la kujivunia. Mpango huu wa *G8* ndio utakaotuwezesha sisi kuwekeza katika kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu kwa miaka kadhaa tumekuwa na misemo na juhudi nyingi katika kuwekeza kwenye Kilimo, Siasa ni Kilimo, Kilimo Kwanza, Azimio la Arusha, Chakula ni Uhai, Kilimo cha Kufa na Kupona na kadhalika. Lakini nchi yetu ina watu zaidi ya 40,000,000 na 80% ya Watanzania, wanaishi kwa kutegemea shughuli za kilimo. 34% ya Watanzania, wanaoishi kwa kutegemea kilimo ni maskini wa kutupwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nimwombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, mtoto wa mkulima, kama unataka Watanzania wa leo tukukumbuke, basi ni kuhakikisha kwamba, unai-*transform* hii *society* ya Watanzania ambao wako na maisha duni, kuwa katika *middle income earning society* kwa ku-*invest* kwenye kilimo. *You can never go wrong with agriculture in this country.* Kilimo kinahitaji nini? Kilimo kinahitaji ardhi, kinahitaji viwanda, kinahitaji miundombinu, kinahitaji watu, kinahitaji teknolojia na soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ni tajiri. Sisi hatuna shida ya ardhi. Tuna 44,000,000 ya hekta za ardhi ambazo zinafaa kutumika kwa kilimo. Katika hizo ni 26% tu ndio zinatumika kwa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna hekta 29,000,000 za ardhi ambazo zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Katika hizo ni 1% tu ndio inayotumika kwa kilimo cha umwagiliaji. Hatuna shida ya maji, maana tuna mito na tuna maziwa na mabwawa kedekede ya kutosha kwa kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni neema tosha kwa Watanzania. Hatuna shida ya watu maana tuna vijana wengi sana tumekuwa tukilia tatizo la ajira kwa vijana. Kilimo ni ajira, pelekeni teknolojia vijijini. Sambazeni umeme vijijini, vijana watarudi. Pelekeni barabara vijijini na hili naipongeza Serikali, sio kwamba, hatuna barabara kabisa, sisi tulikuwa tuna kilometa 200 tu za barabara ya lami, kutoka Dar-es-Salaam kwenda Morogoro. Lakini sasa hivi tuna maelfu ya kilomita zenye barabara ya lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vijana wa leo ni vijana wa teknolojia. Pelekeni umeme, unganisheni umeme kwenye kaya za Wanavijiji wote, mje kuwachaji gharama zao mtakapochaji gharama za *service* ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapeni vijana *skills* za kuweza kulima. Ni lazima muweke mapinduzi ya viwanda vijijini ili tuweze kukoboa mpunga, tuweze

kusaga kama ni mahindi tupate unga, tuweze kuuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niiombe Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi. Najua Serikali, imetenga shilingi takriban bilioni 70; bilioni 30 imepelekwa kwenye Benki ya Kilimo, bilioni 30 imepelekwa kwenye Benki ya *TIB.* Pesa hizi ni lazima zimwezeshe mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima ili aweze kuchukua mkopo mkubwa wa kuweza ku-*invest* kwenye kilimo, anahitaji nini? Anahitaji Hati, hati ya shamba lake. Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, imeainisha wazi kwamba, wananchi walioko vijijini ni lazima na wao wakubali kuchangia, ili kuwezesha kupata Hati za Kimila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Serikali yetu haitaonesha juhudi ya kuwasaidia wananchi kushiriki katika huu mchakato ili waweze kujipatia zile hati, ili waweze kuzitumia kupata mikopo na kuweza ku-*invest* vizuri katika kilimo na kuchangia katika kilimo chetu, ambacho sasa hivi tunasema tunapata 4%, ambayo pia ni 26% ya Pato la Taifa, pesa hizi zilizoingizwa kwenye Benki ya *TIB,* zitakazoingizwa katika bajeti ijayo, zinaweza zisiwafikie walengwa. Ni lazima Serikali, ifanye juhudi kuanzia awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza ku-*invest* sawasawa katika kilimo, nina uhakika tutakuwa tumeweza kutatua tatizo la ajira, tutakuwa tumeweza kutatua tatizo la mfumko wa bei, tutakuwa tumeweza

kutatua tatizo la uhaba wa chakula. Tutakuwa tumeongeza *income* kwa kuuza vyakula vyetu nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kama ya China, inatengeneza *products* mbalimbali inazoiga katika nchi nyingine, kama Marekani, Japan. Lakini *products* hizi haiwezi kuziuza Marekani wala Japan kwa sababu, *they are producing the same products.* Mnunuzi wa bidhaa za China na za Marekani na za Japan, ni Mtanzania. Usipomfanya Mtanzania akawa *middle income earner,* atanunuaje hizi *products?* Kwa maana ya teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bahati tuliyonayo uki-*produce* katika kilimo ni nini? Mchina, anaweza akaigaa, lakini hawezi kuiga mchele wa Kyela. Hawezi kuiga mchicha wa Tanzania. Hawezi ku-*produce* ma-*apple* yanayofanana na ya watanzania. Hiyo ndio faida ambayo sisi tunaweza tukaipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wenzangu leo wanaweza wakanishangaa ni kwa nini, nimezungumzia sana kilimo. Tunacho Chama cha Wafanyakazi wa Mashambani ninaowawakilisha. Kwa hiyo, leo nimewawakilisha vizuri wafanyakazi wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukuhakikishia Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mimi ni msemaji mzuri sana, kwa kuzaliwa ni mwanasiasa. Nina uwezo wa kukusemea vizuri mpaka kufa kwangu kwa sababu, naujua umahiri wako. Nina uwezo wa kuisemea Serikali

yangu vizuri sana kwa sababu, najua imefanya mengi. Nawashangaa sana wale ambao, safari moja kuna Gazeti la Rai, liliniandika, nadhani lilikuwa linanichonganisha tu, eti nilisema kwamba, Nyerere, akifufuka leo akiona hali hii, atahamia chama fulani. Nataka niwaambie *I am not a political mediocre.* Chama cha Mapinduzi ni Chama Tawala, siwezi kukilinganisha na chama ambacho hakijawahi kuonja madaraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwomba Waziri Mkuu na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, *just do me one favour, to invest* katika kilimo. Tu-*invest* katika kilimo, ndipo tutakapomkomboa Mtanzania kufikia katika kuwa *middle income earner. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimalizie, kuna maoni niliona yalitolewa kwamba, hii Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iko mingi sana. Labda tujaribu ku...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** *Ooh*, muda umekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nawaomba wenzangu wote, tuunge mkono hoja ili tumsaidie Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Awali ya yote, naomba nitume nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa bajeti yake ambayo ametuletea jana mbele yetu na kwa hivi sasa tunatakiwa kuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, naomba niseme, jamani pamoja na kelele zote, ukiona kinaelea ujue kimeundwa. Nchi yetu ya Tanzania, tulipotokea mpaka tulipofikia ni kazi ya sisi Watanzania wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwakumbushe ndugu zangu 1961, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, akiwa anadai uhuru wa Watanzania, naamini kabisa ni Mtanzania aliyekuwa kichaa tu ambaye, angekubali kuipokea nchi hii na kuifikisha hapa tulipo. Nchi ilikuwa haina barabara, nchi ilikuwa haina maji, nchi ilikuwa haina shule, lakini Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alijua Watanzania tunaweza; akaipokea nchi na akaiendeleza hadi hapa tulipofika. Ndio maana nasema hivi, tuna kila sababu ya kujivuna Watanzania, tuna kila sababu ya kujivuna Watanzania kwa sababu, Mwalimu Nyerere alithubutu, pamoja na Watanzania wa wakati ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile Watanzania wa sasa tumeweza kufikisha nchi hapa tulipo. Ombi langu kwa Serikali na kwa Watanzania wote, wakati tunatafakari kwenda mbele, tuna kila sababu ya kutafakari tunaondokaje hapa tulipo. Kwa sababu,

kuna kila ukweli kwamba, yako mambo yamefanywa na Serikali, lakini yako mambo ambayo kwa kweli, tunatakiwa tutafakari kwa pamoja ambapo naamini ni changamoto na katika changamoto, huna sababu ya kuziogopa, ni lazima upambane nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, naishukuru Serikali yangu kwa kazi kubwa ambayo imeifanya katika Wilaya ya Morogoro Vijijini na hususan katika Jimbo la Morogoro Kusini. Bajeti ya mwaka wa jana, tuliahidiwa suala la umeme; umeme umeshafika nguzo na waya mpaka Kata ya Kishemu, Kata ya Lundi na unaelekea Makao Makuu ya Wilaya ya Morogoro Vijijini, Mvuha. Tuna kila sababu ya kuipongeza Serikali kwa jitihada hizo na wananchi wangu wamenituma wana imani kabisa kwamba, mradi huu kufikia mwezi wa Tisa mwaka huu na hasa baada ya kupitisha bajeti hii, umeme utawaka Jimboni, Morogoro Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia bajeti, niombe sasa nimuulize au nitake kujua kutoka kwa Waziri Mkuu, Wilaya ya Morogoro Vijijini, Makao Makuu yake mpaka sasa yako Morogoro Mjini. Lakini katika Mpango Kazi wa Halmashauri, tulipendekeza kwa Serikali, kwamba, tunahamia Mvuha. Tuliletewa shilingi milioni 500 katika bajeti ya mwaka juzi, mwaka jana hatukupata chochote. Tumetumia pesa hiyo milioni 500 katika kutengeneza michoro, kutengeneza kupima viwanja, lakini vile vile kufanya *thorough test* na zimekwisha. Mwaka jana hatukupata hela na mwaka huu katika bajeti, kutokana na kikomo cha bajeti, imeonekana hatukupata hela. Tumetuma maombi

maalum ya shilingi bilioni moja. Nataka nijue kutoka kwenye Ofisi yako, nini hatima ya maombi yetu haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba vilevile nimuulize Waziri Mkuu, katika mchanganuo wake kupitia yeye mwenyewe au Wizara ya Maji, kuna ujenzi wa Bwawa la Kidunda. Mwaka jana tuliambiwa katika Bunge hili kwamba, ujenzi utaanza mwaka huu ambao unaishia sasa hivi. Lakini hadi hivi sasa wananchi hawajalipwa fidia, Halmashauri yetu haijapewa pesa kwa ajili ya kuandaa makazi mapya wananchi wetu hao. Tumepeleka vitu vyote *DAWASA* na tunaamini kwamba, vipo Wizarani, lakini hakuna kinachojulikana. Tungependa, katika majibu yako, nipate majibu ya hatma ya ujenzi wa Bwawa la Kidunda, upo au haupo? Kama haupo, tuambiwe ili wananchi waendelee na shughuli zao. Tumekwamisha shughuli za maendeleo ya wananchi wa Kata ya Serembala, Kata ya Kidunda, kwa zaidi ya miaka mitano sasa, wakisubiri mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile ningependa nijue wakati Mheshimiwa Waziri wa *TAMISEMI,* mama yangu Hawa Ghasia anachangia, alizungumzia suala la maboresho katika Halmashauri. Lakini vile vile alizungumzia suala la Serikali, kwa hatua ambazo imezichukua kwa Wakurugenzi waliofanya uharibifu wa pesa za Serikali. Wako Wakurugenzi wamefukuzwa kazi, wako Wakurugenzi wamehamishwa na wako wakurugenzi ambao wamepata ajira mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua, wakati sijawa Mbunge, mimi ni Kiongozi wa Chama katika Mkoa wangu, Halmashauri yetu ya Wilaya ya Kilosa, ilikosa pesa kwa sababu ilikuwa imepata Hati Chafu. Sijajua Halmashauri yangu nayo kama itakosa pesa kwa kupata Hati Chafu kwa ajili ya maendeleo. Sababu ambazo *CAG,* amezionesha katika ripoti yake, moja amesema, Serikali, kutokutoa mafunzo yaliyostahiki kwa Watendaji wake. Lakini vilevile ameainisha kwamba, Watendaji wabadhirifu, wezi, waharibifu wa fedha zetu, wanasababisha Halmashauri ipate Hati Chafu. Sasa sisi kama Halmashauri yetu ya Morogoro Vijijini, nayo imepata Hati Chafu katika Mwaka wa Fedha 2010/2011 wakati sisi tunaingia tukiwa kama Wabunge; mimi ninaomba niulize, Je, wananchi wangu watapata hela au hawapati? Lakini kama wanapata, ni kigezo kipi, Serikali, au ni Sheria ipi Serikali, inayoitumia katika kuwahukumu wananchi ambao *CAG,* hakuwataja kwamba, wao wamesababisha Halmashauri yao ipate Hati Chafu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika hili, Wabunge wote, ambao Halmashauri zao zimepata Hati Chafu, lakini wananchi wetu hawahusiki kwa kusababisha Halmashauri zetu zipate Hati Chafu, tuungane kwa pamoja tuishinikize Serikali, iondoe Sheria Kandamizi, ambayo inawahukumu wananchi bila sababu, wakati wezi wetu tunawajua. Ninachotaka kupongeza ni kwamba, Serikali, angalau imeshachukua hatua na sisi kama Halmashauri ya Morogoro Vijijini, tulishalianza hilo, tulishamwomba wenyewe *CAG* aje kwa sababu, ndani ya kipindi kifupi

tulipokuwa Viongozi, tumegundua madudu makubwa ambayo yanafanywa katika Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa heshima na taadhima, kwa wananchi wote wale ambao Halmashauri zao zimepata Hati Chafu, kama Sheria imetungwa na Bunge, Sheria hiyo ni kandamizi, irejeshwe tena Bungeni, tuivunje. Lakini kama Sheria hiyo imetungwa na Watendaji au na baadhi ya pengine Mashirika ambayo yanatupa misaada katika Serikali, sio Sheria stahiki kwa wananchi. Tunawanyanyasa wananchi wetu bila sababu yoyote ya msingi. Tumejipanga sisi kama Wabunge, katika Halmashauri yetu ya Morogoro Vijijini humu na Mama yangu Nkya, Baraza letu la Madiwani, tumejipanga na bahati nzuri mmetuletea Mkurugenzi mpya, tunataka tufanye mambo makubwa kwa wananchi wetu, waendelee kuiamini Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama ataweza kunijibu yeye au labda wakati wa bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula, Serikali imepanga mpango gani katika suala la migogoro ya wakulima na wafugaji? Kwetu sisi wananchi wa Morogoro Vijijini, tuna tatizo kubwa la migogoro ya wakulima na wafugaji. Mwaka jana kwenye bajeti nililia na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu, hata ulipokuja Morogoro wakati wa Nane Nane, tulikaa Kikao cha Ndani na Mkuu wa Mkoa wakati huo alikuwa hayupo na Viongozi wa Chama na Serikali, tulikuomba. Naamini kwa kweli, barua ile ambayo ilitolewa wakati ule ya kusitisha uondoaji wa mifugo,

wavamizi katika Halmashauri za Wilaya za Mkoa wa Morogoro, bado ni kikwazo ambapo wafugaji wanaendelea kutunyanyasa. *(Makofi)*

Mkoa wa Morogoro ni mkoa ambao umetamkwa na Mheshimiwa Rais kuwa ghala la Taifa la chakula. Mkoa wa Morogoro una mito 177 inayotiririka mwaka mzima, kwa kwenye hotuba wafugaji…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa, hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Naunga mkono hoja, lakini ningependa Serikali ijue kwamba tumepiga *yena yena* miezi mitatu, Serikali ikapatikana. *(Makofi)*

**MHE. DONALD K. MAX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nami nijiunge na Wabunge wenzangu katika azma ya kutekeleza mambo yetu ya Serikali ili kukamilisha mipango yote tuliyokwishaiandaa. Kwa niaba ya Wabunge wenzangu kutoka Mkoa mpya wa Geita, naomba awali ya yote niwapongeze wananchi wa Geita, Wabunge wenzangu wote tunaotoka kwenye mikoa inayolima pamba kwa msimamo ambao tumeuweka na nawaomba wakulima wawe na subira. Tulivyokubaliana ni kwamba, kilimo ni uti wa mgongo na wanaumia miezi minane katika kuhangaika na hii pamba. Kwa hiyo, sisi tumeungana kwa pamoja na najiunga na Wabunge wenzangu kwamba bei ya pamba msimamo wetu ni 1,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa pili, nina shida ya Wizara kama mbili tatu, ya kwanza kabisa ni Wizara ya Maji, tuna mradi mkubwa sana katika iliyokuwa Wilaya ya Geita ambayo sasa ni Mkoa wa Geita. Kuna mradi wa shilingi bilioni 15 ambapo Serikali ilikubaliana na mgodi wa dhahabu, mgodi wa dhahabu umeshatoa shilingi bilioni sita, vifaa vyote vimefika, chekeche la maji, *pump* na mabomba yake. Upande wa Serikali kidogo ni tete, toka mwaka jana mwezi wa nne. Sisi Geita tulikuwa tumeahidiwa kwamba *African Development Bank* itatoa msaada wa pesa hizo mpaka leo hazipo, mwaka jana nimefuatilia hazipo na mpaka sasa hivi naangalia vitabu vya bajeti hazipo. Sasa Wizara hii kwa kusema kweli nitatoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapokuja kwenye suala la Wizara ya Nishati na Madini nafikiri hili ni suala la miaka mingi sana, kwa sababu uundaji wa ajira kwa vijana wetu bado ni mgumu na bado ni tete, naipongeza sana na nakipongeza Chama cha Mapinduzi kwa sababu sera zetu ambazo tunajaribu kuziangalia kila baada ya miaka mitano zinatekelezeka. Tulisema tujenge shule za msingi, tumejenga; tumesema tujenge shule za sekondari, tumejenga; leo hii tuko kwenye vituo vya afya pamoja na huduma nyingine ndogo ndogo. Naiomba Serikali tunapokuwa na mikakati hii na mambo mengine tungejaribu kidogo kuyaendeleza mapema. Leo hii tunajenga zahanati na vituo vya afya, kesho tutahangaika kama tunavyohangaika na walimu tunajenga vituo vya afya, tunajenga hizi zahanati

halafu kesho tuanze kutafuta Madaktari na wahudumu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitu kwa kusema kweli ningeomba Wizara husika irekebishe. Ninapokuja kwenye Wizara ya Nishati na Madini, vijana wetu wanajituma sana katika kujitegemea, wanamaliza *form four* hawana ajira, wanamaliza vyuo hawana ajira, lakini wanapofanya kazi zao ndogo ndogo ambazo toka zamani kabla ya viwanda vikubwa vya madini havijaingia nchi hii, zile kazi zao ndogo nafikiri hata ule uharibifu wa miji ulikuwa haupo, vijana wetu wanajitahidi kujitegemea, yale mashimo madogo madogo mpaka leo yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha kushangaza ni kwamba toka Serikali imesema kwamba itawatengea maeneo yao sasa hivi Wilaya kama ya Geita au tuseme Mkoa mpya wa Geita pale Mjini, mjini Geita sasa hivi ni kisiwa cha walemavu kwa sababu ya ugomvi kati ya Polisi, *FFU* na vijana. Kinachotokea ni kwamba, vijana hawa huwa wanachukua yale mawe wanaita *Magwangala*, ambayo yanapatikana baada ya wachimbaji wa migodi kumaliza kutoa *products* zao, hayo mawe huwa wanayatupa, lakini kwenye mkataba wa Tanzania na hii migodi, yaani Serikali ya Tanzania bado haijaruhusu yale mawe yatolewe, hawa vijana wangekuwa wanafanya kazi *very peacefully*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichopo ni kwamba, inakuwa wao wanavizia usiku usiku, giza limeingia, ndio wanachukua yale mawe, askari wakiwakuta ni kutwanga risasi tu. Sasa haiwezekani mimi kama

Mbunge nitawabeba wangapi, sasa hivi janga la hawa walemavu Geita ni kubwa, Wodi namba nane pale kwenye Hospitali ya Wilaya yote ni *Magwangala* tu kila asubuhi kukicha mpaka *magwangala*, unapokuja kwa waganga wa kienyeji sasa hivi wamefanya biashara. *Magwangala* siyo Dokta Kigwangala, samahani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unakuta kwamba, pale sasa hivi kuna waganga wa kienyeji wamejenga jenga vile vibanda vyao vya msonge, kazi yao sasa hivi ni kuunganisha mifupa, maana yake kila leo usiku ni shaba tu inatembea pale. Sasa nitabebaje Wilaya kama ile kwa sababu sasa hao watu, kama nguvu kazi inapotea, ina maana mzigo unanirudia pamoja na Wabunge wenzangu ambao tuko kule, hakuna jinsi hapa na kila tukienda kule wanauliza Mbunge yuko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema kweli naomba Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Nishati na Madini na Waziri Mkuu suala hili analielewa vizuri hata kule Mgusu matatizo ni hayo hayo. Naomba sana Mheshimiwa Waziri na nakushukuru kwamba umekubali kuja Geita mwezi wa Nane na naomba suala hili tulirekebishe ili hizi bajeti zetu tujue nini kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapokuja kwenye masuala ya madai ya Serikali, Geita tunadai, wafanyakazi 456 wanadai milioni 484, suala hili nililileta Utumishi, nimefuatilia Utumishi mpaka leo pesa hii

haijalipwa. Naomba kwenye bajeti hii milioni 484 ambayo ni madai ya toka mwaka 2003, yalipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapokuja kwenye posho za Madiwani na Wenyeviti, naomba Madiwani waongezewe pesa, Diwani mmoja anabeba vijiji vitano sita, ule mzunguko wa kutembelea wananchi lazima ashirikiane na yule Mwenyekiti, Mwenyekiti, hawezi kuendelea kufanya kazi bure ndiyo sababu ubadhirifu unazidi sana kwenye Majimbo yetu. Kwa hiyo, naomba hata wale Wenyeviti, kwa sababu Wenyeviti ndiyo wanaotuandalia kila kitu, kama ni mikutano ya hadhara, ni hao hao Wenyeviji, inapokuja migogoro ya wanafunzi na walimu ni hao hao Wenyeviti; sasa ningeomba Wenyeviti wetu wa Serikali za vijiji tuwajali kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye Wizara ya Afya, naomba sana, najua sana wenzangu wamechangia, naomba turudi *TBS,* hizi dawa zinazotoka *MSD* ziwekewe nembo, tumechoka haiwezekani ukanishushia lori ya tani 40 wiki mbili hela ipo, kwenye Hospitali ya Wilaya, kwenye hizi hospitali nyingine ambazo ziko katikati ya pembezoni. Kwa hiyo, naomba zile zinazotoka Serikalini ziwekewe nembo kama zinavyowekewa vinywaji na vitu vingine, ili kusudi nikikuta kwenye Famasi ya mtu na mimi nijue kwamba hii ni mali ya Serikali kwa sababu sasa hivi wazee wetu wanapata shida kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee vijijini sasa hivi wanakufa tu kwa sababu wanashindwa hata ile asprini yenyewe, kwa hiyo, unakuta gari ikishuka pale, kesho

yake famasi zote mjini Geita zimejaa dawa hizo. Kwa hiyo, naomba sana Serikali itusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusifanye makosa kwenye zahanati na vituo vya afya kama suala la walimu, haiwezekani shule ya sekondari, Wanazengo tumejitahidi, kujenga tunajenga, halafu sasa hivi mnaniachia walimu watatu, wataalam wa *art;* pale kuna maabara, sayansi hakuna; walimu watatu hawawezi kubeba wanafunzi 800, naomba sana Wizara ya Elimu ituelewe kwenye hili, walimu hawatoshi, tumejenga shule nyingi kwa kutekeleza sera ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, lakini ningeomba hayo yaangaliwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, namwita Mheshimiwa Agripina Buyogela, Mheshimiwa Ntukamazina ajiandae, Mheshimiwa Dokta Ndugulile ajiandae tafadhali.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa namna gani ilivyompendeza leo mimi kuweza kusimama mbele ya Bunge letu Tukufu, lakini pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais katika uteuzi mbalimbali alioutekeleza kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hususan kwa kumteua Mwenyekiti wangu wa *NCCR* Mageuzi kuwa Mbunge, lakini pia kumteua Mheshimiwa kaka yangu

*Engineer* Chiza kuwa Waziri wa Kilimo, namshukuru sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma hotuba ya Waziri Mkuu, sina ugomvi kabisa hata kidogo na maelezo ya Waziri Mkuu, lakini naomba nitamke mapema kwamba sitaunga mkono hotuba yake kwa sababu ya ukiukwaji ya utawala bora unaofaywa na watendaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifuatilia *Hansard*, tangu nimeingia humu Bungeni nimekuwa nikipiga kelele kwa maslahi ya wakulima wa Jimbo la Kasulu Vijijini kwa maslahi ya walala hoi, wananchi walionipigia kura wa Mkoa wa Kigoma na Wilaya ya Kasulu kwa ujumla. Lakini tatizo kubwa liko kwa watendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na makusudi makubwa sana ya Mheshimiwa Rais ya kufungua Mkoa wa Kigoma na katika ziara yake ya kuja kuuzindua ujenzi wa daraja la Malagarasi alituasa wananchi wa Mkoa wa Kigoma kwamba leo tukiufungua Mkoa huu mkapata barabara za kuwaunganisha na mikoa mingine, nawaomba muwe makini sana msije mkaanza kuuza ardhi yenu mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda hautoshi na yako mengi nimeandika, nitaomba watendaji wayasome kwa makini kwa maslahi ya wananchi wa Kasulu Vijijini, walinichagua kwa kuniamini na niko tayari kupambana kwa ajili yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mwaka jana niliongelea mkataba ambao ulikuwa umeandaliwa na Halmashauri kwa ajili ya Halmashauri kilichoko Kijiji cha Kagera Nkanda, kitalu cha wanyama, kitalu kile kipo tangu enzi ya mababu zetu, ni hazina ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia wananchi wa Kasulu ili tunufaike nayo. Lakini kuna dhambi kubwa sana inayofanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Serikali imeweka utaratibu mzuri wa utawala bora. Mkasema kila Mbunge atakuwa Diwani ili ashiriki katika vikao vya Halmashauri na aweze kutoa mawazo kwa sababu Mbunge hana Kata wala Kijiji. Mbunge anazunguka katika eneo zima la Jimbo anayajua mengi kuliko Madiwani, hakuna Diwani wa Kata nyingine ambaye atapoteza muda wake kuacha kuhudumia Kata yake aende kwenye Kata nyingine. Lakini leo hii vikao vinaendeshwa, Wabunge hatushirikishwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nimezungumzia mkataba na nimewahi kuandika barua kumwomba Mkurugenzi nipitie huo Mkataba ili na mimi kama Mbunge wa eneo husika nijiridhishe nitoe mawazo yangu, nione ni namna gani huu mkataba tunaotaka kumpa huyu mwekezaji kwenye kitalu cha Kagera Nkanda utatunufaisha wananchi wa Wilaya ya Kasulu. Lakini pamoja na hayo na kuwapa barua bado hawakujibu na nilifuatilia na taarifa hizi Mkuu wangu wa Mkoa anazo. Nilifuatilia lakini hawakunionesha mkataba huo. Matokeo yake kwa sababu walijua nimezungumza Bungeni, walikaa kimya ule mkataba kila kikao ambacho sisi tunahudhuria hawazungumzii huo mkataba. Leo hii tuko Bungeni wameitisha kikao

cha Baraza la Madiwani, wamepitisha mkataba mbovu kabisa wa kumpa mwekezaji uwekezaji miaka thelathini, naomba nitamke mbele ya Bunge hili Mkuu wa Mkoa unanisikia niko kamili gado, Mbunge Kamanda mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitokubali wananchi walionipa dhamana kuja kuwasemea kwenye Bunge tukubali kupitisha mkataba wa miaka thelathini kwa mwekezaji wa kitalu ambacho wanyama wale wako miaka yote. Mwaka jana kumbe wakulima walikuwa wanapigwa ikiwa ni *agenda* ya siri ya Serikali waondoke, wanyanyasike ili wao waende wasaini mikataba isiyokuwa na maslahi na hao wananchi. Naomba katika hotuba hii ya Waziri Mkuu atakapojibu atamke kubadilisha kabisa kusaini mkataba huu ili tujipange kwenda kuupitia. Sisi hatupingani na uwekezaji kwa sababu ile rasilimali ambayo tumeipata na iweze kutusaidia wananchi wa Kasulu. Lakini tunahitaji tupitie huo mkataba ili tujipange vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii tunapiga kelele kila siku kwa ajili ya kusaini mikataba mibovu, mikataba ya madini, mikataba mbalimbali ya wawekezaji ambayo haina tija kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hekta za mwekezaji huyu, hekta ni laki moja na hamsini na saba mia tano na kumi, (157,510) halafu anawekeza miaka 30 tena wanavizia, mimi nilikuwa Diwani 2005/2010 na nilikuwa kwenye Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira nimewahi kwenda kwenye hifadhi tumelala kule siku

mbili tukiwa madiwani tunatembelea eneo hilo, kule porini kule mpaka kuna uwanja wa ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri TAMISEMI, sisi ni akinamama, Mungu ametuumba na moyo wa huruma, naomba tusikubali wananchi wetu, watoto wetu, vizazi vijazo, wakaja kupiga makaburi yetu kwamba wakati mikataba hii inasainiwa? Sisi tulikuwa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na ndugu zangu, nadiriki kusema kwamba wapo viongozi watendaji tunaowaamini huko wanaopata nafasi mbalimbali wanakwenda kujali maslahi yao na siyo maslahi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda karibu unakwisha, naomba niende kwenye afya, Jimbo langu la Kasulu Vijiji lina Kata 19, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, haya nayaongea kuiambia Serikali, kwenye Kamati nilishamwambia Waziri naomba katika Bajeti hii mnifikirie ndugu zangu, siyo tulie kwa kila kitu, tulie barabara, tulie afya, elimu na maji, ni hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu suala la afya, katika Jimbo lenye Kata 19 nina vituo vya afya vinne na katika vituo hivyo vinne, kila kituo hakizidi wahudumu wawili wa afya na sisi ni binadamu, huyu mganga, huyu mhudumu anaweza akaugua wakati wowote, sasa akiugua wakati wowote ni nani anamshikia kituo, matokeo yake ni kwamba

Watanzania akinamama wajawazito wanakufa bila msaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunasema kwamba maisha bora kwa kila Mtanzania, tunaepusha vifo vya akinamama na watoto wakati kituo kina mhudumu mmoja, nina zahanati 29. Katika zahanati 29 nina wahudumu 37 katika zahanati 29, nina zahanati mpya nne, nina zahanati za zamani nne, zahanati nane hazina mhudumu hata mmoja. Ndugu zangu yote hayo yanaletwa ofisi ya Mbunge, mimi niyapeleke wapi? Ukienda kwa watendaji wetu, Wakurugenzi ukifika anakuangalia kama wajuzi, nidhamu haipo kabisa, imepotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nidhamu imepotea na wanayafanya haya sijui kiburi wanakitoa wapi, mimi sijui kwa sababu Katiba imefafanua haya mambo vizuri. Wajibu wa Mbunge uko wapi ili twende vizuri na katika hili naomba nimshukuru Mkuu wangu wa Mkoa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru, muda wako umekwisha, ahsante sana.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Ahsante sana, sitaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Ntukamazina na Mheshimiwa Dokta Ndugulile ajiandae.

**MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana, lakini nasikitika kuona naanza kuzungumza wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo kwa sababu wananchi wa Ngara wamenituma nizungumze akiwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja ya Waziri Mkuu kwa sababu nilishaunga mkono wakati wameleta bajeti yao kwenye Kamati yetu ya Katiba, Sheria na Utawala. Kwa hiyo, naendelea kuiunga mkono lakini tatizo la bajeti ya Waziri Mkuu siku zote kwa upande wa Ngara ni kwamba fedha zinazopangwa za maendeleo haziji zote, zinakuja kidogo na zinakuja kwa kuchelewa na mara nyingine zinachakachuliwa. Kwa hiyo, bado tuna matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nina dakika chache sana na dakika kumi hazitoshi, lakini katika dakika kumi hizo naomba niigawe hotuba yangu katika sehemu mbili. Moja, nitatoa ushauri kwa Serikali na nitarudia ushauri ambao niliutoa mbele ya TAMISEMI, lakini mwenye dhamana ya Wizara hii hakuwepo yaani Mheshimiwa Waziri Mkuu, akishakuja nitatoa ushauri huo. Lakini nizungumze kama mwakilishi wa wananchi wa Wilaya ya Ngara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ngara ni Wilaya nzuri sana, Ngara ni Wilaya tajiri sana Wilaya maskini, ina sura mbili yaani tajiri sana na ni Wilaya maskini na wananchi wa Ngara wamenituma nimweleze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba zile fursa ambazo

Ngara inazo, lakini inahitaji Serikali iwezeshe kutumia fursa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ngara ina ardhi nzuri na ina mvua za kutosha, Wilaya ya Ngara inapakana na nchi mbili za Burundi na Rwanda, kwa hiyo, tuna fursa ya kufanya biashara na nchi hizo na nilishazungumza na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba wakiruhusu tuanze kufanya biashara na nchi ya Burundi na Rwanda lakini pia hatupo mbali na Kongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ngara ina madini mengi sana, wakati Wajerumani wanaondoka waliacha wameandika kwamba Wilaya ya Ngara ndiyo tajiri kuliko Wilaya zote za Tanganyika wakati huo kwa madini, lakini wakianza kuchimba madini hayo sijui watatuhamishia wapi? Sijui watatuhamishia Biharamulo au wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ngara katika madini hayo ina Kabanga *Nikel*, Kabanga *Nikel* ni mgodi mkubwa sana wa pili duniani baada ya ule wa Canada. Sasa ombi la wananchi wa Ngara kwa Serikali ni kwamba Kabanga Nikel wameanza kujenga mgodi na watamaliza katika miaka miwili, nimeiomba Serikali iwezeshe *TANESCO* waweze kuwapa umeme wa kutosha ambapo wanahitaji *megawatt* 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ngara ina maporomoko mazuri makubwa sana ya Rusumo ambayo yanaweza kutoa umeme wa *megawatt* 90 na ni mradi wa nchi tatu. Sasa naiomba Serikali ya Tanzania isije ikakwamisha mradi huo washirikiane na

nchi ya Burundi na Rwanda kukamilisha mradi huo mapema iwezekanavyo ili tuweze kupata *megawatt* 30 kwani kila nchi itapata *megawatt 30.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna nguvu kazi nzuri sana kwani wananchi wa Ngara ni watu watulivu, wakiwa na uongozi mzuri wakahamasishwa wataweza kujiletea maendeleo. Reli ya Isaka tunayoizungumzia ambayo Serikali inataka kuijenga itatoka Isaka, itapita Kyeza, Kyeza iko Ngara na baada ya Kyeza itakwenda Burundi na Rwanda. Kwa hiyo, hiyo nayo ni fursa nzuri ambayo tungependa Serikali itusaidie kuhakikisha kwamba reli hiyo inaanza haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Ngara ni maskini, kwa nini nimesema Ngara ni maskini? Ngara ni maskini kwa sababu ukiangalia kipato cha Mwanangara ambazo ni 170,000/= mpaka 240,000/= wakati kipato cha Mtanzania wastani kwa mwaka 800,000/= unajikuta sasa sisi ni maskini. Ni maskini kwa sababu kilimo chetu ni cha kujikimu kwa sababu bado hatuwezi kununua trekta kwa sababu tunapata fedha kidogo za maendeleo, naomba Serikali itusaidie kwani tunapozungumzia *SAGCOT* kupeleka fedha nyingi sana kwenye Mikoa ya Kusini ambayo ni ya kilimo tunaweza tukasahau Wilaya ambazo zipo nyuma sana kama Ngara tukapeleka fedha zote kwenye *SAGCOT*. Lakini pia nimemwomba Waziri wa Kilimo aiweke Ngara katika orodha ya kupata ruzuku ya pembejeo na amesema atatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ngara ni maskini kwa nini? Elimu bado ni ya chini sana, TAMISEMI mmepewa

kazi ya kusimamia elimu ya msingi na elimu ya sekondari, sina ugomvi nayo tena zamani nilikuwa nasema irudishwe Wizara ya Elimu kwa sababu Wizara ya Elimu ndiyo wenyewe wenye elimu, lakini sisemi kwamba irudi lakini ni kazi kubwa sana kuwekeza katika *Human Resource*. Tumesema katika vipaumbele vya kufikia ile nchi ya ahadi yaani *a promise land* ambayo sijui kama tutaifikia, Mussa ilimchukua miaka 40 sisi tumebakiza miaka 14 kufikia *medium income country* au nchi yetu uchumi wa kati kama utekelezaji haupo hatutafika. Sasa nimetembelea shule zangu zote, nimekuta walimu ni wachache sana, hakuna vitabu wala maabara wala maktaba wala nyumba za walimu, walimu wanakuja lakini wanatukimbia kwa sababu hakuna nyumba. Naomba Serikali itusaidie sana, hii Wilaya ambayo ina kipato cha 170,000/= wakati Kitaifa ni 800,000/= tusiisahau wakati tunakwenda kwenya *SAGCOT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye afya; nina Vijiji 73, lakini nina Zahanati 42 tu, nina Kata 20 na vituo vya afya vinne tu lakini ule mpango wa MMAM ambao ulianza mwaka 2008 ambao unakwisha mwaka 2017 sijui kama nitaweza kuwa na zahanati kila Kijiji na kuwa na kituo cha afya kila Kata wakati kumebaki muda mfupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitembelea Ngara na wananchi wameniambia nimkumbushe kwamba alipokuja Ngara alizungumza kwenye Kijiji cha Mlusagamba akawaahidi wananchi wa Ngara kwamba nitasaidiana na Mheshimiwa Ntukamazina katika kupambana na umaskini, ujinga

na maradhi. Sasa wananiuliza Waziri Mkuu yuko wapi? Nawaambia anakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais alitembelea Ngara akatuahidi umeme, maji na barabara ya lami, wananiuliza Rais yuko wapi? Nikawaambia anakuja, nikawaambia kwamba wawe na subira kwa sababu ahadi za Rais na za Waziri Mkuu ni miaka mitano. Naamini kwamba watatusaidia. Mheshimiwa Waziri Mkuu akumbuke ahadi yake aliyoitoa Ngara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nirudie ushauri ambao niliutoa mbele ya TAMISEMI kwa sababu mwenye dhamana yupo. Kama mtawala wa siku nyingi na kama mtawala wa *Management* nilitumia neno moja nikasema kwamba mfumo wa utawala wa Serikali umeziba, lakini leo nabadilisha hilo neno kuziba nasema mfumo wa utawala wa Serikali una matope na inahitaji matope hayo tuyaondoe ili usije ukaziba. Kwa nini nilisema kwamba, mfumo wa utawala umeziba au una matope? Una matope kwa sababu nashangaa kuna baadhi ya watendaji na baadhi ya viongozi ambao wanakuwa kikwazo katika kutekeleza maamuzi mazuri ya Serikali. Mpango wa Serikali ni mzuri sana na bajeti ya Serikali ni nzuri sana, lakini naogopa kuhusu utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitoa ushauri kwamba suluhu ni kufanya mambo mawili yaani uteuzi kwamba Rais na wale wote wenye mamlaka ya kuteua wawe waangalifu sana katika uteuzi, wateue watu wenye sifa, uadilifu, uzalendo, uwezo ili wasije wakaingia mambo ya udini, ukabila na urafiki

tukishateua watu wazuri. Pia nikasema kwenye uwezo tuhakikishe kwamba tunazingatia *principle* moja ya *management* inayoitwa *Peter Principle* inasema usilazimishe kumpandisha cheo mtu au kumpa kazi mtu ambayo hana uwezo nayo. Ukishafanya hivyo atakuwa kituko au chini, atakuwa kituko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba sana watu wenye mamlaka ya uteuzi wateue watu wazuri. Wakishateuliwa nashauri kwamba wawekwe kwenye Mikataba ya Utendaji yaani *Perfomance Conctracts*, Rais aweke Mawaziri kwenye *Perfomance Contracts* au kwenye mikataba ya utendaji. Hivyo hivyo na Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na kadhalika. Tukishafanya hivyo ndiyo tutaweza kuwa na mfumo mzuri wa kuwawajibisha watu. Nisingependa tena Bunge hili limlazimishe Mkuu wa Nchi na Mheshimiwa Rais wetu kuwawajibisha Mawaziri, tuwe na mfumo endelevu, Rais awe na mfumo ambao anapima utendaji kazi wa Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa na Ma-*DC* ili aweze kuwaondoa wale ambao hawana uwezo, asiogope kuwa-*fire* kwa sababu ukiwa na mamlaka ya kuteua ni lazima uwe na mamlaka ya ku-*fire,* yaani *hire and fire*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusimweke Rais katika hali hiyo. Naomba sana hii ndiyo Wizara yenyewe na ambayo ndiyo Serikali yenyewe yaani Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tuhakikishe kwamba Watendaji wanawajibika na wanawekwa kwenye mikataba yaani viongozi pamoja na watendaji na siyo kuwaweka kwenye mikataba na mikataba ikawekwa kwenye *shelf*. Iwe kila baada ya miezi sita

Rais anakaa na Mawaziri wake anaangalia kama kwenye mikataba ile yale malengo waliyowekeana wameyafikia? Hivyo hivyo na kwa Wakuu wa Mikoa. Huo ndiyo ushauri ambao niliutoa wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu na nimefurahi kwamba yupo, ninachoomba ni kwamba tuwaweke watendaji kwenye mikataba ya utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Dakitari Ndugulile na Mheshimiwa Habibu Mnyaa ajiandae.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia. Nianze kwa kutoa pongezi kwa watu watatu yaani Katibu Mkuu Ndugu Peniel Lyimo, Mama Nanai na Mzee John Cheyo wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kazi kubwa na nzuri kwa kushirikiana pamoja na mimi kuhakikisha kwamba fidia ya wahanga wa mabomu katika eneo la Mbagala inalipwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe, lakini nimeshaanza kupata malalamiko ya wananchi kwamba utaratibu ambao unatumika kuwalipa fedha wahanga hawa si mzuri, wananchi wameshaanza kuhangaishwa. Tumefanya kazi kubwa ya kuzitafuta hizi fedha na kuzifikisha kule kwa wahanga lakini Uongozi wa Mkoa na Uongozi wa Wilaya hawajajipanga vizuri wanawaletea bughudha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nataka nichangie kwa ujumla suala zima la elimu na afya. Mfumo tuliokuwa nao pamoja na ugatuaji wa madaraka katika sekta ya elimu na afya si mzuri inabidi tuuangalie upya. Sekta hizi mbili zinapaswa kuwa ni vipaumbele vya kudumu. Migomo ambayo tunaiona katika hizi sekta kwa kiasi fulani zinachangia na mfumo tuliokuwa nao. Inapaswa tukae tuangalie upya na sisi kama Kamati ambayo inasimamia sekta ya afya na elimu tupo tayari kuwashauri njia bora zaidi ya kuliangalia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaunga mkono bajeti hii na nitatoa sababu kwa nini siungi mkono bajeti hii. Mnamo tarehe 16/8/2011 katika bajeti hii na naomba kunukuu kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu akisema na nanukuu:

"Mheshimiwa Naibu Spika, yapo masuala mazito mazito mengine nimeyasikia atayazungumza..." akimaanisha Mama Tibaijuka. "Lakini naomba mimi kama Waziri Mkuu niyasemee kidogo na hasa hili la Kigamboni na maeneo mengine ya Dar es Salaam ina pilika nyingi sana, nichukue tu dhamana ya kumsaidia Waziri kwa ukubwa wa matatizo ya ardhi yalivyo, sisi tutakachofanya ni kumsihi tu pengine baadaye tukipata nafasi Wabunge wale wote wa Dar es Salaam si vibaya tukakaa pamoja. Hebu tulizungumze jambo hili tuone matatizo yalivyokaa, tuone tunaweza tukafanya nini kupunguza matatizo yanayozunguka masuala ya ardhi katika Mji wa Dar es Salaam, Dar es Salaam ni eneo dogo ndiyo maana mnaona

tunagombana kweli kweli. Tusipojipanga vizuri haitatuletea amani hata kidogo. Kwa hiyo, niko radhi na nitamwomba Waziri naye alipe uzito, nadhani tukikaa na Wabunge hawa tunaweza kabisa tukamaliza vizuri." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kauli ya Waziri Mkuu na alituahidi ndani ya wiki mbili baada ya Bunge la Bajeti kumalizika atakaa na Wabunge wa Dar es Salaam lakini mpaka tunavyoongea hivi sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu hajakutana na Wabunge wa Dar es Salaam. Si kwamba hatukumkumbusha, tulimtuma Mwenyekiti wetu zaidi ya mara tatu tukimwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kukutana na Wabunge wa Dar es Salaam. Tumeomba kupitia wasaidizi wake tukutane na Waziri Mkuu lakini hatujafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam tuna matatizo mengi, kuna suala la UDA. Shirika hili limetolewa bure, sasa hivi mali zake zinauzwa na kutapanywa, viwanja vinauzwa, nyumba zinauzwa, kuna madepo yanauzwa na tunaambiwa kwamba kulikuwa na Tume ambayo iliundwa na Waziri Mkuu kuliangalia suala hili, *report* hii hatujaipata, wananchi wa Dar es Salaam wanauliza *report* hii ipo wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala la Jiji la Dar es Salaam. Jiji la Dar es Salaam lilivunjwa lakini juzi hapa tena likarejeshwa lakini nasikia tena kuna mchakato wa kulivunja tena. Je, mmekaa na Wabunge wa Dar es Salaam ambao wanawawakilisha

wananchi wa Dar es Salaam kuwauliza wanataka nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mji mpya wa Kigamboni, kwa kweli niseme tu kwamba Serikali inafanya mzaha na suala hili, lakini suala hili ni kubwa. Wananchi wa Kigamboni wamekuwa wanataabika kwa muda wa miaka minne na mpaka sasa hivi Serikali imeshindwa kutoa majibu ya msingi. Tulitarajia kwamba Waziri Mkuu na Waziri husika atakaa na Wabunge wa Dar es Salaam tuweze kukaa na kujadili lakini kwa sababu inaonekana kwamba Serikali imelipuuzia suala hili basi na sisi tutaamua tutakavyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala ya fidia ya barabara za Dar es Salaam na mimi hapa nitagusia barabara ya Kilwa. Serikali hii alipokuwa Waziri Shukuru Kawambwa aliwaahidi wananchi wa maeneo ya Temeke na Kigamboni kwamba watalipwa fidia, wavute subira. Alipoingia Waziri Magufuli akasema kwamba hatawalipa fidia na Mheshimiwa Waziri Mkuu hili suala nilikufikishia, iweje Serikali ile ile moja kuwe na kauli zaidi ya mbili? Masuala hayo yote tulikufikishia na mpaka sasa hivi hatujapata majibu na wananchi hawa wamekuwa wanalifuatilia na sasa hivi wanataka kuipeleka Serikali Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kivuko, Serikali ilipandisha bei ya kivuko cha Feri na hili nalo Mheshimiwa Waziri Mkuu tulikufikishia pamoja na kukuandikia barua tarehe 3 Januari, tarehe 13 Januari na kuonana na wewe ana kwa ana tarehe 19 Januari tukakubabidhi barua na mapendekezo ya wananchi

wa Kigamboni. Mpaka sasa hivi Mheshimiwa Waziri Mkuu barua zangu hazijajibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunakuja na miradi ya *open Government*, sasa kama tunashindwa kujibu hata barua hata kuitana, kukaa na kuongea sasa hii *open Government* tunayoiongelea ni *open Government* ya namna gani? Ni bora tutoe hizo fedha tukaenda kuziweka katika masuala ya madawati na kuongeza masuala ya madawa, bado hatujafikia *level* ya kuwa na *open Government*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala ya msongamano Dar es Salaam, sasa hata katika bajeti hii hatuoni kwamba hivi vitu vinapewa kipaumbele. Mkazi wa Dar es Salaam *on average* anapoteza masaa mawili kwa kila safari yaani masaa manne kila siku. Sasa sisi ndiyo watu wa Dar es Salaam ambao kwa kweli na sisi inatugusa, uchumi wa Dar es Salaam unadumaa kutokana na msongamano wa barabara zilizokuwepo. Tulitarajia kwamba Mheshimiwa Waziri ungekutana na sisi na sisi tukatoa mapendekezo yetu ya kusaidia jinsi gani ya kusaidia hiki kitu. Lakini yote hayo hayajaweza kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa Mbunge takriban miaka miwili lakini miaka yote miwili pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mkazi wa Dar es Salaam lakini hatujawahi kumuona hata kumsikia siku moja akifanya ziara katika Mkoa wa Dar es Salaam. Wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam tumekuona umekwenda Mabwepande, tumekuona katika masuala ya mafuriko lakini hatujawahi kukuona

Mheshimiwa Waziri Mkuu ukifanya ziara katika Mkoa wa Dar es Salaam. Wananchi wa Dar es Salaam wanahoji kwamba wamekukosea nini Mheshimiwa Waziri Mkuu? Kwa nini Mheshimiwa Waziri Mkuu unawafanya wananchi wa Dar es Salaam waonekana wanyonge ilhali na wewe ni mkazi wa eneo lile? Hebu basi panga muda hata kama hutaki kuonana na Wabunge wa Dar es Salaam basi uende ukawatembelee wananchi ili kuwatoa unyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nimalizie hapo sitataka kumaliza muda lakini kwa kweli pasipo na majibu ya kina katika hizi hoja kwa kweli kwetu itakuwa ni ugumu sana, kwa kweli Wabunge wa Dar es Salaam tumesema kwamba hapana, hii bajeti hatuiungi mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia hapo.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa na kwa ku-*balance* vyama Mheshimiwa Christowaja Mtinda ajiandae.

**MHE. MOHAMMED HABIBU JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi. Kwa kuwa, sifa wameshasifiwa wengi na kupongezwa kanuni haziruhusu, iliyobakia ni wananchi wa Mkanyageni tu wanivumilie kwani nipo kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite moja kwa moja na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu hali ya uchumi. Nasikitika sana na maelezo yaliyopo hapa,

amesema kwamba, hali ya uchumi mwaka 2011 imekuwa kwa 6.4%, lakini akalinganisha na mwaka 2010 ambapo uchumi ulikuwa kwa nukta saba. Sasa huku kwa ufupi ni kwamba, siyo kukua bali umeshuka kwamba mwaka 2010 ilikuwa 7% na mwaka 2011 ni 6.4%, ni kushuka na siyo kukua. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, katika hapo panalinganishwa na nchi za Kusini mwa Afrika kwamba uchumi wao unakua kwa asilimia 5.1, hili ni tatizo lingine, ukiacha nchi kama mbili hizo nchi za Kusini mwa Afrika hiyo asilimia 5.1 iweje leo wenye asilimia 5.1 wanakula milo mitatu, wanaishi vizuri, siye wenye asilimia nyingi hali iwe kama hii? Kuna tofauti kubwa kati ya tafsiri ya uchumi wa kwenye makaratasi na hali halisi. Huo ulinganifu wetu inaonekana kuna kasoro *somewhere*. Huko wenzetu wenye asilimia tano wanakwenda vizuri, lakini sisi wenyewe asilimia sita tunaiona hali ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu ninukuu kwanza katika Bajeti ya mwaka 2011/2012, Serikali ilisema hivi: "Serikali inatambua changamoto zinazowakabili wananchi katika kupambana na makali ya maisha. Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa 2011/2012, pamoja na mambo mengine inalenga katika kuchukua hatua za kurekebisha hali hiyo." Hii ni bajeti ya mwaka jana, lakini mwaka mwingine ndiyo umefika, hali inaonekana sasa. Mfumuko wa bei mwezi Juni mwaka 2011 ulikuwa asilimia 10. Mwisho wa mwaka huo wa 2011 ilikuwa asilimia 20. Mei mwaka huu umeshuka mpaka asilimia 18, sababu zinazoelezwa ni hizo hizo za ongezeko la bei ya mafuta katika soko al dunia na ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi sababu tumeelezwa na zimeshatutosha kwa sababu dunia nzima tunajua suala la ukame, tabianchi, zaidi ya miaka mitano au sita iliyopita, leo ni vipi tuje na sababu hizo hizo? Hizo nchi za Kusini mwa Afrika zinazozungumzwa wana matatizo ya ukame na soko la mafuta ndiyo hilo hilo. Lakini la ajabu ni kwamba mwaka jana wakati bajeti inapitishwa pipa moja la mafuta lilikuwa dola za Kimarekani 120, lakini baadaye mafuta yamepungua na hadi mwanzoni mwa mwaka huu ilishuka mpaka chini ya dola 100 zaKimarekani, lakini mfumko wa bei bado uko juu na hasa katika bei ya vyakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili suala litafutiwe ufumbuzi. Visingizio vya soko la mafuta, ukame na hizo nchi nyingine zote tunaishi katika hali ya hewa sawa. Hali ya hewa ni *global issue,* siyo *issue* ya Tanzania tu. Hivi ni visingizio ambavyo havifai Wabunge kuelezwa kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nizungumzie ukurasa wa 28 wa hotuba hii ya Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Kuna hili suala la chenji ya rada. Maelezo mazuri yametolewa ya Paundi milioni 29.5 kwamba asilimia 75 ya fedha hizo ambayo ni bilioni shilingi 54.2 itakwenda kwenye vitabu na asilimia 25 ambayo ni bilioni 18.1 itakwenda kwenye madawati. Swali hapa ni kwamba, kwa nini Mheshimiwa Waziri Mkuu ofisi yako inahusika katika kuongeza matatizo ya Muungano? Hizi fedha zilikuwa ni za Serikali ya Tanganyika iliyojificha katika koti la Muungano au ni fedha za Jamhuri ya Muungano?  Rada ilikuwa ni ya

nani, si ya Jamhuri ya Muungano? Sasa iweje leo Mheshimiwa Waziri Mkuu uhusike katika ofisi yako fedha hizi zisisaidie chochote Zanzibar, zote zitumike upande mmoja wa Jamhuri? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya Muungano tuliyonayo ni lukuki na bado yanaendelezwa. Tuna matumaini, Katiba mpya hiyo hapo inakuja yapungue, lakini kabla hatujapata Katiba mpya bado yanaendelezwa! Bajeti hii hatuna haki ya kuipitisha kama hatujaona fungu la Zanzibar, kwamba katika chenji hii ya rada ni kiasi gani kinapelekwa huko? Matumizi wanayo na wanajua namna gani ya kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ofisi yake isiwe chanzo cha kuongeza matatizo ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye malengo la Milenia. Kutokana na haya matatizo ya bajeti na ukweli wa mambo, hizi bajeti zetu tatizo ni nini? Tatizo bajeti ya Kilimo, Uvuvi, zaidi ya miaka 10 iliyopita haijapata angalau asilimia tano (5%). Leo kuna makubaliano ya *SADC countries,* Tanzania imesaini na inahusika kwamba, angalau bajeti ya Kilimo ifikie asilimia kumi ya matumizi ya Taifa. Kwa nini tunasaini mikataba halafu tunashindwa kuitekeleza? Kwa nini tuendelee na mfumo wa bajeti wa namna hiyo? Kwani ni lazima kuwe na *projects* 100 au 1000 kila mwaka? Hatuwezi kuzipunguza au lazima tuendelee na mfumo wa bajeti wa kikoloni? Hatuwezi kupanga vipaumbele vichache

tukavitekeleza kwa fedha tuliyo nayo? Hili ni tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la makubaliano ambayo ni ya *SADC* ndiyo sasa sawa na yale makubaliano ya kuanzisha Mfuko wa Muungano uliotajwa. Kumbe chanzo ni huku huku ndiyo kwenye matatizo, Jamhuri hii hii ndiyo inayoleta matatizo kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la malengo ya Milenia leo hapa ninayo *latest document* ya *UN.* Muda ungekuwepo ningeyasoma yote, lakini kuna viashiria vya mambo manane (8) ambayo hayawezi kutekelezeka. Yaliyoweza kutekelezeka ni mambo saba na pengine mambo matano ndiyo yanaweza kufikiwa. Muda ungekuwepo ningeyasoma yote, lakini malengo ya milenia ambayo tuliahidi kwamba mwaka 2015 yatafikiwa, hayawezi kufikiwa. Hili ni tatizo lingine na chanzo kinakuja palepale, mpango wa bajeti yetu na vipaumbele vyetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze suala dogo hili la wachimbaji wadogo wadogo wa Mgusu na hili linamhusu Mheshimiwa Waziri Mkuu moja kwa moja. Tarehe 2 Aprili, 2009 Mheshimiwa Waziri Mkuu alitembelea Mgusu kwenye ule mlima ilipotokea ajali na kwa kauli yake nanukuu alisema, “Sina mahali pengine pa kuwapeleka wachimbaji wa Mgusu.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pale pakafungwa kwa miezi mitatu, leo ni miaka mitatu hapajafunguliwa na wananchi wale wanahangaika. Lakini acha hilo

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri katika kampeni tarehe 29 Oktoba, 2010 akifuatana na aliyekuwa wakati ule Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Ngeleja alitoa ahadi akasema: "Nyarugusu, Rwamgasa, Mgusu wapewe wachimbaji wadogo wadogo". Inakuwaje leo ni miaka mitatu wachimbaji wale wamefungiwa mtaji wao, hawana pa kukimbilia na kauli za Mheshimiwa Waziri Mkuu haziendani na kauli ile? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba wakati wa kuhitimisha bajeti hii Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe kauli wale maaskari wapo pale mlimani hawajaondoka na hakuna sababu wananchi wasipewe pale wakati mliishatoa ahadi! Yeye ametoa ahadi na Mheshimiwa Rais ameshatoa ahadi, kwa nini isitekelezwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo lingine dogo, haya mambo yote tunaweza tukayalinganisha na mambo haya ya nchi yanavyokwenda. Kuna hii ripoti ya Mo Ibrahim (*Ibrahim Index*) hii hapa ya mwaka 2011. Hii ripoti ukiangalia yapo mambo mengi yanayohusiana na usalama na utawala wa sheria, ushirikishwaji wa haki za binadam, fursa za uchumi endelevu, maendeleo ya binadamu. Ukiangalia hii ripoti Tanzania katika mambo ya usalama na utawala wa sheria ni nchi ya 18 kati ya nchi 53. Ziko nchi za Mauritius, Botswana, Cape Verde na Namibia, zinaongoza kwa kuwa katika kumi bora, Tanzania tuko katika nafasi ya 18. Hii ni kuhusiana na utawala na usalama wa sheria. Kwa hiyo, lazima tutambue kosa letu ni nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, acha hiyo. Ukienda kwenye ushirikishwaji wa wananchi, hapa ndiyo Tanzania angalau tuko katika nafasi ya 11. Ukienda katika suala la *stable economy opportunity* angalau Tanzania tuko katika nafasi ya 11, lakini tunafanya vibaya sana katika masuala ya *human development* (maendeleo ya watu) tuko katika nafasi ya 27 kati ya nchi 53. Hili ni tatizo na haya yote yanaendana na haya mambo ya bajeti na uchumi wetu unavyokwenda. Ni lazima tujikwamue katika *stage* hii, tusikubali angalau tukisema nchi yetu haina amani na utulivu basi tuwekwe katika ile kumi bora. Amani na utulivu halafu tunakuwa watu wa 27 na 18, nini! Sasa amani na utulivu uko wapi namna hiyo? Tujikaze tuendelee ili tulete ule utawala bora kwa kiwango cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda unakwenda, lakini la mwisho labda ili nisije nikagongewa kengele, kuna Tume ya Katiba ambayo Mheshimiwa Rais aliizindua mnamo mwezi Aprili mapema pale. Kwa mujibu wa hadidu za rejea na kwa mujibu wa *timeframe* ina miezi 18 ya kukamilisha kazi. Sote tunatamani uchaguzi wa mwaka 2015 tuwe na Katiba mpya. Lakini inaonekana wana uhuru wa kuanza kazi hizo, yaani hii *gape* ya miezi mitatu kwanza wako *silent* wanajipanga panga. Hilo ni jambo ambalo halikutakiwa liwepo. Sasa hivi napata taarifa kwamba wamekwishaanza kufanya kazi, lakini je, kwa ugumu na matatizo yaliyopo miezi 18 watakamilisha kazi yao? Ikiwa hawatakamilisha kazi yao ni nini cha kufanya? Ni lazima hivi sasa iletwe sheria ibadilishe Tume ya Uchaguzi kwa sababu haiaminiki…(*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi kuwa mmoja wa wachangiaji katika hotuba ya Waziri Mkuu. Mimi nitachangia kwa upole kabisa ili Serikali iweze kunielewa, kwa sababu ukichangia kwa jazba inawezekana utakosa hata pointi na vitu vingine hutaeleweka.

Nianze moja kwa moja kutokana na muda mchache wa dakika kumi (10) labda tu niseme kwamba, tumekuwa tukizungumzia Kilimo kwa aina tofauti sana humu ndani. Tumezungumzia kwamba kilimo hakipewi fedha ya kutosha, kilimo hakithaminiwi, fedha ni chache, lakini hatujaweza kuangalia kwamba hata hizo fedha chache zinazotengwa kwa ajili ya kilimo zimefanya kazi gani. Ukiangalia hata hizo fedha chache zinazotengwa kwa ajili ya kilimo na zenyewe nazo zimeliwa. Kwa hiyo, Wabunge tunapozungumza kwamba kilimo kiendelee kupewa fedha nyingi ina maana kwamba walaji waendelee kula kwa bidii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hapa hamna mtu asiyefahamu kwamba wananchi wengi wa Tanzania, karibu asilimia themanini (80%), lakini tunachotakiwa kukizungumza ni kile ambacho kipo na kiweze kutekelezeka. Naongea mara chache sana Bungeni, lakini naishukuru Serikali kwamba, vingi huwa inavifanyia kazi. Kwa vile naongea kwa upole nafikiri

Mheshimiwa Waziri Mkuu naye ataona huruma na atatekeleza haya ninayoyazungumza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika ukurasa wa 23 wa hotuba yake mwenyewe Waziri Mkuu, sitaki kutoka nje ya hotuba yake, naomba nimnukuu; "Itakumbukwa kwamba Serikali kupitia SUMA JKT iliingiza nchini matrekta makubwa 1,860 na zana zake." Sasa mpaka leo haya matrekta Wabunge wote hapa ni mashahidi, mkipita pale Kilimo Kwanza yapo mamia ya matrekta hayanunuliki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikikumbuka wakati nikiwa bado mdogo mwaka 1984 na nikiangalia katika kumbukumbu aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Chrisant Mzindakaya, alipata msaada wa matrekta 400 lakini yote yalikwisha na kulikuwa na waombaji zaidi ya 2000 ndani ya mkoa mmoja. Sasa hapa kuna matrekta 1,860, lakini matrekta haya mpaka sasa hivi hayanunuliki. Pamoja na juhudi Serikali na naishukuru kwa kushusha bei, kwa mfano, hili trekta la *HP* 50 limeshushwa bei kutoka milioni 25.6 hadi milioni 16, trekta la *HP* 70 limetoka milioni 45.8 hadi milioni 38.8 na kuna lingine hapa kwa sabahu nimefanya *research*, amelisahau Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni la *two wheels drive (2WD)*, hili limetoka shilingi milioni 40.5 mpaka shilingi milioni 32.5 lakini bado haya matrekta hayanunuliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini haya matrekta hayanunuliki? Hapa ni lazima tujiulize. Kwa mfano, hapa Dodoma matrekta haya yanatakiwa yauzwe Morogoro, Manyara, Singida, Dodoma, Tabora,

Shinyanga mpaka sehemu nyingine kama Mwanza, Musoma, lakini bado matrekta yamejaa pale. Naishauri Serikali mambo yafuatayo:-

Moja, ni lazima ihakikishe kwamba *down payment* inayotumika sasa hivi isiwe hiyo. Sasa hivi ili kupata trekta hili pamoja na kushusha bei hamna mtu atakayeweza kulinunua kwa sababu unatakiwa ulipe *fifty percent*. Sasa kwenye milioni 38 kuna mkulima gani mwenye nusu ya hiyo fedha? Ni mkulima yupi mwenye hiyo fedha, *fifty percent*? (*Makofi*)

Halafu baki hapo tena, unapewa mkopo wa miaka miwili, ni trekta gani litakalolipa mkopo huo kwa muda wa miaka miwili? Serikali imekiri kwamba matrekta haya ni yake, ukiangalia hapo hapo una Mfuko wa Pembejeo. Mfuko huu unakopeshwa trekta unatoa asilimia 20 na unalipa baada ya miaka sita (6). Sasa kuna mifuko miwili hapo hapo ya Serikali, lakini iko tofauti. Kwa hiyo, tunaomba badala ya kulipa asilimia hamsini 50 mkulima alipe asilimia 25 na badala ya kumpa miaka miwili ya kulipa alipe baada ya miaka minne mpaka mitano. Kwa sababu unapomwambia mtu alipe kwa miaka miwili asilimia kubwa ya ukulima wa nchi yetu hii unategemea mvua siyo umwagiliaji. Ni msimu wa mvua, unapompa miaka miwili kama katika miaka yote miwili mvua haijanyesha au mwaka mmoja mvua imenyesha na mwaka mwingine haijanyesha unataka ukamnyang'anye? Si unataka umdhulumu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu mpango uliowekwa ili mkulima akopeshwe ni lazima aende kwa

Mkurugenzi wa Wilaya, akasaini zile fomu na hawa Wakurugenzi walivyokuwa na roho mbaya hawasaini. Halafu tena unataka aende na hati ya nyumba, vitu vingi, haiwezekani vitu kama hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mkurugenzi wa Wilaya atumike kumtambua yule mkulima na yeye apate barua kutoka kwa Mtendaji wa Kijiji huko, kwa watu wa chini yake, amtambue tu na dhamana ya mkulima iwe trekta lenyewe. Usitafute sijui shamba lake au nyumba yake, la sivyo mtakopesha hapa watu wenye fedha tu. Kwa upole kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo ndiyo hali halisi. Kama mtu anakopeshwa lori lenye thamani ya milioni 150, anakopeshwa basi lenye thamani ya milioni 500 analipa asilimia 20 na bado lori au basi ambalo linaweza likatumika miaka miwili likawa limekufa kabisa linajidhamini lenyewe itakuwa trekta ambalo linakaa zaidi ya miaka 15 na tayari pale umekwishamwekea *instalment* ya kulipa kila baada ya miezi sita? Kwa hiyo, utamwangalia pale, je, kila miezi sita analipa au halipi ili ujue kama anakwenda vizuri au la? Kwa hiyo, hapo ndiyo kumkomboa na tuzungumzie kitu kiko pale, la sivyo hawatanunua matrekta yale na matairi yatapasuka kutokana na jua, halafu tunajisifia tunaleta matrekta yanakuwa urembo. Mimi hiyo hapana! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kingine, hii Benki inayokuja ya Maendeleo ya Kilimo. Hii benki tunaisifia na kuipigia makofi kwa mbwembwe, lakini tujiulize hii benki itakuwa wapi? Je, itakuwa tena Dar es Salaam

kama ilivyokuwa *TIB* kule kule watu wengi wanakopenda kukaa au itakuwa katika kila kanda au kila mkoa ili kila mkulima aifikie? Maana yake hatuwezi kuweka benki Dar es Salaam halafu mtu atoke sijui Kigoma, Mwanza, Same huko, Gairo au wapi aende kule, haiwezekani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uanzishwaji wa hiyo benki, umemuandaaje mkulima ili akopesheke? Maana yake hakuna benki yenye urafiki na mtu maskini. Benki ina urafiki na mtu tajiri. Sasa umemuaandaaje, maana yake lazima umuandae ili akopesheke. Kama ni shamba lake kwa sababu ndiyo raslimali anayotegemea, umempa hati? Kama ni nyumba yake, umempa hati? Au tunaanzisha tu ili wajanja waende wakale zile fedha? Eeh, maana yake lazima tuangalie, tumeleta hizi hati za kimila zimekuwa za kisanii sanii tu. Ukitaka mwana kijiji apimiwe ili apate ile hati ya kimila ni lazima aende Wilayani achukue Afisa Ardhi ina-*cost* milioni mbili mpaka mbili na nusu (2,000,000 – 2,500,000). Sasa huyu mtu anashindwa kumpeleka mtoto wake kwenye shule ya Kata kwa shilingi 20,000 leo aje atoe shilingi milioni mbili ya kupimiwa ardhi! Jamani tusiwe tunazungumza vitu ambavyo havitekelezeki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema naiunga mkono hotuba hii na najua Waziri Mkuu ni mtu msikivu. Muweke masharti nafuu ya ukopeshaji kwa wakulima. Hata hiyo benki kama hamuwezi kuwapimia maeneo, kwa sababu yatakuwa ni makosa ya Serikali, basi muwape tu mikopo bila hata hati. Kwa sababu yatakuwa ni makosa yenu kwamba, hamjawapimia

ardhi, wapate haya matrekta. Kwa mfano, toka nazaliwa kwenye Jimbo (Wilaya ya Gairo sasa hivi) haijawahi kupata ruzuku ya aina yoyote kuhusu kilimo. Hizo vocha zenyewe zilikuja Gairo hatutumii mbolea, wamechukua wajanja wameziuza, sasa hivi ni mwaka wa pili hazijakuja. Hata siku moja mkulima wa Gairo hapati chochote. Hapati ruzuku ya mbolea, mbegu, wala chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mahindi yote mnayosikia yanaitwa mahindi ya Dodoma, yanatoka Gairo, Kongwa na Kiteto tu. Hao ndio wanaolima. Lakini hamna chochote, isipokuwa akilima akipata unaanza kumpangia masharti. Akiuza mahindi mabichi unamwambia wewe usiuze, nchi itaingia kwenye njaa. Akipata mnunuzi kutoka Kenya au sehemu nyingine, unamwambia usiuze, nchi itaingia kwenye njaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia kwenye spika hii nasema mkulima anachopata, anachotaka hata kama ni kuuza mahindi mabichi aachwe auze tu, hakuna msaada wowote anaoupata.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Muda wetu umekwisha. Tuna dakika chache kama tatu au nne vile. Napenda kabla ya kuahirisha nitoe matangazo mawili: Kwanza Mheshimiwa Sara Msafiri, Katibu wa Wabunge wote wa Mkoa wa Morogoro anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wa mkoa huo kwamba, saa 2.00 usiku baada ya kuahirisha hapa wakutane katika Ukumbi wa Msekwa.

Tangazo la pili, naomba niwataje ambao watachangia kesho baada ya kipindi cha maswali na majibu ili wapate nafasi ya kujiandaa zaidi. Hao ni Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, pia Mheshimiwa Dunstan Mkapa na Mheshimiwa Daktari Mary Mwanjelwa watachangia kesho.

Baada ya matangazo haya, naomba kuahirisha shughuli hizi mpaka kesho saa 3.00 Asubuhi.

*(Saa 1.44 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano Tarehe 27 Juni, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*